Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

# BUNGE LA TANZANIA

## MAJADILIANO YA BUNGE

### MKUTANO WA NNE

**Kikao cha Kumi na Nne – Tarehe 28 Juni, 2011**

*(Mkutano Ulianza Saa Tatu Asubuhi)*

**D U A**

*Spika (Mhe. Anne S. Makinda) Alisoma Dua*

**MASWALI NA MAJIBU**

Na. 130

**Ujenzi wa Madaraja ya Mito ya Mongo – Obakima na Waku – Luba**

**MHE. LUHAGA J. MPINA** aliuliza:-

Ujenzi wa madaraja ya Mto Mongo – Obakima na Mto Waku-Lubiga ni muhimu sana kuliko wakati mwingine wowote uliopita kwa ajili ya shughuli za maendeleo na uchumi na Mheshimiwa Rais kwa kulitambua hilo, wakati wa Kampeni za Uchaguzi Mkuu, 2010 aliwaahidi wananchi wa Mwambusu, Mwanduitinje, Mwagayi, Itinje, na wale wa Lingeka, Mwabulutango, Mwamhongo, Mwamasengele kuwa madaraja hayo yatajengwa haraka sana katika Bajeti ya kwanza ya Serikali.

Je, Serikali imekwishatenga fedha kwa ajili ya ujenzi wa madaraja hayo muhimu katika Bajeti ya 2011/2012?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu naomba kujibu swali la Mheshimiwa Luhaga J. Mpina, Mbunge wa Kisesa, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kuwa wakati wa Kampeni za Uchaguzi Mkuu, 2010 Mheshimiwa Rais aliahidi kujenga madaraja katika jimbo la Kisesa. Mojawapo ya ahadi ambazo Mheshimiwa Rais alizitoa ni kusaidia ujenzi wa daraja katika mto Mongo – Obakima, katika jimbo la Kisesa.

Mheshimiwa Spika, katika kutekeleza ahadi ya Mheshimiwa Rais, Halmashauri ya Wilaya ya Meatu, imefanya upembuzi yakinifu ambapo gharama za ujenzi wa daraja la Mongo Mwarabu kwenye barabara ya kutoka Nkoma (Kata ya Nkoma) – Mwangudo - Makao (Kata ya Mangudo) katika jimbo la Meatu ni shilingi milioni 426.5. Katika Bajeti ya mwaka 2010/2011 Halmashauri iliidhinishiwa kiasi cha shilingi milioni 350 kwa kazi hiyo. Halmashauri imepokea fedha kiasi cha shilingi milioni 139 na shughuli za ujenzi wa daraja hilo zinaendelea baada ya kupatikana kwa Mkandarasi.

Mheshimiwa Spika, katika Bajeti ya mwaka 2011/2012 Halmashauri ya Wilaya ya Meatu imeidhinishiwa sh milioni 76. 5 ili kukamilisha ujenzi wa daraja hilo. Ukamilishaji wa daraja hilo utasaidia kuboresha mawasiliano ya barabara hiyo inayopita katika Hifadhi ya Wanyamapori ya Maswa *(Maswa Game Reserve)* na kuunganisha Mkoa wa Shinyanga na Mkoa wa Arusha kupitia Wilaya ya Ngorongoro.

Mheshimiwa Spika, Halmashauri ya Wilaya ya Meatu imeanza kufanya upembuzi yakinifu wa daraja la Mongo – Obakima, ili kupata makadirio halisi ya gharama za ujenzi wa daraja hilo na kutafuta fedha za kulitengeneza ikiwa ni utekelezaji wa ahadi ya Mheshimiwa Rais.

**MHE. LUHAGA J. MPINA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa majibu mazuri. Ninayo maswali mawili ya nyongeza.

(i) Kwa kuwa sasa katika Bajeti ya mwaka huu ni upembuzi yakinifu wa hilo daraja la mto Mongo – Bakima pamoja na mtu Waku?

Je, Waziri atakubaliana na mimi sasa katika Bajeti inayofuata fedha zitakuwa zimepatikana za kujenga madaraja haya?

(ii)Kwa kuwa 30% ya fedha zinazotolewa katika Mfuko wa Barabara kwa ajili ya Halmashauri zinatumika kwa ajili ya matengenezo tu na siyo kuchonga barabara mpya, nazo zinakuwa hazitoshi kulingana na ukubwa wa barabara, na kwa kuwa 70% ya wananchi wanaoishi vijijini mpaka sasa hivi hawana barabara za uhakika toka Mungu alipoumba dunia.

Je, sasa Serikali ina mpango gani mahususi kufikia mwaka 2015 wananchi hawa wawe wamepata barabara za uhakika?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI):** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Luhaga J. Mpina, Mbunge wa Kisesa kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, tunachozungumza hapa madaraja ni mawili, na hili daraja la kwanza hapa tumebakisha shilingi milioni 76.5 ili likamilike. Mheshimiwa Luhaga Mpina, madaraja haya ninayazungumza ninayafahamu kwa sababu nimekwenda katika

jimbo lake, anafahamu kabisa kwamba fedha hizi tunazozungumza hapa ni fedha ambazo tumetenga maalum.

Mheshimiwa Spika, kwa bahati mbaya daraja huwezi kulijenga hivyo kwa awamu, daraja linawekwa kama halipo basi unajua kwamba halipo. Nataka nimthibitishie Mheshimiwa Luhaga Mpina, Mbunge wetu wa hapa na Mbunge wa Bunge la Afrika, kwamba hizi shilingi milioni 76.5 ninazozungumzia hizi zitapatikana, fedha hizi nyingine anazozungumza kwa ajili ya hili daraja la pili ni fedha ambazo zitapatikana katika mwaka wa fedha unaokuja.

Mheshimiwa Spika, hapa nimeeleza fedha ambazo zimetolewa, kwa hiyo anaposema kwamba tunataka tena tupate hizo ni hizo hizo tulizopanga kwa sababu Bajeti itakuwa imepita hapa na ninamwomba atusaidie kupitisha bajeti hii ili tuweze kumsaidia katika jambo hili.

Mheshimiwa Spika, la pili anazungumzia habari ya *Road Fund*. Hapa kuna fedha za aina mbili, fedha za *Road Fund* ukizichukua hapa hutumii kwa ajili ya ukarabati wala kujenga barabara, fedha za *road fund* unafanya kitu kinaitwa *periodic maintenance*, mambo yale ya dharura pale kusaidia kuhakikisha kwamba barabara ile inapitika.

Mheshimiwa Spika, ninakubaliana naye kwamba fedha hizi zinazotengwa ni kidogo, na fedha hizi zinapitishwa hapa ni kweli ni kidogo, ukigawa kwa nchi nzima ni kidogo lakini sasa tufanyaje uwezo wetu ndiyo huo na majukumu yetu ndiyo hayo? Mimi naomba tushirikiane na yeye, atusaidie kuonesha vipaumbele katika wilaya yake ili sisi tuelekeze hizi fedha ziende katika hilo eneo.

**SPIKA:** Nashukuru, afadhali hakuna daraja lingine linalofanana na hayo. (*Kicheko*)

Na. 131

**Fedha za Ujenzi wa Makao Makuu ya Wilaya ya Ikungi**

**MHE. CHRISTINA L. MUGHWAI** aliuliza:-

Serikali ilitangaza Wilaya mpya ya Ikungi na kuamua kuwa Makao Makuu ya Wilaya hiyo mpya na Halmashauri yake itajengewa katika eneo lililopo Mashariki mwa Mji Mdogo wa Ikungi:-

Je, Serikali itatenga lini fedha za kuanza ujenzi wa majengo na miundombinu mingine katika Makao Makuu hayo ya Wilaya na Halmashauri ya Ikungi?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Christina L. Mughwai, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo.

Mheshimiwa Spika, nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kuwa Serikali ilitangaza kusudio la kuanzisha maeneo mapya ya utawala katika Mkutano wa Tisa wa Bunge la Bajeti. Wilaya ya Ikungi ambayo inatokana na kugawanywa kwa Wilaya ya Singida ni miongoni mwa maeneo hayo.

Mheshimiwa Spika, kama nilivyoeleza wakati najibu swali na. 66 la Mheshimiwa Vick Kamata, Mbunge wa Viti Maalum, kwamba uanzishaji wa maeneo mapya ya utawala unatawaliwa na Sura 397 ya Sheria inayoelezea uanzishaji wa mikoa na wilaya. Kwa kuzingatia sheria hiyo mchakato wa kuanzisha maeneo hayo unazingatia hatua mbalimbali hadi kukamilika kwake kama ifuatavyo.

(i)Mheshimiwa Rais mwenyewe kuonesha nia yake njema ya kutaka kuanzisha maeneo mapya ya utawala. Dhamira hiyo hutangazwa katika Gazeti la Serikali;

(ii)Uhakiki wa mipaka ya maeneo mapya yanayopendekezwa kuanzishwa yakiwemo Kata, Vijiji na Vitongoji kwa mujibu wa Sheria na taratibu zilizopo. Hatua hii imekamilika;

(iii)Kuwashirikisha wananchi wa maeneo hayo kutoa maoni yao ya mwisho ambapo hupewa siku sitini (60) kutoa maoni yao; na

(iv)Kutoa tangazo la mwisho la kuanzisha Mikoa na Wilaya hizo katika gazeti la Serikali.

Mheshimiwa Spika, suala la kutenga fedha kwa ajili ya kujenga miundombinu ya wilaya mpya ya Ikungi litafanyika baada ya kukamilika kwa taratibu za kuanzisha maeneo hayo kisheria kwa kuwa siyo rahisi kutenga fedha kwa ajili ya jambo ambalo halijaanzishwa. Naomba Waheshimiwa Wabunge tuvute subira wakati taratibu hizo zinakamilishwa.

**MHE. CHRISTINA L. MUGHWAI:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Pamoja na maelezo ya Mheshimiwa Waziri, nina maswali mawili ya nyongeza.

(i)Ili kutimiza nia ya Mheshimiwa Rais na hamu ya wananchi wa Wilaya ya Ikungi ya kuwa na Wilaya na Halmashauri yao, Waziri anaweza kutuambia kwamba hivi sasa Serikali imefikia katika hatua gani ya mchakato wa kutimiza lengo hilo?

(ii) Je, Serikali haioni kuwa kuna haja ya kuharakisha mchakato huo ukizingatia kuwa hivi sasa Makao Makuu ya Wilaya na Halmashauri ya Singida yapo mjini na inakuwa vigumu kwa wananchi kufuatilia masuala yao?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI):** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa

Waziri Mkuu, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Christina L. Mughwai, Mbunge wa Viti Maalum kama ifuatavyo.

Mheshimiwa Spika, hizi wilaya huyu baba alipotoa hotuba hapa amezitaja na zile mbili ambazo zimeondolewa zikaondolewa, hii anayosema Mheshimiwa Christina L. Mughwai, imo humu ndani.

**SPIKA:** Baba gani, baba gani aliyezitaja? (*Kicheko*)

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI):** Eeh!

**SPIKA:** Baba gani aliyezitaja huyo? Umesema huyu baba, baba nani sasa? (*Kicheko*)

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI):** Mheshimiwa Spika, nimesahau nilikuwa nafikiria ameuliza huyu mama. (*Kicheko*)

Kwa hiyo, ninachotaka kusema hapa ni ...

**SPIKA:** Wasikuchanganye, ulitaka…

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI):** Mheshimiwa Spika, naomba niondoe hiyo Mheshimiwa.

**SPIKA:** Mheshimiwa nani?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI):** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya … (*Kicheko*)

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Christina L. Mughwai, kama ifuatavyo.

Mheshimiwa Waziri Mkuu, alikwisha kusimama hapa, wilaya hii anayozungumza Mheshimiwa Christina L. Mughwai, imetajwa humu ndani wala haina ubishi, wala hakuna ugomvi kwamba hii wilaya iko au haiko. Wilaya zilizoondolewa hapa ni ile Wilaya ya Kahama na ile nyingine ya Ulyankulu. Kwa hiyo, hakuna tatizo lolote.

Mheshimiwa Spika, kuhusu kwamba nini kinafanyika, pia alijibu hapa akasema utaratibu umekwishakuwekwa katika Wizara ya Fedha na kama ikibidi kuja mpaka hapa na kuomba kibali hicho, itafanyika hivyo. Ndivyo nilivyomsikia Mheshimiwa Waziri Mkuu akieleza pale, kwa hiyo mimi sipo hapa kutengua Torati, niko hapa kuimarisha Torati, hilo la kwanza. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Spika, la pili ni hili la Makao Makuu. Suala la Makao Makuu mimi hapa sitaki nijibu kitu chochote kwa sababu Makao Makuu hapa ni sehemu ya *politics* hizo na nilijua kwamba Mheshimiwa Mbunge alikuwa analenga hapa. Makao Makuu ni jambo ambalo wao wenyewe kwenye Halmashauri wanazungumza wanakubaliana wanasema kwamba ni hivi. Kwa hiyo, mimi hapa ninachojua ni kwamba maoni ya wananchi yameendelea kuja na wao wamekuwa wanazungumza kuhusu wapi wanapofikiri kwamba panafaa. Sisi tutakapopokea tutahakikisha kwamba tunazingatia mapendekezo yaliyoletwa na wananachi. *(Makofi)*

**MHE. TUNDU A. LISSU:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Naomba kuuliza swali dogo la nyongeza kwa Mheshimiwa Waziri.

Mheshimiwa Spika, tayari vikao viliishafanyika katika ngazi ya *DCC* na *RCC* na tayari Ofisi ya Waziri Mkuu, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) iliishatuma wataalam kwenda kuangalia mahali ambapo Makao Makuu ya Wilaya mpya ya Ikungi yatajengwa; na tayari ripoti zote ziliishatolewa kwa wananchi na kila mtu anafahamu kwamba angalau kwa nyaraka za Serikali Makao Makuu yatakuwa Ikungi?

Sasa Mheshimiwa Waziri anaposema kwamba Makao Makuu yatakuwa wapi ni uamuzi wa wananchi, anataka tuamini kwamba hicho ambacho kimefanyika kilikuwa ni upotezaji tu wa fedha za wananchi au ni kazi ya wataalam wa Serikali ambayo inapaswa izingatiwe?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI):** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Tundu A. Lissu, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, mimi naomba niseme kwa kifupi tu, wala hakuna ubabaishaji wowote hapa, kazi hii ya kuhakiki na kuangalia kwamba mapendekezo ya wananchi yanasema nini ndiyo inaendelea.

Kwa hiyo, mimi ninataka nimwombe tu Mheshimiwa Tundu A. Lissu, hakuna mtu anayepuuza, gharama zimeingiwa mimi sibishi. Ninachosema hapa ni kwamba utaratibu wetu unatutaka sasa tuangalie hayo yote ambayo yamependekezwa na wananchi na kwa msingi sasa ndipo tunapo-*declare* hapa kwamba Makao Makuu hakuna wasiwasi wowote wala alama ya ulizo, uwe na amani moyoni mwako, uwe na hakika kwamba mapendekezo ya wananchi yatazingatiwa. (*Makofi*)

Na. 132

**Ajira katika Sekta za Muungano**

**MHE. MARIAM SALUM MSABAHA** aliuliza:-

Je, ni Wazanzibari wangapi wameajiriwa katika sekta za Muungano?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MUUNGANO)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa ruhusa yako naomba kujibu swali Na. 132 lililoulizwa na Mheshimiwa Mariam Salum Msabaha, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, nataka nikiri kwamba mpaka sasa hakuna takwimu maalum zinazowekwa kuonesha idadi ya wafanyakazi wanaotoka Zanzibar wanaofanyakazi katika Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Takwimu zilizopo ni zile zinazowekwa na Taasisi za Muungano zinazowahusu wafanyakazi wao bila kujali walikotoka ili mradi tu ni Watanzania.

Hata hivyo, Ofisi ya Makamu wa Rais inafuatilia kwa karibu hoja ya ajira kwa watumishi wa Zanzibar katika taasisi za Muungano. Ni hivi karibuni tu Wizara za Utumishi wa Umma, za Serikali ya Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, zilikutana kuzungumzia suala hili.

Katika kikao cha tarehe 2 Mei, 2011, sekta hizo za utumishi wa umma zilikubaliana kufanyia kazi suala hilo la takwimu za watumishi wa Zanzibar wanaofanya kazi SMT. Hata hivyo, kazi ya ukusanyaji na uchambuzi wa takwimu hizo itabidi lifanywe kwa uangalifu mkubwa ili kutotoa taswira yoyote mbaya.

**MHE. MARIAM SALUM MSABAHA:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Nashukuru kwa majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri. Kwa kuwa Wazanzibari wengi wa mikoa ya Pemba na Unguja wamekuwa wakilalakimia sekta ya Muungano kuwa nafasi zinazotolewa na Muungano hazitolewi kwa uwiano.

Je, Waziri atanihakikishiaje kwamba Wazanizbari hawa wanapata haki zao?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MUUNGANO):** Mheshimiwa Spika, kwa ruhusa yako naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Mariam Salum Msabaha, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, katika kikao hicho hicho nilichokitaja Mawaziri wa Utumishi katika Sekta za Umma walikubaliana pia kwamba, Serikali ya Mapinduzi Zanzibar ihimize watu wake au Wazanzibari kuomba nafasi zinazotangazwa katika Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Lakini mbali na hili walikubaliana pia kwamba katika kufanya mahojiano ya ajira, Sekretarieti ya Mahojiano ya Ajira ijumuishe pia Sekretarieti ya Mahojiano ya Ajira ya Zanzibar ili mahojiano yaende katika mtindo unaotakiwa kwa sababu kumekuwa kuna malalamiko kwamba Wazanzibari wamekuwa wakiomba lakini katika mahojiano wanaangushwa. Kwa hiyo wakifanya kwa pamoja hayo malalamiko yatakuwa yameondoka. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. MUSA HAJI KOMBO**: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii, naomba kumwuliza Mheshimiwa Waziri swali moja.Kutokana na *population* ya nchi mbili hizi. Je, haoni kuna maana ya kuwa na hesabu maalum ya kuonesha Wazanzibari watapata haki kiasi gani na Watanganyika watapata haki kiasi gani? Ukiwachanganya hawa, sisi ambao tuko millioni moja katika milioni 40 tutaonekana tuna kitu gani Mheshimiwa Waziri?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MUUNGANO):** Mheshimiwa Spika, kwa ruhusa yako naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Mussa Haji Kombo, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kwamba zoezi hili limekuwa likifanyika katika baadhi ya Sekta, hasa sekta za ulinzi. Jeshi la Polisi na Jeshi la Wananchi wamekuwa wakifanya hivyo. Hata hivyo, katika nafasi nyingine mazungumzo yaliyokuwa yakifanywa ni kwamba wakati wa kufanya mahojiano Wazanzibari wote walio- *apply* wawe kundi moja la mahojiano na washindanishwe wao wenyewe na kundi la pili washindanishwe wao wenyewe. Halafu watakaotoka huku na huku watachukuliwa kwa jinsi matokeo ya *interview* yalivyotokea. Ahsante sana.

Na. 133

**Uchimbaji wa Bwawa la Maji Kwa Ajili ya Mifugo - Serengeti**

**MHE. DKT. KEBWE S. KEBWE** aliuliza:-

Serikali ina mpango gani wa kuanza kuchimba lambo kubwa la maji kwa ajili ya mifugo na binadamu lililopimwa miaka mitatu iliyopita?

**WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO NA UVUVI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Dkt. Kebwe Stephen Kebwe, Mbunge wa Serengeti, kama ifuatavyo:-

Mheshimwa Spika, Serikali kupitia iliyokuwa Wizara ya Maji na Umwagiliaji ilianzisha zoezi la kubaini maeneo yanayofaa kwa kilimo cha umwagiliaji mwaka 2008 katika Wilaya ya Serengeti katika vijiji vya Bugerera, Nyamitita na Majimoto kwa lengo la kujenga mabwawa kwa ajili ya umwagiliaji na matumizi mengine ya binadamu na mifugo. Zoezi hilo lilibaini vijiji vya Bugereza na Nyamitita kuwa na maeneo yanayofaa kwa ujenzi wa mabwawa.

Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia Halmashauri ya Wilaya ya Serengeti imepanga kutekeleza moja ya miradi hiyo katika mwaka 2011/2012 kwa kuanza kuchimba bwawa la maji kupitia Mfuko wa Kuendeleza Kilimo cha Umwagiliaji Wilayani (*District Irrigation Development Fund*) ambapo jumla ya shilingi milioni 200

zimetengwa kwa ajili ya mradi wa umwagiliaji katika Kijiji cha Nyamitita.  Inatarajiwa kwamba mradi huu pia utatoa huduma ya maji kwa ajili ya mifugo na binadamu.

**MHE. KEBWE S. KEBWE:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri ninayo maswali mawili ya nyongeza.

(a) Kwa vile wananchi wa Kata hii ya Majimoto walishapata hamasa baada ya utafiti ule wao wanajua kwamba Serikali ina mpango wa kuchimba bwawa.  Lakini kwa sababu Kata hii inao ng'ombe kama 500 wananchi hawa bado wanaelewa Serikali ina mpango huo.  Je, maeneo kama ya Gabande ni sehemu nzuri, Serikali haioni kwamba kuna umuhimu kuchimba bwawa.

(b) Ni hesabu ambazo zinaeleweka katika Mkoa wa Mara, Wilaya ya Serengeti ni Wilaya ya pili kuwa na ng'ombe wengi wapatao 324,579.  Je, Serikali ina mpango gani kwa hali ya ukame ambao unaendelea nchini kupanua uchimbaji wa mabwawa kwa ajili ya binadamu, mifugo na kilimo?

**WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Spika, swali la kwanza linahusu kwamba wanakijiji wa Kijiji cha Majimoto walikuwa wameshapata hamasa kwamba watajengewa bwawa?

Lakini napenda kumjulisha Mheshimiwa Mbunge kwamba kijiji hiki cha Majimoto kilishafanyiwa uchunguzi na kikaonekana kwamba kwanza eneo lake ni dogo, eneo ambalo linajengwa kwa ajili ya kuvunia maji ni dogo, kwa hiyo halifai.  Lakini pia eneo la ujenzi wa tuta halitatosha kukusanya maji mengi, lakini sababu ya tatu ni kwamba hakutakuwa na torosho, torosho ni kwa kiingereza wanaita *spillway*.  Kwa hiyo hivi vitu vitatu eneo la *spillway*, eneo la kujenga tuta pamoja na eneo la kuvunia maji linatakiwa liwe kubwa kusudi bwawa hilo liweze kusaidia wanyama wengi zaidi pamoja na umwagiliaji.

Mheshimiwa Spika, lakini swali lake ka pili, Wilaya hii pamoja na kwamba ina mifugo mingi na ni mfano mzuri wa Wilaya zenye mifugo mingi, lakini pia Wilaya hii ina malambo mengi kuliko Wilaya nyingine yoyote ya maeneo yanayozunguka katika jimbo lake.  Kwa mfano kuna malambo 15 na sasa hivi Halmashauri ya Wilaya wana mpango wa kuweka mabirika katika majosho 12.  Lakini pia Halmashauri ina mpango kwa sasa hivi mpango wa kupanua bwawa la Nyamitita liweze kutumia kiasi cha shilingi bilioni moja kwa kutumia fedha za *BIDF* pamoja na *DADP's* ili liweze kutumika kwa mifugo pamoja na binadamu.

**MHE. MICHAEL L. LAIZER:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kunipa nafasi niulize swali dogo la nyongeza.

Kwa kuwa fedha za malambo hazipo katika Wizara ya Mifugo na ni vigumu sana Wizara ya Mifugo kusimamia au kujua malambo yaliyochimbwa.  Je, Serikali haioni kwamba ni makosa kuondoa fedha za malambo katika Wizara hii na itakuwa ni kumwonea Waziri kumwuliza malambo ambayo hayako katika  Bajeti yake.

**WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Spika, fedha hizi zinapokuwa zinatoka Serikali, Serikali ni moja hakuna kusema hizi zinakwenda Halmashauri hatuwezi kusimamia. Sisi ndio tunahakikisha kwamba ubora wa Malambo yale na mabwawa yale unakuwa ni mzuri. Sisi ndio *regulators* wa kuhakikisha kwamba vitu hivi vinakuwa katika viwango. Kwa hiyo, fedha zile zinatumwa kule kwenye Halmashauri kwa sababu Halmashauri ndiyo inakuwa *responsibles* kutekeleza *"D by D"*.

Kwa hiyo, hatuwezi kusema kwamba sisi hatuwezi tukaona kinachoendelea Wilayani. Sisi tunatoa fedha kama Serikali kupitia kwenye Programu za *ASDP* pamoja na programu zingine lakini tunatuma wataalam kuhakikisha kwamba mabwawa yanayojengwa yanakidhi viwango ambavyo vimewekwa. Lakini niseme kwamba Serikali ni moja na vyote tunafuatilia kwa pamoja.

**SPIKA:** Ahsante sasa tunaendelea na swali linalofuata. Mheshimiwa Dkt. Titus Kamani, pole alinusurika kwenye ajali juzi.

**MHE. DKT. TITUS M. KAMANI:** Ahsante sana na nashukuru sana kwa sala zako na wengine wote walionipatia pole niko salama na tunaendelea. *(Makofi)*

Na. 134

**Kufufua Kituo cha Wafugaji cha Igalukilo - Busega**

**MHE. DKT. TITUS M. KAMANI** aliuliza:-

Kituo cha kufundishia wafugaji na kupandisha mitambo cha Igalukilo Jimboni Busega kilifanya kazi nzuri sana iliyochochea mabadiliko ya tabia za wafugaji kutokuhama; au kuja maeneo ya malisho na kuboresha mbegu za mifugo. Kwa sasa kituo hicho kimeachwa bila usimamizi na wananchi wanakaribia kufanya makazi yao hapo:-

Je, ni lini Serikali itakifufua kituo hicho ili kifanye kazi yake ya awali na hatimaye kuongeza mapato ya wafugaji wa Busega na Mkoa wa Simiyu kwa ujumla?

**WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO NA UVUVI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mhe. Dkt. Titus Mlengeya Kamani, Mbunge wa Busega, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Kituo cha kufundishia wafugaji na kupandisha mitamba cha Igalukilo kilichoko katika Tarafa ya Kivukoni Kata ya Igalukilo katika Halmashauri ya Wilaya ya Magu kilianzishwa mwaka 1958 kwa lengo la kutoa huduma za ugani ambazo ni pamoja na tiba na ushauri kwa wafugaji, kufuga madume bora kwa ajili ya kuboresha kosaafu za mifugo ya asili na kuzalisha malisho bora.

Wizara yangu ilikabidhi kituo hiki kwa Halmashauri ya Wilaya ya Magu tangu mwaka 1974 na Halmashauri hiyo imeendelea kukitumia kutoa huduma za tiba ya mifugo na ushauri kwa wafugaji.

Mheshimiwa Spika, nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kuwa kituo hiki kilifanya kazi nzuri iliyochochea mabadiliko ya wafugaji kuacha tabia ya kuhamahama na kufuga kisasa. Kwa kutambua umuhimu wa kituo hiki na kuleta mapinduzi ya ufugaji, Halmashauri ya Wilaya ya Magu imepanga kukifufua kituo hiki kwa awamu kuanzia mwaka 20011/2012 kwa kupima upya eneo la kituo hiki na kukarabati miundombinu iliyochakaa. Baada ya ukarabati huo, kituo hiki kitapewa madume bora sambamba na huduma za uhimilishaji ili kuboresha mifugo ya asili. Aidha, kituo kitatoa mafunzo ya ufugaji bora kwa wananchi wa Busega na vijiji jirani.

**MHE. DKT. TITUS M. KAMANI:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipatia nafasi niulize swali dogo la nyongeza.

Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri, sekta ya mifugo ni moja ya sekta ambayo ni muhimu sana sasa hivi kwa uchumi wa wananchi wetu. Kituo hiki ni muhimu sana katika kubadilisha hali ya ufugaji na uchumi wa mifugo katika eneo lile na ukanda mzima wa Ziwa. Sasa kwa utaratibu wa fedha ya Halmashauri kwa kweli nafikiri itachukua muda mrefu sana kituo hiki kufufuliwa.

Sasa sijui Mheshimiwa Waziri anaweza kuwa tayari kutembelea kituo hiki na kujionea ukubwa wa kazi wa kukifufua kituo hiki ili aweze kuangalia namna gani kinaweza kufufuliwa haraka. Ahsante sana.

**WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO NA UVUVI:**Mheshimiwa Spika, kwanza natambua umuhimu wa kituo hiki na pia niweze kumpongeza Mheshimiwa Kamani kwa sababu yeye ni Daktari wa Mifugo na nadhani atatoa huduma nzuri sana kuwashauri wananchi wake kwenye jimbo lake katika ufugaji bora.

Nakubaliana na yeye kwamba nitatembelea eneo hili ili niweze kuona ukubwa wa kazi, lakini pia namshauri kwamba sasa hivi nguvu zetu tuzielekeze katika kupima eneo hili upya na tukarabati miundombinu pamoja na kuhakikisha kwamba huduma za uhimilishaji zinaanza. Mimi niko tayari kusaidiana naye katika kuhakikisha kwamba huduma hizi za uhimilishaji pamoja na kupeleka madume bora katika kituo hicho inafanyika mara moja punde tu ukarabati wa awali utakavyoanza kufanyika.

Na. 135

**Mirathi na Athari Zake Kwa Watoto Yatima**

**MHE. NAOMI A. M. KAIHULA** aliuliza:-

Hali ya kutopatikana mirathi kwa wakati kumewaathiri kwa kiasi kikubwa watoto ambao wazazi wao wamefariki na kuwafanya watoto hao kuishi maisha ya taabu na wengi wao wamekuwa watoto wasio na makazi wanaoonekana kwenye miji yetu na kuwa fedheha kwa Taifa, na kwamba hakuna sheria maalum kuhusiana na masuala ya urithi:-

(a) Je, ni hatua gani zinachukuliwa dhidi ya taratibu zinazowakandamiza wahitaji wa huduma ya mirathi?

(b) Katika kipindi cha muongo mmoja ni mirathi mingapi imefanikiwa na mingapi haikufanikiwa, sababu zake ni nini?

(c) Je, Serikali inachukua hatua gani dhidi ya sheria kandamizi za mirathi?

**WAZIRI WA AFRIKA MASHARIKI (K.n.y. WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Katiba na Sheria, kwa ridhaa yako nayajibu maswali ya Mheshimiwa Naomi Kaihula, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, masuala ya mirathi katika nchi yetu hutawaliwa na mojawapo ya sheria tatu ambazo ni:-

Sheria za kimila (*Customary Laws*) ambazo hutumika ikiwa Marehemu alikuwa akiishi kwa kufuata ustaarabu wa Mila na Desturi za kabila lake bila kufuata ustaarabu wa kigeni au usio wa kabila lake.

Sheria ya Kiislam ambayo hutumika ikiwa Marehemu alikuwa mfuasi au muumini wa dini ya Kiislamu.

Sheria ya Mirathi ya India ya mwaka 1865 iliyopokelewa na Mahakama za Tanganyika na ambayo hutumika ikiwa marehemu hakuwa muumini wa dini ya Kiislamu au hakuwa akifuata Mila na Desturi za kabila lake.

(a) Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, Serikali haina mamlaka yoyote ya kubatilisha sheria za kidini, hata ikiwa zinaonekana kuwa na mwelekeo wa ukandamizaji. Hata hivyo, kwa sheria za Kimila na Desturi Mahakama zina uwezo wa kuzitangaza sheria hizo kuwa ni batili endapo zitakuwa zinakiuka misingi ya haki iliyomo katika Katiba au Sheria za Nchi.

(b) Mheshimiwa Spika, bado hadi sasa Serikali haijakamilisha takwimu anazozihitaji Mheshimiwa Kaihula za kuainisha idadi ya kesi za mirathi katika miaka 10 iliyopita. Mashauri ya mirathi yapo katika ngazi zote za Mahakama kuanzia Mahakama za Mwanzo hadi Mahakama za Rufaa. Siyo rahisi kupata takwimu za kesi za mirathi pekee kwa miaka kumi yaani muongo mmoja.

(c) Mheshimiwa Spika, suala la sheria kandamizi za mirathi mpaka sasa Serikali inafanyia kazi kwa umakini mapendekezo yaliyotolewa na Tume ya Kurekebisha Sheria, tukizingatia ya kuwa suala lenyewe ni nyeti na linagusa Mila na Desturi za wananchi walio wengi.

**MHE. NAOMI A. M. KAIHULA:**Mheshimiwa Spika**,** ahsante. Namshukuru Waziri kwa majibu yake. Lakini nasikitika kuwa hajajibu swali langu. Hata hivyo nina maswali ya nyongeza.

Swali la kwanza ninapenda kufahamu ni kwamba kuna sheria zinazokuwa Kikatiba kwa sababu Katiba yetu inalinda haki za binadamu. Sheria zetu hazina dini. Sasa nikiambiwa kwamba kwa ajili ya Mila, Desturi na ndio maana inashindikana na ndiyo inamaanisha kwamba Katiba haina maana sheria mama? Hilo la kwanza.

Suala la pili, napenda kuuliza kwa vile nilivyokuwa napenda kuuliza. Nilikuwa nataka kusema hivi kwanza ni *declare interest* mimi mwenyewe ni muathirika wa hilo suala. Ni kwamba wanawake walio wengi ambao wanaathirika na kufuatilia mirathi kwa mfano wafanyakazi huwa hawapewi haki zao.

Kwa mfano mimi hapa mwenyewe, miaka 10 toka mwaka 2002 toka mume wangu afariki na mimi ni mwanamke ambaye ninafahamu na najua taratibu na *documents* zote za mume wangu nilikuwa nazo lakini nilishindwa kupata hizo hii inamaanisha kwamba wale walio wengi mpaka sasa huwa hawapati na ndicho nilichokuwa nauliza.

Sasa wale watoto wao wanakuwa wanasumbuka ada na wengine wanaishia mitaani. Je, ni kwa nini na kama ni hivyo kwa nini Serikali haifanyi taratibu ambapo amekiri mwenyewe yaani inasikitisha sipendi hata Mataifa ya nje yasikie yaani hatuna *document* za miaka 10 tunapangaje sasa.

Kwa hiyo ninachouliza ni hicho inafanya nini kupunguza taratibu kandamizi za kutowapatia kwa wakati waathirika ambao wengi wao ni wanawake, haki zao za fedha au mirathi. Ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante Mheshimiwa Mbunge Mataifa yameshasikia.

**WAZIRI WA AFRIKA MASHARIKI:** Mheshimiwa Spika, lile la kwanza kuhusu dhana anayoiona yeye kwamba labda Katiba ipo chini ya Mila au masuala ya Dini, sivyo hivyo. Ndani ya Katiba misingi hiyo ya kuheshimu imewekwa hiyo misingi.

Kwa hiyo na ndani ya misingi hiyo ni kuheshimu kila imani iliyopo kwa sababu ndio Katiba ilitoa uhuru wa Watanzania kila mmoja kuweza kuwa na imani yake na dini yake bila ya kuingiliwa hata kidogo. Kwa hiyo kuitaka Serikali ibadili msingi huo itakuwa ni kuvunja Katiba na hatupendi kufanya hivyo kwa sababu Katiba ndio sheria mama. Sasa kama yeye haridhiki katika zile sheria zinazohusu imani yake hilo suala asiilaumu Serikali kwa sababu hilo ni suala la imani.

Suala la pili, nampa pole sana kwa haya yote yaliyomkuta, lakini haya mambo ni marefu sana ya mirathi inategemea shemeji zake walikuwaje, wifi zake na kama ukoo wa mume wake ni mpana basi ni mgogoro mkubwa sana ambao unahusu mali za marehemu, wadogo zake. Ndio maana tunasisitiza kwamba ni vizuri kila Mtanzania aweze kuandika wosia kwa sababu wosia unaweza kupunguza kabisa utata. Kwa kuwa hakunifahamisha zaidi kuhusu mambo yake yalivyokuwa pengine tungeweza kuonana baadaye ili nimpe ushauri wa kisheria kuhusu hilo. (*Makofi/Kicheko)*

**SPIKA:** Ahsante nakuletea mjane mwingine.

**MHE. FATMA A. MIKIDADI:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi hii ili nami niweze kuongeza swali la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, imeshaonekana kwamba sheria hizi ziko aina, aina, sheria za kiislamu, sheria za kimila, sheria za Serikali. Kwa kuzingatia kwamba siku hizi Waislam na Wakristo wanaoana ni jambo la kawaida. Serikali haioni sasa ni wakati muafaka wa kuchambua sheria zikaongezwa kwamba sheria za ndoa mchanganyiko Wakristo na Waislamu. Ahsante Mwenyekiti.

**WAZIRI WA AFRIKA MASHARIKI:**Mheshimiwa Spika, sheria ya ndoa ya mwaka 1971 inatambua hizo ndoa mchanganyiko. Kwa hiyo hakuna haja ya kuwa na sheria yoyote mpya. Lakini tahadhari tu kwa wanaoingia katika ndoa hizi mara nyingi hilo nalo linaleta matatizo kama watu ni imani tofauti. Kwa sababu kutakuwa na mvutano kuhusu sasa sheria ipi itumike.

Lakini kama mwanamke wa Kitanzania ambaye si muislamu amekubali kuolewa na muislam basi ajue kwamba yale masharti ya mirathi katika dini ya kiislamu ndiyo yatamkuta yeye sasa. Kwa hiyo, hilo nalo ni la kuangalia.

Na. 136

**Athari za Kuchelewa Kumaliza Kesi za Mirathi**

**MHE. MARTHA M. MLATA** aliuliza:-

Mahakama nyingi hapa nchini zinaonekana kushindwa kumaliza kesi za mirathi kwa wakati na kusababisha watoto wengi yatima kushindwa kumudu maisha na kukimbilia mitaani kwa kukosa fedha za shule na kujikimu maisha.

Je, Serikali inatoa tamko gani juu ya haali hiyo?

**WAZIRI WA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI (K.n.y. WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa ridhaa yako na pia kwa niaba ya Waziri wa Katiba na Sheria naomba kujibu swali la Mheshimiwa Martha Moses Mlata, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kesi za mirathi huchukua muda mrefu kupatiwa maamuzi na Mahakama kwa sababu ni kesi ngumu na zenye ushindani mkali na mara nyingi ninahusisha masuala ya imani ama za dini ama za kimila. Aidha marehemu wengi huwa hawaichi wosia na hivyo kusababisha mashauri ya mirathi yaamuliwe kwa kutumia Sheria ya Mirathi ya India ya mwaka 1865 au ya Kiislam au Sheria za kimila.

Mheshimiwa Spika, ikumbukwe pia kwamba mashauri ya mirathi hutawaliwa na hisia kali miongoni mwa wanafamilia wahusika kuhusu masuala kama vile nani mwenye haki ya kusimamia mirathi, wajibu wa msimamizi wa mirathi na kuainisha warithi halali. Tatizo linakuwa kubwa zaidi pale mali za marehemu zinapokuwa nyingi. Aidha, upana na ukoo *(extended family)* ya marehemu unapokuwa mkubwa wadai wa mirathi huongezeka na kuwa ni wengi pia.

Mheshimiwa Spika, katika hili hii Serikali inawashauri wananchi wote kujenga tabia ya kuandika wosia kwa sababu wosia ndiyo hueshimika katika Mahakama kuwa ndiyo Kauli rasmi ya mgao ya mirathi.

**MHE. MARTHA M. MLATA**: Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa majibu ya Mheshimiwa Waziri, lakini masikitiko yangu ni kuona kwamba swali lililopita na swali hili yote yanakilio kimoja na Serikali bado haijatoa majibu ya kuridhisha kwa sababu kwenye swali langu nimeulizia kwamba Serikali itoe tamko na haijatoa tamko naijatoa tamko. *(Makofi)*

Sasa ninamwuliza Mheshimiwa Waziri, kwa mateso wanaoyoyapata wanawake wa Tanzania wanapoondokewa na wenzi wao na watoto wanopata mateso makali wanapoondokewa na mzazi wao hasa wa kiume.

Serikali imekuwa ikitoa tamko hapa Bungeni mara kwa mara kwamba italeta Sheria mpya. Miaka mitano niliyokaa iliyopita Sheria ile haikuletwa na sasa hivi wanatoa tamko la juu juu. Ninaomba nipatiwe tamko kwa ajili ya wanawake wote wa Tanzania na watoto yatima, Serikali inasema nini? (*Makofi*)

Swali la pili, wajane wengi kwa sababu wamesema wasimamizi wa mirathi kunakuwa na mzozo namna ya kusimamia ile mirathi na wajane wengi wanapofika Mahakamani wanakuwa hawajui Sheria na hawajui taratibu za Mahakamani na wanashindwa kuweka Wakili kwa sababu ya gharama.

Je, Serikali sasa iko tayari kuweka wasimamizi wa mirathi wa kisheria kwenye Mahakama zote watakaowasaidia wajane hawa? *(Makofi)*

**WAZIRI WA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI:** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Katiba na Sheria naomba nijibu maswali ya Mheshimiwa Martha Mlata, kama ifuatavyo:-

Kwanza kauli ninayoweza kutoa ni kuendelea kuwapa pole tu wale ambao mambo haya yanawasibu. Kwa sababu kwa vyovyote vile maamuzi kuhusu uhalali wa mirathi ni masuala ya Sheria. Kwa hiyo Serikali kama mtawala haiwezi kutoa tamko la kuzifunga Mahakama na vyombo vya maamuzi kuhusu namna ya kugawa mirathi. Litaendelea kubaki suala lenye utata kwa sababu ya mchanganyiko wa masuala ya imani, masuala ya mirathi na masuala ya Sheria na tabia za wananchi. Hili ni suala ambalo linahusu hata Utamaduni wetu kwa sababu bado nasikitika mfumo huu tulionao ni mfumo dume una matatizo sana. *(Makofi)*

Kwa hiyo, tutegemee tu kadri tunavyoelimisha wananchi kuhusu kuheshimu haki za wanawake na jitihada hiyo ifanyike kwa makini na Serikali tuko mstari wa mbele matatizo haya yataendelea kupungua. Lakini wenye matatizo mahususi tunawashauri wafike Wizarani ili yaweze kuangaliwa kwa sababu kuna njia nyingi inawezekana mambo yalikosea toka mwanzo. Kwa hiyo unaweza kupata ufumbuzi.

Hili la pili ambalo linafanana na hilo la kwanza la kuhusu tamko na namna gani kusaidia wanaoteseka na kadhalika, hakuna namna ambayo Serikali inaweza ikaingilia kati masuala haya, kwa sababu yanahusu ndoa, yanahusu talaka, yanahusu mapenzi na mambo haya ni magumu kidogo, inafikia hali wengine wanawaua watoto sio tu suala la mirathi. Wanaachana na baba na mama, mmoja anakasirika anawaua watoto. Sasa hili ndilo linaonesha suala hili lilivyo na hisia kali sana.

Kwa hiyo, suala kubwa ni kuelimishana, tulifanya utaratibu Serikalini kupitia Tume ya Kurekebisha Sheria wakapita mikoa yote ya Tanzania, tunayo taarifa Wizarani kubwa ambayo tunaiangalia na kuifanyia kazi lakini hata wakati ile Tume tu ya kurekebisha Sheria inapita katika Mikoa tulipewa tahadhari kwamba msiingie hata kidogo katika masuala ya imani. Kwa hiyo, ndiyo maana mnaona mambo haya yanachukua muda lakini tuwe na subira na tutafika pazuri baadaye. *(Makofi)*

**SPIKA:** Maswali ya nyongeza ya nini? Kasema kwamba hili tatizo lipo tu. Tunaenda Wizara ya Viwanda na Biashara.

Na. 137

**Mauzo ya Tanzania na AGOA**

**MHE. RIZIKI OMAR JUMA** aliuliza:-

Kwa kutumia mpango wa makubaliano wa kukuza fursa za kiuchumi kati ya Afrika na Marekani *(AGOA)* mwaka 2009 mauzo ya Tanzania yalifikia Dola 42.2 milioni kutoka Dola 40.3 milioni mwaka 2008.

(a) Je, ni kiasi gani cha mauzo ya Tanzania kimeongezeka nchini Marekani mwaka 2010?

(b) Je, Serikali ina mikakati gani ya kuhakikisha mauzo yanaongezeka zaidi nchini Marekani?

**SPIKA:** Naibu Waziri wa Viwanda na Biashara majibu. Kwanza ahsante Waziri wa zamani wa Sheria na Katiba kutujibia matatizo makubwa ya mirathi.

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kabla ya kujibu swali la msingi la Mheshimiwa Riziki Omari Juma, Mbunge wa Viti Maalum, naomba kutoa maelezo mafupi kama ifuatavyo:-

Kwanza mauzo ya Bara zima la Afrika katika Soko la *AGOA* mwaka 2008 yalikuwa ni asilimia 1.3 ya manunuzi yote ya nchi ya Marekani. Pili asilimia 3.8 ya mauzo hayo yalitokana na nchi moja tu ya Bangladesh. Tatu katika mauzo yote yaliyofanyika kutoka Afrika asilimia 96 ya bilioni 56.3 ambazo ziliuzwa mwaka 2008 yalitokana na bidhaa za mafuta na nchi ya Nigeria, Angola na baadhi ya nchi ambazo zinazouza mafuta kwa wingi zilinufaika zaidi na mpango huu. Majirani zetu nchi ya Kenya walikuwa wameuza bidhaa za shilingi milioni 200 Dola za Kimarekani. Takwimu za mauzo zilizotolewa na Mheshimiwa Riziki Omar Juma, ni zile zinazojumuisha mauzo yote ya Tanzania nchini Marekani ikiwa ni pamoja na mauzo ya Mpango wa *AGOA* na bidhaa ambazo zinazotozwa ushuru.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo naomba sasa kujibu swali la Mheshimiwa Riziki Omari Juma, Mbunge wa Viti Maalum, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a)Mheshimiwa Spika, Tanzania ilianza kutumia fursa ya Mpango wa AGOA Februari 2002, baada ya kutimiza masharti yaliyotajwa. Mauzo ya Tanzania kupitia Mpango huo kuanzia mwaka 2002 hadi 2007 yalifikia jumla ya Dola za Kimarekani milioni 13,400,000/-. Mauzo ya *AGOA* kwa mwaka 2008 na 2009 yalikuwa ni kiasi cha Dola za Marekani 1,527,00 na 1,006,000 sawia. Kwa mwaka 2010 mauzo ya bidhaa za Tanzania kupitia mpango wa *AGOA* yalifikia Dola za Marekani 1,867,000 ikiwa ni ongezeko la asilimia 85 ukilinganisha na mauzo ya mwaka 2009. Bidhaa zilizouzwa kwa utaratibu huu ni pamoja na bidhaa za sanaa, kilimo, nguo, madini na misitu.

(b) Mheshimiwa Spika, ili kuhakikisha mauzo ya Tanzania yanaongezeka katika soko la Marekani kupitia Mpango wa *AGOA,* Serikali kwa kushirikiana na wadau mbalimbali imeandaa na kuanza kutekeleza Mpango Unganishi wa Biashara Tanzania *(TTIS),* Mpango huo unajumuisha bidhaa za kipaumbele ambazo ni pamoja na korosho, kahawa, nguo na mavazi, madini na bidhaa za sanaa.

Aidha Serikali inaendelea Maeneo Maalum ya Uzalishaji kwa Mauzo ya Nje *(EPZ)* pamoja na kuanzisha utaratibu wa kutenga maeneo maalum ya uwekezaji (*Special Economic Zones -SEZ*) kwa ajili ya uzalishaji unaolenga masoko ya ndani na nje.

Aidha Serikali imeendelea kuwajengea uwezo wajasiriamali kwa kuwapa mafunzo pamoja na kuwaunganisha na fiursa zilizopo nchini ili kuwawezesha kufikia soko la *AGOA. (Makofi)*

**MHE. RIZIKI OMAR JUMA**: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kunipa nafasi maswali mawili ya nyongeza lakini pia namshukuru Mheshimiwa Waziri kwa majibu yake mazuri. Swali la kwanza, Tanzania tunayo pamba ya kutosha inayoweza kutumika kwa kutengeneza nyuzi na hata vitambaa na nguo na iwapo Serikali itajitahidi kufungua viwanda vya kutengeneza nguo kwa njia ya PPP, tunaweza kusafirisha nguo hizo na kupeleka katika soko la *AGOA.* Je, Serikali inachukua hatua gani ya kutoa fedha kutoka vyombo vya fedha ili viwanda hivyo vifunguliwe na kupata soko hilo kama vile wafanyavyo wenzetu wa Madagascar?

Mbili, kwa kuwa Soko la *AGOA* linaweza kuwa ni sehemu ya ukombozi kwa nchi zinazojitutumua kutengeneza bidhaa zenye viwango na kupelekwa Marekani na kwa kuwa soko hili la *AGOA* ni la muda maalum. Je, ni kwanini nchi yetu ya Tanzania isiombe wataalam wa kutengeneza *design* mbalimbali za nguo hasa kama vile T-shirt, suruali au mashati kama nchi marafiki kama vile Vietnam, India, Thailand na kadhalika ili waje wawafunze vijana wetu kutengeneza biadhaa hizo? *(Makofi)*

**SPIKA:** Sasa uliza swali sio hotuba.

**MHE. RIZIKI OMAR JUMA**: Na kusafirisha kwenda katika soko la *AGOA* iwapo viwanda vitakuwepo ambayo itakuwa ni njia moja ya kuongeza ajira ya vijana wetu?

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA:** Mheshimiwa Spika, nakubaliana kabisa Mheshimiwa Riziki kwamba Tanzania inazalisha pamba, kufikia mwaka jana tayari tulikuwa na uwezo wa kuwa na marobota zaidi ya laki tatu ambayo asilimia 80 ya pamba yetu kwa sasa hivi zinapelekwa nje bila kuongezwa thamani hapa nchini.

Kwa maneno mengine kama tukiongeza uzalishaji wa viwanda kwa kupitia mpango wa *EPZ* na kwa kupitia *SEZ* tunaweza kabisa tukafanikisha kuongeza uzalishaji wa viwanda na tukaweza kushindana na Kenya ambayo hadi kufikia 2008 mauzo yao kwa ujumla yalikuwa yamefikia dola za kimarekani milioni 200 mauzo ya wafanyabiashara wa Tanzania kwa miaka ile mitano niliyoitaja yalikuwa ni Dola za Kimarekani milioni 13 peke yake. *(Makofi)*

Swali la pili, ni kweli na nidhahiri kwamba mpango wa *AGOA* umezisaidia nchi nyingi za Afrika. Lakini naomba nisisitize kama nilivyosema kwenye jibu langu la msingi zaidi ya asilimia 96 ya mauzo yote yaliyotoka Afrika kwenye soko la *AGOA*

yalikuwa ni mauzo ya bidhaa za mafuta. Nchi ya Nigeria na nchi zile ndogondogo ambazo zinazalisha mafuta chini ya huu mpango walinufaika sana. Bara zima la Afrika kwa ujumla wake tuliuzasha bidhaa za nguo na mavazi kwa asilimia 1.3 katika hili soko la Marekani.

Tunahitaji tuwashawishi wafanyabiashara wa ndani na wafanyabiashara wa nje waweze kuwekeza katika utaratibu wa SEZ na EPZ na Serikali imetoa fursa maalum ya kuwapa nafuu ya kodi wakati wanaanza kuwekeza wanapoleta mitambo yao na hili litaenda sambamba na sisi kuweza kupata wataalam ambao watakuwa na ujuzi wa kutengeneza nguo na bidhaa zingine bora zaidi ambazo zitaingia kiushindani katika soko hili la *AGOA.* *(Makofi)*

**MHE. RAJAB MBAROUK MOHAMED**: Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa nafasi hii. Kwa kuwa Visiwa vya Zanzibar ni wazalishaji wazuri wa viungo.

Je, Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, itakuwa tayari au ina mpango gani wa kuweza kuisadia Zanzibar kuinua uchumi wake kupitia njia hii ya *AGOA* hasa kupeleka bidhaa yake hii ya viongo? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA:** Mheshimiwa Spika, kwanza tunakubaliana kwamba viungo vinavyozalishwa Zanzibar ni muhimu na vinapendwa sana kote duniani na Zanzibar ni jina ambalo linavuta hisia ya wanadamu wengi sana duniani na wanatamani kuja watembelee Zanzibar katika uhai wao.

Serikali inaamini kwamba kama wazalishaji wa hivi viungo kutoka Zanzibar, jambo la kwanza kama wataongeza umaridadi katika kuvifungasha. La pili wataongeza wingi, la tatu wataongeza kuaminika kama mnunuzi anahitaji marobota matatu ya *spices* kila mwezi Wazanzibar watampatia. Ni matumaini yetu tutatafuta hili soko kwa pamoja na Wizara inayohusika Zanzibar na tunaweza kushirikiana kuhakikisha kwamba wanauza katika soko hili la *AGOA* na kwingineko duniani. *(Makofi)*

Na. 138

**Uwekaji wa Mkongo wa Taifa**

**MHE. ABDUL JABIR MAROMBWA** aliuliza:-

Uwekaji wa Mkongo wa Taifa unaendelea na baadhi ya maeneo kama vile Kibiti, Rujifi Mkongo huo umepitishwa chini ya nyumba za wananchi.

(a) Je, ni sababu gani zimefanya Mkongo huo upitishwe katika nyumba za watu?

(b) Je, ni madhara gani yanaweza kuwapata wananchi wanaioshi kwenye nyumba hizo?

**WAZIRI WA MAWASILIANO, SAYANSI NA TEKNOLOJIA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Abdul Jabir Marombwa, Mbunge wa Kibiti, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano unajengwa ndani ya hifadhi za barabara, reli na nguzo za *TANESCO*. Wamiliki wa hifadhi hizo ni pamoja na *TANROADS, TANESCO, RAHCO,* Manispaa/Halmashauri na *TAZARA.* Wizara imekuwa ikiomba vibali kwa taasisi husika ili kupata ruhusa ya kutumia hifadhi hizo katika ujenzi wa Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano.

Sehemu kubwa ya Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano umewekwa kwenye hifadhi ya barabara zinazomilikiwa na *TANROADS.* Kwa mujibu wa mabadiliko ya Sheria ya Hifadhi za Barabara ni mita 30 kutoka katikakati ya barabara. *TANROADS* wametoa kibali cha kujenga Mkongo ndani ya mita moja ya mwisho ya hifadhi ya barabara yaani kati ya mita 29 na 30.

Mheshimiwa Spika, wakati wa ujenzi wa Mkongo, imebainika kuwa baadhi ya wananchi wamejenga nyumba ndani ya hifadhi ya barabara. Hivyo ili kuendena na Sheria ya Hifadhi ya Barabara, Wizara imelazimika kupitisha mkongo chini ya nyumba hizo mita tatu kwenda chini ili kuepuka kuzibomoa. Mitambo maalum *(thrust boring machine)* inatumika kufanya zoezi hilo.

Aidha utaratibu huu hutumika wakati wa kuvusha mkongo kwenye barabara za lami ili kuepuka kuzibomoa na hatimaye kuzijenga upya.

(b) Mheshimiwa Spika, kupitisha mkongo chini ya nyumba hizo hakuna madhara yoyote kwa nyumba zenyewe wala kwa afya za wananchi wanaoishi kwenye nyumba hizo kimsingi mkongo hauna madhara yoyote ya kiafya mahali unapopita. *(Makofi)*

**MHE. ABDUL J. MAROMBWA:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu ya Naibu Waziri, nina swali moja la nyongeza.

Kwa kuwa ujenzi wa Mkongo huu wa Taifa umezingatia Sheria Mpya ya Barabara; na kwa kuwa nyumba nyingi zilizopitishwa Mkongo huu zilijengwa kabla ya kupitishwa Sheria hiyo; na kwa kuwa kuna baadhi ya nyumba pale Kibiti zimebomoka kutokana na kupitishwa kwa Mkongo huo; je, Serikali ipo tayari kulipa fidia pindi ikibainika kuwa nyumba hizo zimebomoka kutokana na kupitishwa kwa Mkongo huo?

**NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Spika, kama nilivyojibu kwenye swali la msingi, kimsingi, MKONGO WA MAWASILIANO tunapokuta nyumba ipo katika hifadhi ya barabara, tunachimba mita tatu kwenda chini, halafu kwa kutumia mashine maalum tunavusha ule mkongo kwenda upande mwingine. Kama itadhihirika kwamba, nyumba hiyo ambapo mkongo umepitia ilikutwa pale, yaani ilikuwa zaidi ya mita 22.5 kama Sheria ya Barabara ilivyokuwa

zamani, basi Serikali kama inavyoahidi siku zote, itaangalia uwezekano wa kuwafidia wahusika wa nyumba hizo.

**SPIKA**: Ahsante. Waheshimiwa Wabunge, maswali yamekwisha na muda pia umekwisha. Orodha ya wageni ambao ninao hapa ni Wakuu wa Mikoa kama kawaida, kwa sababu Ofisi ya Waziri Mkuu, inaendelea na mjadala. Pamoja nao leo wamekuja Mke wa Mkuu wa Mkoa wa Dodoma, Mrs Nsekela. Tunao *DCs* wafuatao: Mheshimiwa Dari Rwegasira, *DC* wa Mpwapwa; Mheshimiwa Tupa wa Dodoma Mjini; Mheshimiwa Betty Mkwassa, *DC* Wilaya ya Bahi; Mheshimiwa Lephy Gembe, *DC* wa Wilaya ya Chamwino; na Mheshimiwa Lembrice Kipuyo wa Wilaya ya Kongwa. Wawa walikuwa Wakuu wa Wilaya za Mkoa wa Dodoma, lakini ninaona hawapo watakuja baadaye.

Waheshimiwa Wabunge, nitangaze shughuli za kazi; Mwenyekiti wa Kamati ya Huduma za Jamii, Mheshimiwa Margaret Sitta, anaomba niwatangazie Wajumbe wa Kamati yake kwamba, leo saa saba mchana, watakuwa na kikao chao katika Ukumbi Namba 227.

Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba, Sheria na Utawala, Mheshimiwa Pindi Chana, anaomba niwatangazie Wajumbe wa Kamati yake kwamba, leo saa saba, watakuwa na kikao katika Chumba Namba 231.

Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama, Mheshimiwa Erdward Lowassa, anaomba niwatangazie Wajumbe wa Kamati yake kwamba, leo saa saba, watakuwa na mkutano katika Chumba Namba 219.

Kaimu Katibu wa Kamati ya Waheshimiwa Wabunge wote wa CCM, Mheshimiwa Hussein Mzee, anatangaza kwamba leo tarehe 28, saa saba mchana, kutakuwa na kikao chao katika Ukumbi wa Pius Msekwa.

Waheshimiwa Wabunge, haya ndiyo matangazo niliyonayo leo. Ningependa pia kutoa taarifa kwamba, kufuatana na sherehe ambazo ziliandaliwa kwa mfulululizo na Idara ya Utumishi ya Ofisi ya Rais, Bunge kwa mara ya nne mfululizo tumeshiriki Maonesho ya Wiki ya Utumishi wa Umma, ambayo huratibiwa na Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma. Mwaka huu Maonesho haya yamefanyika kuanzia tarehe 16 hadi tarehe 23 Juni, 201 na walijikita katika kuonesha na kuelezea Utumishi wa Umma tangu nchi yetu ipate Uhuru, miaka hamsini iliyopita. Ofisi ya Bunge, chini ya uratibu wa Idara ya Elimu kwa Umma, Habari na Uhusiano wa Kimataifa, pia imeshiriki Maonesho haya kwa umahiri mkubwa na hivyo, kutunukiwa Kombe na Cheti kwa kuwa Mshindi wa Pili. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge, katika Maonesho haya, Ofisi ya Bunge, imeshiriki kwa kutoa elimu kuhusiana na wajibu na majukumu ya Bunge kwa Wananchi, ambao walitembelea banda letu na hivyo kuwafanya waelewe vyema nini Bunge lao linafanya. Aidha, kwa kutumia Maonesho haya, Wananchi wameweza kutambua umuhimu wa kufuatilia kwa umakini, maamuzi yanayotolewa na Bunge.

Kwa kuwa Bunge ni chombo chenye madaraka, kwa niaba ya Wananchi kuisimamia na kuishauri Serikali na vyombo vyake vyote katika utekelezaji wa majukumu yake, ninapenda kuwahimiza Wananchi ambao watapata nafasi kufika kwenye Banda la Bunge wakati wote wa Maonesho ya Sabasaba, ambayo Bunge linashiriki kule Dar es Salaam, yaliyoanza leo na Maonesho ya Nane Nane ambayo yatafanyika hapa Dodoma ili kupata elimu. Aidha, pamoja na Maonesho haya, tunategemea kuanzisha Vipindi Maalum kwenye *television* na redio, ambavyo vitatumika kwa lengo la kuwaelimisha Wananchi, lakini pia kuwa karibu nao maana Bunge ni chombo chao. Ninaomba kuwasilisha Kombe pamoja na Cheti, tulivyokabidhiwa na Mgeni Rasmi, Mheshimiwa Dkt. Mohamed Shein, Rais wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, Siku ya Kilele cha Maadhimisho ya Wiki ya Utumishi wa Umma, tarehe 23 Juni, 2011.

Waheshimiwa Wabunge, Cheti chetu hiki hapa na Kombe letu pia hili hapa. Mkiingia Ofisi ya Spika mtakuta makombe haya yapo mengi; ahsante sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, somo hili la Bunge tutaendelea kulitolea maelezo kwa Wananchi waweze kuelewa, maana mara nyingine wanaweza kuanza kutafsiri vitu ambavyo sivyo. Bunge lolote linaendeshwa kwa Kanuni na siyo vinginevyo, kwa sababu tukiendesha Bunge kwa utaratibu mwingine wowote, tutagombana hapa halafu ugomvi huu hautakuwa na uamuzi wowote. Kwa hiyo; ni wajibu wetu kuwaelewesha Wananchi Kanuni hizi zinavyotumika. Ninawapongeza waliokwenda kufanya kazi hiyo kwa niaba yetu na Waheshimiwa Wabunge, tufanye kazi kwa kufuata Kanuni zetu, tutapata heshima tunayostahili kwa Wananchi. Ahsanteni sana.

## HOJA ZA SERIKALI

### Makadirio ya Matumizi ya Serikali kwa Mwaka 2011/2012 - Ofisi ya Waziri Mkuu na Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa

*(Majadiliano yanaendelea)*

**SPIKA**: Waheshimiwa Wabunge, kama nilivyosema, tunaendelea kujitahidi kuwaita wale waliopo kwenye orodha na siyo vinginevyo ili tumalize majina yaliyostahili. Sasa ninamwita Mheshimiwa Lediana Mng’ong’o; ninaona hayupo. Mheshimiwa Eugen Mwaiposa, atafuatiwa na Mheshimiwa Dkt. Mary Manjelwa na Mheshimiwa Beatrice Shellukindo atafuatia. Mheshimiwa Eugen Mwaiposa, tafadhali.

**MHE. EUGEN E. MWAIPOSA:** Mheshimiwa Spika, ninaomba nichukue nafasi hii, nikushukuru kwa kunipatia nafasi ili na mimi niweze kuchangia katika Bajeti ya Waziri Mkuu. Niungane pia na wenzangu ambao wamekwishachangia, kuipongeza Serikali pamoja na Wizara husika, kwa kuleta Bajeti nzuri, ambayo ina mwelekeo ambao tuna matumaini makubwa kwamba, itatatua sehemu kubwa ya kero za Wananchi wa Jimbo la Ukonga pamoja na Watanzania kwa ujumla.

Mheshimiwa Spika, pamoja na uzuri wa Bajeti, nimeona kuna umuhimu mkubwa wa mimi kuchangia katika baadhi ya vipengele ili kuweza kukamilisha uwakilishi wangu kwa Wananchi wa Jimbo la Ukonga. Nitachangia kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, katika kipengele changu cha kwanza, nitaanza kwa kuchangia vitu ambavyo wamenituma Wananchi wa Jimbo la Ukonga, lakini baadaye katika kipengele cha pili, nitajitahidi sana kuzungumzia baadhi ya vipengele ambavyo vimechangia sana katika umaskini wa Wananchi wa Tanzania.

Mheshimiwa Spika, Jimbo la Ukonga lipo pembezoni sana mwa Mkoa wa Dar es Salaam, kwa jina ambalo Wananchi wa Mkoa wa Dar es Salaam waliliita lile Jimbo wanasema ni Jimbo la Shamba; kwa sababu hiyo, basi miundombinu ya Jimbo ile imekuwa ni mibaya kwa sababu ya kuwa pembezoni. Nianze kuzunguzia Miundombinu ya Barabara.

Mheshimiwa Spika, kwa heshima kubwa, ninamwomba sana Waziri Mkuu, aliangalie Jimbo la Ukonga katika suala la barabara, kwa sababu pamoja na kuwa pembezoni, kuna barabara moja tu ya *TANROAD* inayoanzia pale *Airport* kuelekea Msongola.

Barabara nyingine ambazo ni nyingi sana zipo katika kiwango cha changarawe. Ipo Barabara moja ya Banana ambayo imejengwa takriban miaka 20 sasa, lakini haijafika hata kilomita ishirini, nilikuwa ninamwomba Waziri Mkuu atusaidie ili tuweze kupata barabara za lami, ambazo zitachangia sana kuendelea kuwapa moyo wa kiuchumi Wananchi wa Jimbo la Ukonga.

Mheshimiwa Spika, pamoja na tatizo hilo la barabara, ninaomba nizungumzie bajeti ndogo sana ambayo Barabara ya Banana inapewa. Kwa miaka yote hiyo niliyoisema, barabara hiyo inajengwa kila mwaka nusu kilomita, ambayo haioneshi au haileti *impact* kabisa katika kushirikisha Wananchi katika kuleta maendeleo. Ninaomba sasa Serikali ifike mahali itenge fungu kubwa kwa ajili ya kutengeneza barabara ili *impact* iweze kuonekana.

Mheshimiwa Spika, pamoja na hilo, ninaomba nizungumzie suala la foleni kwa Mkoa wa Dar es Salaam kwa upande wa Jimbo la Ukonga. Wafanyabiashara na Wafanyakazi sasa wanachukua karibu muda wa saa mbili kutoka Ukonga au Msongola mpaka kufika Mjini kwa sababu ya foleni. Ninatambua kabisa kwamba, Serikali imekuwa na mipango mingi, kwa ajili ya kukwepa hili suala la foleni, lakini ninaomba Waziri Mkuu aangalie upya suala la kutumia treni ambayo ingeweza kuchukua Wananchi wa Msongola, Pugu, Kitunda na mahali pengine hasa wakati wa asubuhi na wakati wa jioni kuwamwaga mjini. Upo utaratibu mwingine ambao ungeweza kutumika, mwezi uliopita niliweza kufanya tathmini ndogo tu, magari mengi ambayo yanajaza foleni ni magari ya watu binafsi; magari ambayo yanachukua mtu mmoja mpaka watu wawili au watatu.

Mheshimiwa Spika, ninafikiria kwamba, Serikali iangalie kutumia utaratibu wa kupanga ni magari ya aina gani yataingia mjini hasa wakati wa asubuhi na wakati wa jioni. Mfano, wangeweza wakasema kwamba, magari yanayochukua watu wasiopungua kumi na nane basi yasiingie mjini kwa muda wa asubuhi, waanze kuingia mjini alfajiri mpaka saa kumi na mbili, kuanzia saa kumi na mbili mpaka saa mbili basi yaanze kuingia mabasi na magari mengine ambayo yanachukua wanafunzi wengi. Kwa hiyo, magari yapangiwe ni muda gani wa kuingia na kutoka Mjini.

Mheshimiwa Spika, utaratibu huu umetumika katika nchi nyingi na wameweza kufanikiwa kwa kiwango kikubwa, kuliko Wananchi kupoteza muda wa saa nne kwenye foleni, magari mawili kwenda na mawili kurudi, basi itasaidia sana muda huu kutumika katika utaratibu wa kiuchumi zaidi.

Mheshimiwa Spika, sambamba na hilo, ninaomba nichangie katika suala la umeme. Kama nilivyosema, Jimbo la Ukonga lipo pembezoni, zaidi ya robo tatu ya eneo hilo halina umeme. Ninaomba sana Waziri anayehusika pamoja na Waziri Mkuu, watusaidie ili tuweze kupata umeme. Hakuna kitu ambacho kinaweza kikasaidia *TANESCO* kuendelea kupanua wigo ili waweze kuendelea kupata wateja wengi zaidi.

Mheshimiwa Spika, ninashauri kwamba, kwa sababu Wananchi wa Jimbo la Ukonga wana kipato cha chini, ninaomba *TANESCO* ifanye utaratibu ili Wananchi hawa waweze kuweka umeme kwa wingi, lakini kwa kutumia mkopo.

Ninalisema hili kwa sababu, kwa utaratibu wa *TANESCO,* kama unataka kuweka umeme ile *initial payment* tu ya kwanza kama umbali labda hauzidi mita 30 na ni *single phase,* inakugharimu shilingi laki nne na sitini na nane. Siyo rahisi kukuta Wananchi wengi wana umbali huo, umbali unakuwa ni mkubwa, kwa hiyo, wanahitajika sana kutumia fedha mpaka shilingi milioni mbili mpaka milioni tatu kwa ajili ya kuweka umeme kwa mara ya kwanza. Ninaomba *TANESCO* iangalie ni namna gani inaweza kuwakopesha Wananchi kwa *initial payment* ili fedha hizi ziweze kulipwa kidogo kidogo wakati wanapokuwa wanalipa bili zao za umeme.

Mheshimiwa Spika, lakini pia katika utafiti nilioufanya, kwa sababu tatizo la umeme limekuwa kubwa sana Tanzania, nimegundua kwamba, *TANESCO* inadai fedha nyingi sana kwa Wizara, lakini pia hata taasisi nyingine na wafanyabiashara wengine wakubwa na wadogo. Ninaomba Waziri Mkuu aangalie, kwa sababu mpaka sasa hivi Wizara tu zinadaiwa zaidi ya bilioni themanini na sita kutoka katika Wizara mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, nilikuwa ninajiuliza kama Wizara hizi zinaleta bajeti katika Bunge hili na tunazipitisha; inakuwaje hawalipi fedha hizi kwa *TANESCO* ili waweze kuendelea na Miradi ya Umeme? Ninaomba Serikali watumie utaratibu wa kwamba, Bunge likipitisha bili ya umeme na bili ya maji kwa Wizara, basi fedha hizi ziweze kwenda kulipwa moja kwa moja katika Wizara ya Nishati ili zisiweze kuchakachuliwa tena katika Wizara nyingine. Jambo hili litasaidia sana *TANESCO* iweze kuendesha miradi yake vizuri.

Mheshimiwa Spika, ninaomba sasa niendelee kuchangia katika kipengele cha maji. Maji ni kilio kikubwa sana kwa Wananchi wa Jimbo la Ukonga. Ninamwomba Waziri atusaidie kupata visima vikubwa, ambavyo vitatusaidia kusambaza maji kwa sehemu kubwa ili Wananchi wengi waweze kupata maji.

Mheshimiwa Spika, nizungumzie suala la kuhamisha rasilimali watu kutoka sehemu mbalimbali za mjini ili kupisha upanuzi wa maendeleo mbalimbali ya Serikali. Kama nilivyosema, Serikali inaliangalia sana Jimbo la Ukonga na kuhamishia huko watu wake, lakini cha kushangaza, Serikali imeshindwa kuanza kuandaa miundombinu ambayo itasaidia watu hawa kuweza kuishi vizuri kama walivyokuwa wanaishi mijini. Ninaomba sana Serikali iangalie, kabla haijahamisha rasilimali watu kwenda sehemu yoyote, wahakikishe kwamba, kuna umeme, kuna barabara, kuna maji na miundombinu mingine ambayo inaweza kuwafanya Wananchi hao waishi vizuri.

Mheshimiwa Spika, katika hili la kuhamisha watu, nizungumzie watu waliohamishwa kutoka Kipawa kwenda Kata ya Pugu Kinyamwezi. Kulikuwepo na shule ambayo ilikuwa pale Kipawa na walipewa fedha zao, lakini mpaka hivi sasa Serikali haijaweza kutoa zile fedha ili wale wanafunzi waliohama na wazazi wao waweze kujengewa shule.

Mheshimiwa Spika, ninakwambia nimetembelea Shule ya Viwege, ina wanafunzi 900 lakini ina madawati 60 tu! Kwa hiyo, limekuwa ni tatizo kubwa sana katika Jimbo la Ukonga hasa Kinyamwezi, ambako Wananchi hawa walihamia. Ninaomba zile fedha zitoke kwa sababu ipo sehemu ya kujenga shule ili shule ile iweze kujengwa.

Ninaomba niende moja kwa moja katika eneo la Bangulo. Eneo la Bangulo lipo katika Kata ya Pugu. Wananchi walioko pale ni zaidi ya 800 na walihamishiwa pale mwaka 1973 wakati wa Operesheni ya Vijiji walipelekwa pale na Serikali. Pamoja na kwamba, eneo lile lilikuwa la Wizara ya Uvuvi na Mifugo, mpaka sasa Wananchi wale wameendelea kujenga nyumba zao za kudumu. Cha kusikitisha, wameletewa barua sasa kwamba, wanatakiwa wavunjiwe zile nyumba zao.

Nilikuwa ninaomba, kwa sababu Serikali inahangaika sana kuhakikisha uchumi wa Wananchi unakua; iangalie ni namna gani inaweza kuwaacha wale Wananchi sehemu ile na kutafuta eneo lingine kwa ajili ya kufanya shughuli zake za maendeleo, kwa sababu katika Jimbo la Ukonga, yapo maeneo makubwa ambayo bado hayajaendelezwa na Wananchi.

Mheshimiwa Spika, ninaomba niongelee pensheni. Wazee wetu ambao ndiyo waliofikisha uchumi wa nchi kufikia mahali hapa, wanalipwa kati ya shilingi 20,000 mpaka shilingi 50,000. Fedha hizi ni nyingi sana kama akipewa mtu ambaye ana nguvu ya kuweza kuzitumia na kuweza kuongeza thamani fedha nyingine. Kwa wazee wetu imekuwa ni tatizo kubwa hasa ukizingatia kwamba, mpango wa Serikali wa kuwapatia matibabu bado unasuasua sana katika zahanati zetu. Nilikuwa ninaomba Serikali iangalie ni namna gani inaweza ikawaongezea wastaafu fedha za kuwawezesha kutatua matatizo yao ya kawaida.

Wapo wazee wengine ambao hawakuwa wameajiriwa, lakini walikuwa wafanyabiashara, wakulima na wavuvi. Wamechangia kwa kiwango kikubwa katika kuhakikisha kwamba, uchumi wa nchi hii unakua, lakini hawapati pensheni. Ninaiomba Serikali ianze kujipanga sasa na kuangalia ni namna gani wanaweza wazee hawa nao wakapata pensheni kwa namna ya pekee.

Mheshimiwa Spika, ninaunga mkono hoja hii na ahsante. *(Makofi)*

**MHE. DKT. MARY M. MWANJELWA:** Mheshimiwa Spika, ninakushukuru sana kwa kunipa nafasi na mimi niweze kuchangia Hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu. Vilevile ninampongeza sana Mheshimiwa Waziri Mkuu na timu yake nzima, kwa Hotuba nzuri, yenye mantiki ambayo inaendana na Dira ya Maendeleo ya Mpango wa Miaka Mitano ijayo. Nitakuwa mchoyo wa fadhila, nisipowashukuru Wanawake wote wa Mkoa wa Mbeya hususan wana UWT, kwa kuendelea kunipa ushirikiano wao. Ninawashukuru sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninaomba niipongeze sana Hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, kwa sababu amezungumzia masuala ya Vitambulisho vya Taifa. Tunapozungumzia Vitambulisho vya Taifa tukumbuke kwamba, hatujawa na Mradi wa *Physical Address*. Tunaweza tukawa na Vitambulisho vya Taifa, *yes,* lakini ni sawasawa na kuwa na gari ambalo halina *engine*. Ningeiomba Serikali kupitia Wizara husika, ianze kwanza na Mradi wa *Physical Address,* ambao utakuwa una *zip code,* baada ya hapo ndiyo tuzungumzie suala la Vitambulisho vya Taifa. Kwa sababu tukianza kuwa na Vitambulisho vya Taifa kabla ya Mradi wa kuwa na *Physical Address,* tunaweza tukajikuta Serikali inapoteza fedha nyingi sana. Unakuwa na Vitambulisho vya Taifa, lakini kunakuwa na jina tu na anwani, huna *contact* za huyu mtu. Kwa hiyo, zoezi zima linakuwa halina faida. Ninaomba  Serikali ilione hilo na ijaribu kuliangalia. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kitu kingine ni kuhusu suala la kodi. Serikali yetu inategemea sana kodi.  Pato kubwa lipo kwenye kodi. Ningeomba Serikali ifanye utaratibu wa kuendesha semina kwa wafanyabiashara wetu hawa ili kuwahamasisha, wapewe *sensitization,* umuhimu wa kukusanya kodi ili Serikali iendelee kupata pato kupitia kodi mbalimbali. Kitu kingine, tunapozungumzia suala hili la kodi, tumekuwa tukipoteza kodi nyingi sana na Serikali yetu inasema uchumi unakua, lakini Wananchi bado wanadorora sielewi kwa nini. Kwa hiyo, ningeomba misamaha ya kodi isiyo ya lazima ifutwe. Ninasema hivyo kwa sababu ukiangalia Sekta ya Madini wapo *exempted,* lakini sasa wanakuwa wanachukua mali ghafi zetu wanapeleka nje ya nchi na fedha inakuwa *circulated* huko huko hairudi nchini na wakati hizo ni mali zetu wenyewe na haya makampuni ya madini unakuta yamekuwa *exempted* katika kodi. Kwa mfano, katika Ripoti ya Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali unakuta kwamba, hii misamaha ya kodi tumepoteza karibu bilioni 680, Sekta ya Madini peke yake bilioni 48 kwa mwaka 2009/2010; hii siyo sahihi hata kidogo. (*Makofi*)

Jambo lingine ambalo ningependa kulizungumzia ni Sekta ya Afya. Tukumbuke kwamba, afya ya mama na mtoto ni muhimu sana.  Humu ndani wote wamezaliwa na

wanawake, ni kweli Serikali ninaipongeza inatilia mkazo mambo mengi ya muhimu hususan miundombinu, lakini Sekta ya Afya, ninaomba izingatiwe sana. Katika Kitabu cha Hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, ukurasa wa 45 umezungumzia vifo vya mama na mtoto. Hii hali hairidhishi. Ningeomba Serikali iongezewe fungu. Nimekuwa nikiongea na Mheshimiwa Waziri wa Afya mara nyingi sana, yuko *very positive and supportive*, lakini sijui Azimio la Abuja lile la asilimia 15 tutalifikiaje na wala sielewi Mpango wa *Millennium Goal* Namba Tano na Sita tutafikiaje kama afya ya mama na mtoto hatuizingatii?

Hawa ndiyo walio wengi katika kuendeleza na kukuza uchumi. Tunakumbuka masuala ya barabara na mengineyo, lakini afya ya mama na mtoto tumesahau kabisa, ninaomba hili jambo lizingatiwe kwa sababu Bajeti haijaakisi kabisa usawa wa kijinsia, kwa maana ya kuinua afya ya mama na mtoto. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ni mzigo wa kuiendesha Serikali Kuu usambazwe mikoani. Tunazungumzia masuala ya *Decentralization by Devolution (D by D);* kweli ni jambo zuri na la msingi. Vilevile ningeomba sana hizi Manispaa zetu ziwezeshwe Mikoani ili waweze kuwa na *Municipal Bonds*, kwa maana ya kwamba, watakuwa na hisa zao wenyewe, watajiendesha na wataweza kukuza uchumi wao, kwa maana wanaweza wakawa wamekuwa *empowered. (Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lingine, ningependa kuzungumzia suala la elimu. Ninaishukuru sana Serikali, imekuwa ikitoa ruzuku ya shilingi 25,000 kwa kila mwanafunzi ingawa wanatoa 7,500. Serikali iangalie suala la ku-*control* ada kwa shule zetu za binafsi. Kwa sababu kuna watoto wengi sana wenye kipato cha chini, hawawezi kumudu shule za *private* na wao wangependa kwenda kwenye shule hizo waweze kupata *better facilities*, lakini hawawezi. Kwa hiyo, ningeiomba sana Serikali iliangalie hilo.

Vilevile kwenye Bodi ya Mikopo wakati mwingine tunazungumzia masuala ya migomo. Bodi ya Mikopo nayo inachangia kuleta migomo kwenye Vyuo Vikuu. Ninasema hivyo kwa sababu utaratibu wake hauridhishi, kwa maana ya kwamba, kuna wengine ni watoto ambao wana uwezo wa kipato cha juu, lakini bado wanaendelea kupewa hii mikopo na Bodi. Sasa wale watoto wa kipato cha chini ambao na wao wangependa kufika kwenye Vyuo Vikuu watafanyaje, maana unakuta kwenye hivyo Vyuo Vikuu bado kuna watoto wenye uwezo wamepewa mikopo na bado wanaendelea kuwasaidia wasiokuwa na uwezo. Sasa wasiokuwa na uwezo wafanye nini? Ninaomba Bodi ya Mikopo iliangalie hili na ijaribu kufanya utaratibu mzuri, ambao utawawezesha wale wengi wa kipato cha chini waweze kunufaika na hii mikopo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nisingependa kuzungumza mengi sana, lakini nitakuwa sijatenda haki, nisipozungumzia suala la Uwanja wa Kitamaifa wa Songwe Mkoa wa Mbeya. Hili jambo limekuwa likiimbwa sana. Ninamshukuru Waziri muhusika, siku nne zilizopita alitembelea huo Uwanja, lakini kwa kweli bado tunaendelea kusisitiza, hili suala wengine kabla hata hatujaingia hapa Bungeni tumekuwa tukilisikia, imekuwa ni wimbo kwamba utakwisha, utakwisha. Imekuwa ni hadithi na historia ambayo haitekelezeki. Ningeomba ifike mahali sasa Serikali iwe na *legacy*, utekelezaji ufanyike,

kwa sababu huu Mkoa wa Mbeya na Uwanja huu tukumbuke kwamba, ndiyo *gate way* ya nchi zote jirani za Kusini pamoja na Mikoa yake.

Kwa hiyo, tunazungumzia uchumi ni kwamba, upo tu *obvious* utakua. Tunaambiwa mwezi Desemba ndege zitaanza kutua na kupaa pale; ninaomba hili jambo liwe kwa vitendo ili tushuhudie tusiendelee kupiga kelele.

Baada ya kuzungumza haya, ninaomba nisichukue muda mwingi, ninaunga mkono Hoja ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, kwa asilimia mia kwa mia. Ahsante. *(Makofi)*

**WAZIRI FULANI:** Mheshimiwa Spika, ninaomba nitoe taarifa kuhusu utoaji wa mikopo kutokana na Kanuni ya 64 …

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri, ninakushukuru sana, lakini ninaomba watakapokuwa wanajibu watajibu maana tulikubaliana tukiwa na taarifa nyingi tutaharibu ratiba yetu. Ninaamini kabisa wenyewe wamelichukua watajibu na wataweza kusaidia kujibu wakati huo. *(Makofi)*

**MHE. BEATRICE M. SHELLUKINDO:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi na mimi ya kuchangia. Awali ya yote, niseme ninamshukuru sana Mwenyezi Mungu, kuweza kurudi katika Jengo hili; ni kwa neema yake nimeweza kuwepo mahali hapa. (*Makofi*)

Vilevile ninachukua fursa hii kwa sababu ninaongea kwa mara ya kwanza, kuwashukuru sana Wananchi wa Mkoa wa Kilindi, kwa imani kubwa waliyonipa na kunipa kura za kishindo na kuweza kuongoza katika tano bora kwa kura nyingi katika nchi hii. Ninakushukuru sana. (*Makofi*)

Wananchi wa Kilindi, wameonesha wao hawajali fedha na maneno ya uchafuzi, wanachojali ni maendeleo yao. Kwa hiyo, Wananchi wote angalieni maendeleo yenu na siyo vinginevyo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, ninakusudia kuongea maneno mazito, magumu na pengine ambayo yatawaudhi watu, lakini ndiyo imani yangu, ndiyo fikra zangu na ndiyo upeo wangu. Kwanza kabisa, ninaomba niwashukuru wapigaji wangu wote walionisaidia kampeni yangu; ni wengi mno siwezi kuwataja kwa majina, wengine sikuwa ninawafahamu; Masheikh, Wachungaji, Maaskofu, akina Saluki, Nkaka, Kingalangala, wengi ninashindwa kuwataja wote, lakini wote ninawashukuru sana. Kwa sababu muda ni mdogo, inabidi niende haraka haraka.

Nichukue fursa hii, kukupongeza Spika wetu Mwanamke. Tanzania tumeonesha, juzi nilikuwa kwenye mkutano nikakuta watu wanatamba wana Spika Wanawake nikasema jamani Tanzania tuna Spika Mwanamke. Kwa hiyo, ni sisi tunajiringia, hii imedhihirisha kwamba, wanawake tunaweza. Ninaamini kabisa hata huko juu zaidi tunaweza tukaonesha miujiza mwaka 2015. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nichukue fursa hii, kwa sababu nina mengi kidogo na muda ni mfupi, nimpongeze sana Waziri Mkuu, pamoja na Mawaziri wa Nchi, TAMISEMI, Mheshimiwa George Mkuchika, Naibu Mawaziri, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (Sera, Uratibu na Bunge), Mheshimiwa William Lukuvi, Makatibu Wakuu na hasa Bwana Lyimo na hapa ninaomba nimtaje maalum Bwana Maswi; Bwana Maswi amekuwa ni uti wa mgongo kwa Halmashauri nyingi; ninaomba nimtaje kipekee. *(Makofi)*

Ninakipongeza sana Kitengo cha Maafa, kilitusaidia sana Kilindi tulivyopata shida na hapa nimtaje maalum, mtumishi mmoja, Afisa Chinyuka; alifanya kazi usiku na mchana; ni vyema kuwatambua watu wakajisikia na wao kwamba tumewajali. Ninawapongeza Watumishi wote wa Ofisi ya Waziri Mkuu, kwa kazi nzuri iliyopelekea kuletwa Bajeti nzuri. *(Makofi)*

Ninaomba nimpongeze Mkuu wangu wa Mkoa, Afande Kalembo, pamoja na Ofisi yake. Ninampongeza sana Mkuu wangu wa Wilaya, Gishuli Charles, pamoja na Ofisi yake, Mkurugenzi aliyekuwepo Kudra Mwinyimvua, ambaye sasa ni *RAS* Tabora na aliyepo sasa hivi Bibi Mnyamagola, Madiwani wote, pamoja na Watumishi wote. *(Makofi)*

Ninaomba nichukue fursa ya kumshukuru mtu mmoja kipekee, mimi amenijenga, amenipa *confidence,* amenipa uelewa, amenipa ujasiri na uwezo; huyu si mwingine bali ni Spika aliyepita, Mheshimiwa Samuel Sitta,; ninakushukuru sana. *What I am to day,* mchango wako ni zaidi ya asilimia 50. Ahsante sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nina mengi ya kuyasema hapa, lakini nilikuwa ninasema nikumbuke tu *NIDA,* hawa wa vitambulisho. Kipekee, ninaomba niwapongeze; ni jambo ambalo nimelibeba sana tangu safari iliyopita hadi sasa na Wabunge wote kwa pamoja na sasa tumefikia hatua nzuri. Kwa hiyo, hili niliona niligusie hapa. (*Makofi*)

Nina mengi ya kusema ambayo Wananchi wa Kilindi wamenituma, lakini kubwa walilonituma ni shukrani zao kwa yote waliyofanyiwa na Serikali. Mheshimiwa Waziri Mkuu, atambue Kilindi tunamshukuru kwa yote; umeme, barabara kupandishwa hadhi, maji na mifugo; kila eneo tumeguswa. Kwa kweli sisi tunasema ahsante sana, tumepata Kata tano na Vijiji vitano. (*Makofi*)

Vilevile bado tuna maombi madogo madogo, ambayo nitayatoa wakati wa sekta husika, mathalani la barabara. Barabara kutoka mashambani kwenda kwenye masoko mijini, unakuta gunia la mahindi linauzwa mpaka shilingi 8000 mpaka 10,000, kwa sababu barabara ni mbovu. Haya yote ninayoyasema ninawaahidi Wananchi wangu nitayazungumza Sekta hadi Sekta ila moja au mawili makubwa ambayo ninaomba niseme ni *GN* ya Ardhi. Kulikuwa na mgogoro wa ardhi mkubwa sana wa mpaka wetu kutoka Pagwi hadi kupita Nkama kwenda mpaka Mafisa na kadhalika. Kazi hii Mheshimiwa Waziri Mkuu, alitoa agizo hili mwaka 2009 hadi leo *GN* haijatoka. Kwa hiyo, inasababisha migogoro watu wa upande wa Kiteto wanaingia na watu wa Kilindi

wanakwenda; inasababisha mauaji. Ninaomba nilisemee hili. Kubwa zaidi ya yote, Bwawa la kwa Maliga, ambalo lilivunjika juzi, ambalo linasaidia vijiji zaidi ya tisa na mifugo zaidi ya 24,000. Hili tunaomba msaada Mheshimiwa Waziri Mkuu. Masuala ya mitandano tayari tunawasiliana na wahusika, nitayasema wakati husika.

Mheshimiwa Spika, nimesema nitasema mambo magumu mawili; ninaomba Wananchi mnivumilie lakini ndiyo ukweli wenyewe. Wananchi wanauliza na mimi nimeulizwa sana na Wananchi; hivi hili Bunge ndiyo kazi tuliyowatuma mwende mkafanye kule? Ndugu zangu Wabunge, tupo hapa kwa sababu ya Wananchi, Jengo hili Tukufu na Takatifu ni kwa ajili ya kujadili maslahi ya Wananchi kero zao, kutunga sheria kwa maslahi yao, kusimamia masuala mbalimbali ya mihimili mingine mahali hapa siyo vinginevyo. Wanashangaa sana, wengine nilikaribishwa kwenye sherehe kwenye ubalozi fulani hata wao wanashangaa tumegeuza Bunge sasa limekuwa uwanja wa kuonesha umaarufu wa vyama, umaarufu wa kuonesha utashi wa kila mtu, nani anaweza kuongea zaidi ya wengine. Nilishangaa, juzi nimekaa mpaka Waziri Mkuu, ameshika tama anashindwa kuongea, Mawaziri wamekaa wanashangaa nini hiki? Imekuwa ni jopo lingine. Kama tunawafikiria tunawafurahisha Wananchi, Wananchi huko wanauliza kulikoni.

Tuna viwanja vingi, tukitoka hata nje ya Ukumbi wa Bunge hapo kuna waandishi wa habari wamejaa, tuna viwanja, tuna *stadium*, tuna majimbo yetu, tuna Mikoa yetu, kuna nchi nzima hapa ndani, tufanye kazi tuliyotumwa kufanya na siyo vinginevyo ama sivyo tutakuwa tunajichanganya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, niombe sana Wabunge tuungane bila kujali itikadi zetu, bila kujali utashi na matamanio yetu, tutekeleze kazi ambayo tumetumwa kufanya hapa kwa kuzingatia heshima na siasa, siyo kukosa adabu, lazima umheshimu aliye mkubwa zaidi yako, si kwa cheo tu hata kwa umri, kuna namna ya kumweleza akaelewa siasa, kuna lugha ya kisiasa.

Mheshimiwa Spika, huwa ninashangaa unaposema kwamba, aah bwana tafadhali watu wageni hawajui, watu wanajua wanachokifanya, wana ajenda za kijingajinga, sasa hizo lazima tuzikemee kuanzia sasa turudishe heshima ya nyumba hii. Unafika mahali unaogopa hata kuitwa Mheshimiwa kwa sababu gani? Kwa kweli mimi ninaomba hilo. *(Makofi)*

Ndugu Wananchi wanasema, alah, samahani, Mheshimiwa Spika, ninawaambia Wananchi. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, ninawaambia ndugu zangu Wananchi wanasema, akili ya kuambiwa changanya na zako, yote yanayosemwa humu ndani mengine ni siasa, unashangaa, kwa mfano, mimi nimefika hapa nikakuta hoja ya posho imepamba moto, nilikuwa Rwanda, ninasikia posho; posho jamani tusidanganywe. Mbunge ambaye anafanya kazi yake ya ukweli kwa Wananchi wake, lazima hii posho anaijua umuhimu wake. Wananchi wa Kilindi wanajua umuhimu wa hii posho. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, *weekend* huwa ninakwenda Jimboni; juzi Jumapili na Jumamosi nilikuwa kwenye Kamati ya Fedha, Wananchi wa Kilindi, wanajua umuhimu wa posho na mimi ninajua umuhimu wake; kuna mambo unakuta lazima uyasaidie. Sasa watu wengine labda pengine hawafanyi kazi zao vizuri, wanaona posho siyo muhimu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, lakini pia Wananchi waelewe wengine wana wafadhili wao, lakini vilevile humu ndani tunajuana vizuri, yale yanayosemwa humu ndani, tukitoka nje habari ni tofauti. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, ninataka kuwatahadharisha Wananchi kuwa, siyo kila linalosemwa watu wanashikia bango. Mambo yanayosemwa humu ndani, eeh fulani kasema, ile ni unafiki wa kisiasa wenye ajenda nyuma yake. Tusimame kwenye mambo ambayo yanaleta maslahi kwa Wananchi na Bunge letu liheshimike, tukitoka nje tufanye majukwaa yetu.

Mheshimiwa Spika, nimalizie na moja; hili nitalisemea kidogo, kuna usemi wa Kiganda, nilivyokuwa kwenye Bunge la Afrika Mashariki na Mheshimiwa Mwakyembe ataukumbuka, walikuwa wanasema; ukiwachukua panzi ukawatia kwenye chupa ukafunga ile chupa, wale panzi watarukaruka, watakosa chakula, wataanza kuumana. Tanzania tupo ndani ya chupa, ndiyo maneno ninayotaka kuwaambia. Maana yake unashangaa, kuna mambo mengi yanafanyika, sisi tuko ndani, tumejifunga na umaskini, tunaambiwa na vitu mbalimbali tuko hapa. Sasa hivi, fursa za biashara nje, juzi Rwanda tunaambiwa na Ubalozi, Wanyarwanda wanakuja Tanzania, Kahama sijui wapi Karagwe wanabeba mchele, mpunga na vitu mbalimbali, wanapeleka kule.

Unaangalia hapa nchi jirani ya Kenya, wanakuja wao wenyewe wananunua sisi tumekaa hatuangalii hizo fursa. Tuko ndani ya chupa, tunaumana wenyewe kwa wenyewe, leo ooh sijui nani alikuwa CCJ; CCJ inasaidia nini saa hizi? Wananchi wanaumia, njaa kule inawanyemelea, umeme hakuna, ajira hakuna, mnakaa mnazungumza mambo ambayo hayana maana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, rasilimali zipo mbalimbali, madini kila kitu, lakini unashanga bado tunazidi kuwa maskini; tupo ndani ya chupa. Ma-*blog* yameanzishwa huko na *website* sijui *Jamii Forum*, tunachafuana wenyewe kwa wenyewe, tunajianika wenyewe kwa wenyewe, watu wanatushangaa. Siasa za kuchafuana ndiyo usiseme, hakuna kuangalia mkubwa wala mdogo, mtu mradi ana mdomo wa kusema anasema, tuko ndani ya chupa. Maalbino wanauawa; ulisikia wapi duniani? Tupo ndani ya chupa. Mambo mengine, kupasua mguu badala ya kichwa, kichwa badala ya mguu, tupo ndani ya chupa.

Msishangae haya mambo yote yanatokea kwa sababu tumo ndani tumefungwa, hatutaki kufunguka tunasingizia umaskini. Kuna kitabu hapa ninasoma; "*The Trouble With Africa*", visingizio ndiyo vinavyotumaliza, mambo mengi. Vilevile misaada inatolewa haifiki kwa walengwa, kwa nini tumefungwa, sisi tupo tunaumana tu, huyu hivi *story*, *story*, fulani aah! Waziri Mkuu aah! Nini? Wafadhili wanaelezwa upungufu wetu, watu wanatoka wanakwenda kueleza wafadhili upungufu wetu ili wakate misaada

au sijui ili iwe nini, halafu tunafaidika nini; ni kwa sababu tumefungwa, *we can't think*. Tumefungwa pale. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, tofauti za walio navyo na wasiokuwa navyo, ajira vijana hakuna ndiyo maana ukiwaita tu barabarani njooni muandamane, wanakuja *one time*, hawana ajira, tumefungwa hatuoni hayo. (*Makofi*)

Ukabila, udini, maamuzi kutotolewa kabisa na saa nyingine kutolewa yakiwa yamechelewa, tumefungwa ndani ya chupa. Wasomi wanakosa ajira, watu wanagombea Urais wako ndani ya chupa, hamuwezi mpaka tufungue ile chupa tutoke ndiyo mtapata Urais. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tunagombana humu ndani, tunaumana kichikichikichi, Wananchi wanaumia wanashangaa, mipango isiyokamilika; mabasi sijui ya mwendo kasi, sijui zile barabara za juu, *fly overs*, tunasikia kila siku, utafiti utafiti hela zinaliwa, hakuna kinachoendelea. (*Makofi*)

Badala ya kutumia *opportunities* za kujitangaza, jana Mheshimiwa Telele amesema, tumekazana Babu Samunge mchawi, mwongo, nini tunaumana; wenzetu wanatangaza Utalii, watu wanapita kwao wanapata hela. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Kilimanjaro, Serengeti, vinatangazwa sisi tuko ndani ya chupa tunaumana, huyu kachukua, karudisha, kapandisha, kashuka. *(Makofi/Kicheko)*

Magazeti nayo yako ndani ya chupa, unatoa picha ya Waziri au Mbunge amefunga macho Bungeni, hiyo ni sababu gani? Yeye ni mwanadamu anaweza akawa ameamka anaumwa, amechoka kusikiliza, pengine anatafakari hivyo huna haja gani? Sisi ni wanadamu pia, haya yanawasaidia nini Wananchi? Kwa sababu watu hawataki kutoa habari za kutuendeleza, za kutufungua Tanzania twende sawa na wenzetu, tupo ndani ya chupa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, vilevile Wakimbizi wa Burundi wampewa uraia, sasa hivi wanatapakaa nchi nzima, sisi wenyewe Wananchi wetu wanapigana, wanauwana, damu zinamwagika, hakuna maeneo, leo mnataka kuwasambaza Warundi wazunguke nchi nzima, tuko ndani ya chupa, hatutaki kufikiri. Vilevile visingizio vingi; tumekosa umeme, viwanda havifanyi kazi, mchakato wa Katiba Mpya, Wananchi hata ya zamani hawaijui wanashangaa tunataka nini, tutoke wapi, twende wapi. *(Makofi)*

Tunaelekea kwenye hatua ya Shirikisho la Afrika Mashariki, nani anayejua hatua zilizopita? Sasa hivi hatuna *option*, tumeshafika mahali lazima tuingie, lakini sisi tuko ndani ya chupa tunalumbana hapa, posho siyo posho, nani siyo nini, vitu visivyokuwa na maana. Watu wenye uwezo waliostaafu, kwa mfano, Mheshimiwa Shellukindo yuko pale nyumbani ni mtu mwenye kichwa, lakini hawatumiki. Wapo wengi sitaki kusema mifano; Mheshimiwa Pius Msekwa hawatumiki, sisi tunajiona tuliobaki hapa ndiyo wenye akili, tuwatumie, yaani ninasema *let's get out of the bottle,* tutoke nje ya chupa na

kwa kufanya hivyo, kila Mwananchi ana kazi yake ya kufanya, aanze kuwaza mbali kuanzia leo. (*Makofi*)

Magazeti yana kazi yake, Serikali, Mahakama, Bunge tuna kazi yetu, Asasi zisizo za Kiserikali, *NGOs* na *CBOs* zote na vilevile Viongozi wa Dini zote, kila mtu ana nafasi yake. Tumwombe Mungu tuondokane na hii adha, tunakokwenda siyo kuzuri. Tunapozunguka kwenye nchi za wenzetu tunasikitika, Rwanda ilikuwa inapigana juzi, sasa hivi wanatuangalia sisi kama kichekesho. Ninaomba sana, nimeyasema kwa uchungu, sina maana yoyote lakini ninasema kwa uchungu.

Mheshimiwa Spika, ninaunga mkono hoja kwa asilimia mia moja. Ahsanteni. *(Makofi*)

**SPIKA**: Haya, mwenye masikio amesikia, tunaendelea. Mheshimiwa Salum Barwany, atafuatiwa na Mheshimiwa Moses Machali na Mheshimiwa Ezekiel Wenje, ajiandae.

**MHE. SALUM K. BARWANY:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi hii kwa mara nyingine tena ya kutoa mchango huu katika Hotuba ya Waziri Mkuu. Kabla ya yote, kwanza, nawashukuru Viongozi wa Chama cha Wananachi *(CUF)*, kwa juhudi kubwa ambazo kwa pamoja wamezifanya katika kuhakikisha kwamba, wanalinusuru Taifa hili kutokana na maafa ambayo yangeweza kutokea kama siyo busara na hekima ya Viongozi hawa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, leo tunazungumzia suala zima la Serikali ya Umoja wa Kitaifa Zanzibar, ambayo baadhi ya watu wanabeza kuwepo kwa Serikali hiyo. (*Makofi*)

Wananchi kwa jumla na Mataifa yote duniani, wanafahamu hali ya kisiasa Zanzibar ilivyokuwa kabla ya Umoja wa Kitaifa wa Serikali kuwepo. Tayari Chama chetu kimeonesha nyao, ndugu zetu wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo huko Arusha nao wamefuata nyao hizi na ninaamini pia mwaka 2015, Jamhuri ya Muungano nayo itakuwa Serikali ya Umoja wa Kitaifa pia. *(Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nije katika hoja muhimu. Miaka mitatu iliyopita, Taifa hili lilishuhudia mauaji makubwa kabisa ya kikatili, ambayo yalililetea Taifa letu fedheha ndani na nje. Mauaji ambayo yanasikitisha, binadamu wa kawaida anadiriki kumwondoa binadamu mwenzake duniani eti kwa mahitaji ya utajiri; hili limeleta fedheha kubwa katika Taifa letu. Pamoja na juhudi za Serikali katika kuhakikisha mauaji haya yanakomeshwa, lakini bado Serikali haijatoa tamko rasmi ni jinsi gani mauaji haya yanaweza kukomeshwa yasiendelee tena. Tunasikia kwamba, Serikali kupitia Mahakama zake, inajitahidi kutoa hukumu kwa wale ambao tayari walihusika na mauaji haya. Moja kubwa ambalo tayari linatakiwa liangaliwe kwa makani ni jinsi gani wale ambao walishiriki katika jambo hili, walikuwa na soko maalum kwa ajili ya viungo vya albino. Tunaamini kwamba, siyo mtu wa kawaida wa daraja la chini aliyekuwa anahusika na mauaji yale. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, haiwezekani; thamani ya kiungo cha albino leo tunaambiwa siyo chini ya milioni mia mbili mpaka milioni mia nne; hivi ni mtu gani mdogo wa kawaida anayeweza ku-*afford* gharama hizo? Tunaamini kabisa kwamba, kuna watu wa daraja la juu waliokuwa wanahusika na mauaji ya albino. Tunaomba Serikali sasa ifanye utafiti wa kina, kujua nani alikuwa soko la viungo vya albino. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nitatoa mfano mmoja; katika miaka ya sitini kulifanyika mauwaji kule katika Mikoa ya Kusini. Kuna M-Asia mmoja alimuua mkewe, alimuwekea Bima ili akifa alipwe bima hiyo yeye. Serikali kupitia Kampuni ya ile Bima ilionekana kwamba, kulipa fidia ile kupitia Bima ile, ile kampuni ingefilisika kabisa, Serikali ikatafuta vyombo vya Kimataifa kufanya utafiti juu ya mauaji yale ili kuinusuru ile kampuni isifilisike; na ni kweli baada ya muda ilibainika kwamba, *Scott and Lad* kutoka Uingereza, Interpol, walikuja Tanzania na kufanya utafiti juu ya mauaji yale, ikabainika kulikuwa na njama. Ilikuwa ni mara ya kwanza kwa Rais wa Awamu ya Kwanza kutoa idhini ya mauaji ya M-Asia yule. Mauaji yale yalifanyika kwa mbinu za hali ya juu. Sasa mauaji ya albino; zaidi ya albino hamsini na tatu katika Taifa hili wamepoteza maisha yao, Serikali inasubiri Mahakama, Mahakama ambayo haina uwezo wa kuendesha shughuli kwa nguvu zile. (*Makofi*)

Tunakuhitaji Waziri Mkuu, utakapotoa hitimisho katika hotuba yako, utueleze kuna mkakati gani wa Serikali wa kuondoa kabisa mauaji ya albino katika Taifa letu. Kuna taarifa zilizopo kwamba, baada ya mauaji yale sasa albino wanapotea katika mazingira yasiyoeleweka, taarifa hizo tunazo na Serikali imenyamaza kimya kabisa juu ya hilo, tunataka Serikali itueleze sasa.

Mheshimiwa Spika, nizungumzie katika eneo la *disabilities* hilo hilo; ni kwamba, hili ni kundi la mahitaji maalum katika Taifa letu; ni watu ambao wanahitaji msaada mkubwa ndani ya jamii na ndani ya Serikali yake. Kundi hili lenye mahitaji maalum limewekwa katika Wizara ya Afya, lakini kundi hili ni kundi mtambuka, kundi ambalo lina mahitaji mengi kama linavyoitwa kwamba, kundi lenye mahitaji maalum; tulitarajia kwamba, kundi hili lingekuwa katika Wizara mtambuka pia. (*Makofi*)

Leo Waziri wa Afya hawezi kutoa hoja kwa Waziri wa Elimu ambaye pia anahusika na walemavu; ni vyema sasa eneo hili la walemavu lihusishwe katika Wizara mtambuka; aidha liwepo katika Ofisi ya Waziri Mkuu, Makamu wa Rais au Wizara yoyote ambayo tayari inaweza kujumuisha maeneo haya yote ambayo mlemavu huyu anatakiwa ahudumiwe.

Mheshimiwa Spika, katika mchango wangu kwenye Hotuba ya Rais alipofungua Bunge, nilizungumzia suala zima la mgawanyo wa rasilimali katika Taifa letu. Mataifa mengi Duniani yameingia katika migogoro mikubwa, yameingia katika vita vya wenyewe kwa wenyewe kwa kutokuwa na mgawanyo rasmi wa rasilimali katika Taifa hilo; hili nililizungumza. La kusikitisha, Serikali imekuwa kiziwi na pofu juu ya hoja hizi. Wabunge wengi hapa wanazungumza; kuna Mikoa kadhaa ambayo tayari inaonekana kwamba, iko nyuma katika maendeleo na siyo leo ni muda mrefu, kila Mbunge ambaye anatoka katika maeneo hayo anazungumzia juu ya hoja hiyo, lakini

Serikali bado imeweka pamba katika masikio yake, haitaki kusikiliza kilio cha Wabunge waliotoka katika Mikoa hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ili tuweze kuijenga amani ambayo inazungumzwa katika Bunge humu, isiwe hoja ya kinafiki kuzungumzia habari ya amani. Amani lazima iwe ya kweli, tutafute vyanzo vya msingi ambavyo vinaweza kuondoa amani yetu, tutafute vyanzo vya msingi ambavyo vinaweza kupelekea kutoka katika amani yetu. Haiwezekani leo Lindi ukawa ni Mkoa wa mwisho katika Bajeti ya Taifa hili. Siyo kwamba, Lindi tunahitaji maendeleo mapya, hapana; Lindi ndiyo ulikuwa Mji msifika, Mkoa msifika, wenye ustawi na maendeleo kabla ya Uhuru wetu; nani hajui hilo? *(Makofi)*

Lindi tulikuwa na mashamba ya Mkonge kumi na sita, wakati ule yaliwekwa na mabepari, leo mnawaita wawekezaji wale. *(Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Spika, leo yako wapi Mashamba ya Mkonge Lindi? Kulikuwa na reli kutoka Nachingwea kwenda Mtwara, Waingereza waliona umuhimu wa uchumi katika Mkoa wa Kusini wakajenga Bandari ya Mtwara, wakajenga Reli ya Nachingwea, leo haipo! Ndani ya utawala wa miaka hamsini wa Chama chetu, tayari Reli hiyo imeng'olewa haipo katika Mikoa ya Kusini; nani hajui hilo?

Ndugu zangu, Lindi kulikuwa na Uwanja wa Ndege wa Kimataifa, labda Wabunge wengine hamjui hilo; ndege ilikuwa inatoka Cairo, Misri *transit* Lindi, Johannesburg, Afrika Kusini kule, ilikuwa Lindi ya miaka hamsini hiyo; iko wapi Lindi yetu leo? (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, tumuulize nani, kuna watu wanakuja wanasema hapa eti miaka hamsini CCM haijafanya kitu; kwa nini watu wa Lindi wasiseme kwamba uchumi wao umedhoofishwa ndani ya miaka hamsini ya Uhuru wa Taifa letu? *(Makofi)*

Tulikuwa hatuna haja na Dar es Salaam, sisi tulikuwa tuna *import* na ku-*export* bidhaa mbalimbali kupitia Bandari ya Lindi. Lindi ilikuwa inang'aa Mji mzima kwa taa za usiku. Mimi katika maisha yangu zaidi ya miaka kumi katika utoto wangu, sikujua kama umeme unakatika, lakini leo kunakuja kauli kwamba, kuna mgao wa umeme; nini mgao wa umeme? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nilikuwa China juzi nikawaeleza kwetu kuna tatizo la umeme, huku mnasemaje? Wakasema sisi zaidi ya miaka ishirini, thelathini, hata nukta moja umeme kwetu haujakatwa; siyo miujiza ni kweli. Kuna haja ya kufanya mjadala wa Kitaifa sasa. *(Makofi)*

Watanzania wana fikra, wana mawazo, tushirikiane sasa katika kuiona Tanzania yetu inakwendaje katika kujiletea maendeleo. Kuna hoja hapa ambayo tayari inazagaa juu ya stakabadhi ghalani; stakabadhi ghalani Waheshimiwa ni taarifa ambayo Serikali inapata upande mmoja; bado Serikali haijahusisha wadau katika hoja nzima ya stakabadhi ghalani mpaka sasa miaka hamsini ya Uhuru, mkulima mpaka anafika katika

meza ya mnunuzi wa bidhaa yake, hajajua bei ya bidhaa yake leo ni bei gani. Miaka hamsini ya Uhuru leo, mkulima anakopesha kilo tano za ufuta analipwa baada ya miezi mitatu kwa bei ya majaliwa; tunampeleka wapi mkulima huyu? (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kuna soko, Wananchi wanaliona lakini wanaambiwa chini ya mtutu wa bunduki kwamba, huruhusiwi kwenda kuuza pale, soko lako ni lile. Kuna haja ya kukaa na wadau, kuna Wabunge wawakilishi wa Wananchi, kuna Wizara ya Kilimo, tukae tujadili mstakabali wa wakulima, siyo kauli ya Kilimo Kwanza ambayo tayari Wananchi bado hawaoni manufaa yake. Huu ni wakati mwafaka sasa Watanzania kukaa kutengeneza mjadala wa Kitaifa juu ya Taifa letu.

Mheshimiwa Spika, nizungumzie suala la ahadi za Rais. Ahadi za Rais siyo kitu cha kukifanyia mchezo; Rais ni mtu mwenye heshima kubwa, Rais anatarajiwa na Wananchi wake, Rais ni Kiongozi ambaye kauli yake ina thamani mbele ya Wananchi tena zaidi ya sheria, kauli ya Rais siyo kitu kidogo. Rais na Marais waliopita, wametoa ahadi kadhaa kwa Wananchi kupitia kampeni za uchaguzi na kupitia ziara mbalimbali, lakini tukiangalia ahadi nyingi bado hazijatekelezwa. (*Makofi*)

Rais ameahidi Soko Kuu la Mkoa, ameahidi mandhari ya Lindi, ameahidi maji katika mtandao wa Lindi na mambo chungu mzima; bado miaka mitatu anamaliza mkataba wake wa Urais, hakuna hata moja ambalo limetekelezwa na Serikali. Kwa nini tuseme Serikali yake inamdharau Rais wao? Kwa nini tusijenge hoja hiyo? Kama ninyi mnamdharau Rais wenu; watu wengine wa kawaida wanafanyaje katika hilo? Rais ameahidi Wananchi wakampa kura nyingi, kulikuwa na wagombea wengi wa Urais lakini walitoa kura zao kwa mujibu wa ahadi ambayo Wananchi walikuwa na matumaini nazo, ahadi za Rais ziko wapi leo? Tumeambiwa hapa kwamba, tutaishughulikia Bandari ya Lindi, nimeangalia katika Bajeti sioni Bandari ya Lindi iko wapi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mwisho, nizungumzie suala la ajira. Majeshi yetu; Polisi na Magereza ni Majeshi ya Kitaifa, yana sura ya Kitaifa, lakini imefikia mahala sasa nafasi hizi zinatolewa kwa wateule wachache; ni watu wachache tu ambao tayari wamekumbatia dhamana hiyo kwa kutoa ajira kwa watu ambao wako karibu nao. Mashaka yangu, tutakuwa na Jeshi la Polisi, tutakuwa na ulinzi, tutakuwa na Majeshi ya Polisi, ambayo tayari yatakuwa na tabaka katika Taifa letu, yatakuwa majeshi ambayo yanatoka katika eneo moja tu la nchi yetu. Nini hatima yake; ni majeshi ambayo yanatoka kwa mujibu wa Kanda. Leo ukiwa *RPC* Lindi, ukiwa *OCD* Mtwara, tayari unaita watu wa kwenu huko kuna nafasi zimetoka njoni nikupeni ajira huku. Hilo lipo, watu wananung’unika, manung’uniko ya Wananchi tusiyalazie damu, Wananchi wananung’uka sasa hivi kila kona wanainung’unikia Serikali yao, wakulima wanainung’unikia Serikali yao, wanafunzi wananung’unika juu ya Serikali yao. Kila kona, tukae tutengeneze mjadala wa kitaifa, tunalinusuru vipi taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mwisho, nisipoteze muda, yangu yalikuwa hayo. Ahsate kwa kunisikiliza. *(Makofi)*

**SPIKA:** Zamani alikuwa anasoma akihutubia, sasa mnamwona mambo yake. Ahsante sana. *(Kicheko/Makofi)*

**MHE. MOSES J. MACHALI:** Ninakushukuru Mheshimiwa Spika, nami kwa kunipa fursa ili niweze kuchangia hoja ya Ofisi ya Waziri Mkuu iliyoko mbele yetu. Kwanza kabisa, ninaomba binafsi nijiondoe ndani ya chupa kama alivyozungumza Mheshimiwa Shellukindo kwamba, dunia nzima na Tanzania nzima inaonekana kujua kwamba, Watanzania tuko ndani ya chupa katika misingi ambayo ameweza kueleza. Mimi siko ndani ya chupa; ninaomba nieleze kwa nini siko ndani ya chupa na hili litajidhihirisha wakati ninaendelea kutoa mchango wangu. *(Makofi)*

Kwa kuwa hatua za kufanya falsafa au filosofi zipo kadhaa; *scholars* mmoja anatuambia kwamba ni kushangaa kwanza *wondering;* pili, ni *questioning* na tatu ni *answering*. Kwa hiyo, lazima kwanza ushangae, halafu pili, utajiuliza maswali na tatu unaweza ukatoa majibu juu ya tukio ambalo mtu umepata kuliona au kulisikia. Leo Tanzania tuna miaka takriban 50 ya Uhuru. Hiyo kengele, ninaomba muda wangu bado ni mwingi sana.

**SPIKA:** Hiyo kengele siyo ya kwako.

**MHE. MOSES J. MACHALI:** Mheshimiwa Spika, Tanzania tuna miaka 50 ya Uhuru. Ninakumbuka wakati ninafanya *economic history of Tanzania* wakati ninasoma Chuo Kikuu, mwalimu wangu aliwahi kuniambia kitu kimoja; wakati tunapata Uhuru mwaka 1961 kama Tanganyika, hali ya uchumi wa Tanzania ilikuwa sawa sawa na nchi fulani fulani kama vile China, ambazo leo hii zinatupiga *gap* kwa kiasi kikubwa sana.

Mwanafalsafa mmoja aliyeishi Karne ya 20 hususan mwaka 1925 mpaka mwaka 1965, alikuwa mpigania haki za watu weusi Nchini Marekani, Malcom Wax, aliwahi kusema, ninaomba nimnukuu: *"History is people's memory and without memory man is demoted to the lowest animal."* Kama historia haiwezi ikatufundisha na sisi tukaishi karne gani, historia ambayo imetuonesha matukio mbalimbali, tulitoka wapi, tukaenda wapi na tumefikia wapi; basi tunaweza tukafananishwa sawa sawa na mnyama mdogo ambaye anaonekana hana thamani katika jamii yetu. *(Makofi)*

Miaka 50 ya Uhuru wa Tanzania, ninaomba niseme kweli kwa upande mmoja nikisema kwamba, Chama cha Mapinduzi hawajafanya chochote, nitakuwa mwongo. Vilevile hicho kitu ambacho Chama cha Mapinduzi wamekuwa wakipigia watu chapuo kwamba, wamefanya vizuri hakilingani na umri wa Taifa la Tanzania la miaka na miaka ya Uhuru. *(Makofi)*

Kwa nini ninasema hivyo? Mwaka 1961 hali yetu ya uchumi ilikuwa *almost the same* na China, leo hii sisi tunaonekana kuwa ni ombaomba kutoka kwa Mataifa mbalimbali ikiwemo Taifa la China. Tatizo ni kwamba, hakuna *accountability* miongoni mwa Wafanyakazi na Watendaji wa Serikali. Ninakumbuka katika Historia ya Taifa la Ujerumani, aliyekuwa *Chancellor* wa Ujerumani katika miaka ya 1870 aliwahi kusema:

*“The great question of the day shall not be solved by speeches and solutions but only by iron and blood.”* Ninarudia tena: *“The great question of the day shall not be solved by speeches and solutions but only by iron and blood.” (Makofi)*

Hiyo ilikuwa ni imani ya Chancellor Auto Von Bismarck mwaka 1870, kabla hajamvamia Mfaransa na alipomvamia yeye aliweza kufanikisha azma yake. Leo Tanzania tunahubiri amani, amani, amani, amani, Tanzania hatuna amani ila tuna utulivu ulioambatana na nidhamu ya woga. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, huwezi ukaja kunishawishi mimi binafsi nikubali kwamba, tuna amani wakati watu kila kukicha wanawaza ni namna gani watapata kamili, umaskini unawatafuna. Miaka 50 ya Uhuru, huwezi kuja kunishawishi kwamba, Watanzania tuna amani, polisi wanaendeleza vitendo vya kuwapiga polisi na kuwakamata watu ovyo ovyo kama vile ni wakimbizi ndani ya nchi yao. *(Makofi)*

Mambo haya yanafanyika, lakini Serikali bado haijaweza kuona ni namna gani ambavyo inaweza ikachukua hatua na Wabunge tukisema wakati mwingine hatuaminiki; Serikali inatoa kauli ya kusema kwamba tuache mamlaka zenye dhamana zifanye kazi zao. Hii ni fedheha kwa Taifa kubwa kwa sababu sisi ndiyo wawakilishi wa Wananchi na tunapokusanyika mahali hapa na kueleza kwamba, Wananchi wetu wanafanyiwa mambo fulani fulani, lakini Serikali inatoa majibu ambayo hayaridhishi; hali hii mnatengeneza bomu lingine, Watanzania watajichukulia hatua mkononi wakati mwingine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Rais Benjamin Mkapa, alikuwa akisema “Mtaji wa maskini ni nguvu zake mwenyewe.” Leo tunashuhudia maeneo mbalimbali watu wanaanza kujichukulia sheria mkononi baada ya Serikali kuwa imewatekeleza. Yanayotokea huko Babati katika Bonde la Kiu ni kiashiria tosha kwamba, sasa Serikali imekaa kimya halafu matokeo yake watu wameanza kujichukulia sheria mkononi, wanatumia nguvu zao wenyewe, wanaienzi kauli aliyokuwa anaitumia Mheshimiwa Rais Benjamin Mkapa. *(Makofi)*

Ninachukua fursa hii kuishauri Serikali kama kweli wanataka amani ya kweli, wajenge tabia ya kusikiliza Wananchi wanataka nini. Kwa sababu hii nchi ni ya Watanzania wote; siyo ya Chama cha Mapinduzi, siyo ya CHADEMA wala siyo ya NCCR, tuna kila sababu ya kusikilizwa tunapoeleza mambo yetu yaweze kusikilizwa sawa sawa. Nimezungumzia suala la kukosekana kwa *accountability* miongoni mwa Watendaji wa Serikali na hili linathibitika na ninaomba niseme kuna vitu vingine vinafanywa kihuni ndani ya Serikali yetu. *(Makofi)*

Nimekuwa nikiuliza hapa mara kwa mara maswali kuhusiana na barabara Mkoani Kigoma. Mwaka jana katika Bajeti zilitengwa zaidi ya shilingi bilioni sita kwa ajili ya ujenzi wa barabara kwa kiwango ya lami kutoka Kidawe kuelekea Kasulu, lakini zile pesa hazijatoka na mpaka leo tunapozungumza hapa, hata katika Bajeti ya mwaka huu ya Wizara ya Ujenzi, hakuna hata shilingi moja ambayo barabara ile imetengewa kwa ajili ya kuendelea na ujenzi ule. Jambo hili ninasema kwamba, kuendelea kuwaahidi

Wananchi na Bunge limekaa limepitisha na hakuna kinachotoka; ni uhuni wa Serikali. Serikali inawafanyia uhuni Wakazi wa Mkoa wa Kigoma. Ninaiomba Serikali wakati mwingine …

**SPIKA:** Mheshimiwa Machali, unaweza ukasema vizuri tu bila kutumia neno la uhuni, tafadhali hebu endelea.

**MHE. MOSES J. MACHALI:** Ninakushukuru Mheshimiwa Spika. Wakati mwingine inaudhi, kwa sababu nimekuwa nikiwakumbusha. Ninaomba ku-*declare* kwamba, mimi ni Mjumbe wa Kamati ya Miundombinu, nimekuwa nikiwaambia mara nyingi na nimemwambia Mheshimiwa Magufuli kuwa, sasa inapofikia hatua kwamba, pesa zimepelekwa kuanzia Nyakanazi, Nyakanazi siyo Kigoma. Watu wa Kigoma tumewakosea nini? Watu wa Kigoma hatulipi kodi? Huu ni utani mnatutania Watu wa Kigoma.

Mheshimiwa Waziri Mkuu, ninaomba ukae na Mawaziri wako; vinginevyo, lugha hii itaendelea kutumika au mnataka Watu wa Kigoma waje watangaze Jamhuri ya Watu wa Kigoma? Kigoma tumewakosea nini? Mheshimiwa Dkt. Amani Walid Kabourou aliwahi kusema, Kigoma basi muitenge kama siyo *part* ya Tanzania. Inakera sana kuona mnatoa ahadi, hata Mheshimiwa Rais aliahidi kwamba, barabara ile itajengwa na mwaka jana pesa zilitengwa leo mmezihamisha; kama siyo uhuni ni nini? *(Makofi)*

Ninaomba tu nizungumze kwamba, hili linakwenda kwa imani.

**SPIKA:** Tusibishane na vitu ambavyo havijengi. Ukieleza vizuri watakusikiliza, lakini ukimwambia mtu mhuni hakusikilizi.

**MHE. MOSES J. MACHALI:** Ninakushukuru Mheshimiwa Spika, lakini hata Mheshimiwa Beatrice Shellukindo, alitumia maneno ya kijinga jinga na alikuwa anatuzungumza sisi Wapinzani. Inaonekana kwamba, sisi Wapinzani tunapotumia maneno ya ukali kidogo wanatudhibiti. Ninaomba kuwe na *checks and balances.* Ninakushukuru, ninaomba niendelee. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Michael Wax pia anasema: "*The medium is the most powerful entity, they have the power to make the innocent guilty and the guilty the innocent.*" Nami ninasema kwamba, *CCM is the honest political party in this State, they have got the power to make the innocent guilty and the guilty the innocent and it follow us. (Makofi)*

Ninaomba niseme kwamba, tumekuwa mara nyingi tunajadili vitu mbalimbali. Ninashangaa baadhi ya Waheshimiwa Wabunge, ambao wamepewa dhamana ya kuishauri na kuisimamia Serikali, wamevua jukumu na dhamana yao ya kuwa Wawakilishi wa Wananchi, wamejifanya nao ni *part* ya *Executives*. Watanzania wanatuona na wanatusikia. *(Makofi)*

Huwezi baadaye mtu unakuja kujulikana kwamba, wewe ni msemaji wa Serikali, mambo hayaendi sawasawa. Tumejadili hapa sisi Wabunge wa Upinzani, tumesema kwamba, kuna hizi posho za Waheshimiwa Wabunge, *Sitting Allowances*, tunalalamika Serikali inakuja na mipango yake kwamba, ina ufinyu wa bajeti haina pesa, watu wanashindwa kujitoa. Waheshimiwa Wabunge, wanashindwa kujitoa kusema kwamba, *sitting allowance* ikatwe ili izibe *gap* la maeneo ambayo Serikali imekosa pesa, watu wanasema kwamba ni siasa! Siyo siasa hivi vitu tunakwenda kwa imani. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, chonde chonde, kama kweli tunawapenda Watanzania na tunakiri kwamba, Serikali haina pesa, kuna tatizo gani hiyo shilingi 70,000 kupelekwa kwenye Bajeti ya Serikali kuchangia Bajeti ya Maendeleo, ambayo inaonekana ni kidogo kuliko hata matumizi mengine. *(Makofi)*

Mwisho wa siku, Watanzania watatuhukumu sisi wenyewe kwa sababu hivi vitu tunafanya na wao wanaona na leo hii uelewa umezidi kukua. Leo insikitisha kwamba, suala la *accountability* miongoni mwa Watendaji wa Serikali limepungua na linazidi kushuka. Serikali inajua, ilikuwa inatosha tu kutumia taarifa za Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Serikali, kuweza kuwashughulikia wale wote ambao wamesababisha Serikali kupoteza pesa nyingi ambazo zingekwenda kusaidia maendeleo ya watu. Nilisema hapa juzi wakati nimeomba mwongozo wa Spika; Mheshimiwa Mbunge wa Jimbo la Mvomero, analalamika kwamba, *DC* ameshindwa kutoa chakula kwa Wananchi wa Mvomero, ambacho kimetolewa na Mheshimiwa Mbunge. Sasa hiyo inaonesha kwamba, uwajibikaji ndani ya Serikali siyo mzuri.

Nikasema kwamba, watu wa namna hiyo kama ingelikuwa ni katika Nchi ya Mashariki ya Mbali, wangelikuwa wamepigwa risasi, wangeshughulikiwa kama kweli tuko *serious*. Hatuwezi kuwa kila siku tunalalamika, tunaimba wimbo ule ule pesa ni kidogo, halafu mtu anaharibu Kasulu, kesho anapelekwa Kibondo, kesho anapelekwa Singida. Hatujengi Taifa, tunazidi kufanya mambo ambayo hayawezi kutusaidia. Malalamiko ni makubwa; leo ninapozungumza Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii kupitia watu ambao wanakagua, wanazungumza nchi nzima kupitia hospitali, wameifunga *theatr*e ya Hospitali ya Wilaya ya Kasulu.

Leo ina maana kama watu wanahitaji kufanyiwa upasuaji na ndiyo walikuwa wanategemea hawana uwezo, Wananchi wetu ni maskini watakwenda wapi? Serikali ilitoa pesa, *theatre* leo imefungwa kwa sababu ya uzembe wa watu wachache. Serikali mnasubiri nini au mnataka mpaka Watu wa Kasulu wajichukulie hatua mkononi ndiyo mtakapoweza kuona kwamba, sasa ngoja mchukue hatua wakati Wananchi walishaathirika kwa kiasi kikubwa. Chonde chonde, ninaiomba Serikali kupitia Ofisi ya Waziri Mkuu, TAMISEMI, wafanye kila linalowezekana, kuhakikisha kwamba, *Theatre* ya Hospitali ya Wilaya ya Kasulu pia inarudi.

Usishangae Daktari wa Wilaya pamoja na Ofisi ya Mkurugenzi, pengine kwa uzembe wao ukakuta wanahamishwa kutoka pale na kupelekwa mahali pengine ilhali maeneo mengine wameharibu. Hivi hatujengi Taifa ila tunazidi kujenga Taifa la watu

ambao hawajali watu wanaopatikana katika nchi yao na ambao ni walipa kodi katika Taifa lao.

Mheshimiwa Spika, ninakumbuka aliyekuwa Spika wa Bunge lililopita, mwaka 2005/2010, Mheshimiwa Samuel Sitta, alialikwa katika Mahafali ya Chuo Kikuu cha Mtakatifu Augustino, ambako wakati huo nilikuwa mwanafunzi, aliwahi kusema: “Watanzania wengi wamekuwa wakiwasifia watu wakiwa ni Watumishi wa Umma na baadaye wanapomaliza utumishi wao, wanapostaafu, wanaonekana kuwa na mali nyingi ambazo zinazidi kipato chao.” Watu wanakuwa wanawapigia makofi na kuwabeza wale waliokuwa waadilifu kama vile Hayati Baba wa Taifa. Hii ni tabia ambayo imekithiri miongoni mwa Watanzania na inawezekana hata miongoni mwetu sisi Waheshimiwa Wabunge, kama mtu pengine anaonesha kuzungumzia mambo ambayo yanaweza kusaidia Taifa, wakamwona mtu huyo hana akili.

Ninaomba nimpongeze Mheshimiwa Samuel Sitta na wote tuishi katika misingi hiyo. Ninakushukuru Mheshimiwa Spika. *Message sent.* *(Makofi)*

**MHE. EZEKIA D. WENJE:** Ninakushukuru sana Mheshimiwa Spika. Ninaomba nianze kwa kuwashukuru Wananchi wa Mwanza, Jimbo la Nyamagana, kwa kura nyingi walizonipa na kuniwezesha mimi mtoto wa mama ntilie pia kuwa Mbunge katika Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninatambua kwa dhati kwamba, mimi siyo Mbunge kwa sababu Wananchi wangu walinipigia kura nyingi, lakini walikuwa tayari kufa kwa ajili ya kulinda haki zao na kuhakikisha kwamba, ninakuja kuwawakilisha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninaomba nimpongeze kwa dhati, Mheshimiwa Freeman Aikaeli Mbowe, Kiongozi wa Upinzani Bungeni, kwa Hotuba nzuri aliyoitoa, iliyojaa uthubutu. *It was indeed a darling speech* na ninampongeza tena kwa kunipa fursa kuwa Msemaji wa Kambi katika Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa. Ninamshukuru sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninaomba niweke *clear* msimamo wa Chama changu na wa Vyama vingine vya Upinzani kuhusu posho halafu ndiyo niendelee. Chama chochote cha Kisiasa Duniani hapa kinatafuta umaarufu ndani ya Bunge na hata nje ya Bunge. Chama chochote Duniani lazima kiangalie vile vitu ambavyo ni *popular* kwa Wananchi na lazima kuji-*identify* na vile vitu ambavyo ni *popular*. Suala la posho kwa Mtanzania wa kawaida, ninaomba nieleweke wazi, posho tunazoongelea sisi hapa na sasa kuna watu wanai-*quote out context* kwamba, *CHADEMA* wanapinga posho. *It is not all that way.* Tunachosema ni *sitting allowance; is very specific* kwamba, *sitting allowance* ndiyo ziondolewe. Hakuna mwalimu Jimboni kwangu Nyamagana ambaye anapata *sitting allowance* na wewe pia ni *civil servant*.

Kwa hiyo, tunachosema na Serikali inalalamika kila siku kwamba, pesa haitoshi. Hata ukiangalia leo *ratio* ya bajeti kwenye *13 trillion, it is only four point something trillion* ndiyo iliyoko kwenye *Development Project. It is almost less than 50% that is*

*pathetic*. Hiki ndicho tunachokisema. Kwa hiyo, ninasema kwamba, kwenye suala la posho, haki ya mama haturudi nyuma, msimamo ni huo huo na tunaomba kama mnaweza, hata kesho mtuletee fomu mbili; moja inayoonesha mahudhurio na nyingine anayetaka kuchukua posho *as from tomorrow.* Hata mkizileta jioni, hatutasaini hiyo ya posho.

Mheshimiwa Spika, ninaomba niendelee. Martin Luther King, aliwahi kusema kwamba, *peace does not win the absence of war, but rather the presence of justice and truth.* Nimesimama leo kama Kijana wa Taifa hili, anayelipenda Taifa lake. Nimesimama leo kama Mtoto wa Mtanzania mnyonge, ambaye analipenda Taifa hili. Nimesimama leo nikiamini kwamba, Tanzania ni nchi ambayo kila mtoto na kila kijana ana uwezo wa kutimiza ndoto yake na ku-*percive* ndoto yake, *provided* umefanya kazi kwa haki na kwa bidii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika hili Taifa, ninaomba tu nitoe takwimu zilizopita na mmoja wa hawa watu ni mimi; hakuna kitu kinachovuruga amani kama *political animosity;* hii ndiyo ilifanya hata Kenya katika uchaguzi wao uliopita wakaingia kwenye machafuko, *political animosity.* Inasikitisha sana kama tunakwenda kwenye uchaguzi, Wananchi wanaongea kwa kutumia *ballot, they speak their will,* tunachaguliwa kwa kura nyingi, hata kutangazwa inakuwa shida halafu mnatuambia kuna amani! Mimi Wenje, Mwanza nilichaguliwa baada ya Wananchi wangu kadhaa kuvunjwa mikono, wengine walivunjika miguu, *tear gas* ilikuwa ni nyingi, ndiyo nikatangazwa kuwa Mbunge; *this is pathetic. (Makofi)*

Mheshimiwa Spika, siyo mimi tu Wenje, nenda hata Arusha, nenda Ubungo, Kawe, Iringa na kote, mpaka mabomu yapigwe ndiyo watu watangazwe; halafu bado kuna watu wanasema kwamba, eti sisi ndiyo hatupendi amani ya nchi hii! *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, yaliyotokea Jimbo la Shinyanga, *we all know;* mtu anashinda halafu anatangazwa mtu mwingine, kwa sababu ya Kaisari mwachie Kaisari. *Electoral Commission is not independent,* wanafanya kazi ya waliowateua; *that is unfair!* Hakuna kitu kinachovuruga amani kama *political animosity.* Hakuna kitu kinachovuruga amani pale ambapo Wananchi haki yao inaporwa na wanaona na Watanzania wanajua wanaofanya hili ni akina nani na wanakuwa wa kwanza ku-*point fingers* kwamba, akina fulani wanataka kuvuga amani, *come on, let's be sincere!* Haiwezekani kuwepo amani kama hii nchi imejaa *innocent thieves and it is true, we have innocent thieves in this country. (Makofi)*

Mheshimiwa Spika, juzi Mheshimiwa Mkuchika, alikuwa anatoa *speech* yake hapa, mimi nilitegemea atakuja hapa kusema kipindi hiki tumefanya vizuri, kuna Halmashauri sijui kama nne pekee ndiyo zimepata Hati Chafu. Nilitegemea pia atakuja hapa na Ripoti atuambie kwamba, hao watu wanne…

**SPIKA:** Mheshimiwa, katika lugha yetu hapa Mawaziri tunawataja kwa vyeo vyeo.

**MHE. EZEKIA D. WENJE:** Mheshimiwa Spika, nilitegemea Waziri wa TAMISEMI, Mheshimiwa George Mkuchika, angekuja hapa na Ripoti atuambie katika hizi Halmashauri nne zilizopata Hati Chafu, Wakurugenzi tumeshawafukuza kazi na wale wote ambao wamepata Hati Yenye Mashaka, hawa tumewaweka kwenye *probation!*

Tunawapa *probation* ya mwaka mmoja, akipata tena Hati Yenye Mashaka kwenye mwaka unaofuata, *let us sack them,* kwani tunaogopa nini? Hii hata ukienda kwenye Mashirika ya Umma, *ATCL is almost dead,* lakini moja ya mambo yaliyochangia kufika hapo ilipo ni *poor management.* Sasa na hawa watu waliofanya hiyo *poor management* hawakufikishwa popote. Hii nchi imejaa matatizo makubwa, halafu unatuambia kuna amani; amani iko wapi kama nchi ipo hivi*? (Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuna matatizo, hatujui *Kagoda Agricultural Limited,* ni nini! Pesa nyingi za umma zilipotea, *almost 40 billion if I am not mistaken, deep green finance.* Leo tuna *issue* ya rada! Hii nchi inaporwa na kila mtu anajua, Dunia inajua, kama alivyosema Lowassa na Watanzania wanajua kwamba, hii nchi inaporwa *and nobody cares!* Halafu mnatuambia kuna amani! Tukienda kuandamana na kuwaeleza Wananchi kwamba, hii nchi inaporwa, eti sisi tunataka kuvuruga amani! Haiendi hivyo! *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya chama changu, kama alivyosema Mheshimiwa Machali, Tanzania hakuna amani. *In fact* ni uvumilivu tu na tunavumilia na nidhamu ya woga. Tukienda hata kwenye uchaguzi kwa mfano, hii nchi tunapigwa mkwala! Unakuta mfanyabiashara akiweka hata picha ya Wenje kwenye gari lake ni tatizo. *In fact,* ninaomba niseme, Wakoloni walikuwa wakali kuliko hii Serikali; waliwanyonga mpaka Waafrika, lakini *the spirit of struggle did not die,* mpaka Uhuru umepatikana. Nami ninachosema, *on behalf of my Party,* hii *spirit* ya *struggle* haitakufa, tuta-*demonstrate,* tuta-*demonstrate,* tutaandamana, kwa sababu Mahatma Gandhi aliwahi kusema, *"Demonstration is the language of unheard."* Maandamano ndiyo lugha ya sauti zisizosikika. Hili la maandamano, ninaomba ieleweke wazi kwamba, tutaandamana na hata kesho tutakwenda kuandamana. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, ninaomba sasa niende kwenye Jimbo langu. Toka nimekuwa Mbunge, kwa hiki kipindi kichache tu, tatizo kubwa kwenye Jimbo langu ni la ardhi. Mwanza ni mji unaokua kwa kasi sana, *almost 11% per annum,* lakini tatizo kubwa ni la ardhi, watu wangu wanaporwa ardhi. Nami nilifikia wakati nikasema kwamba, wazee kama ardhi yenu inakuja kupimwa ovyo ovyo, mimi Mbunge sina taarifa wala Madiwani hawana taarifa, ikiwezekana fukuzeni hawa watu, ikasemekana kwamba, mimi ninachochea maandamano!

Mheshimiwa Spika, kuna watu walizaliwa Mwanza miaka nenda rudi, baba yake na babu yake ndiyo wako pale. Ana watoto na familia, ana ardhi kwa mfano ekari nane, Halmashauri inakwenda kupima halafu yeye anabakiziwa hekta moja, nyingine zote zinachukuliwa, halafu yeye anapewa fidia labda hata shilingi 400,000 kwa kila hekta, halafu yeye kwenye ile ambayo imepimwa anataka kuachiwa anaambiwa atoe shilingi 1,500,000 ndiyo apewe, wakati fidia aliyopewa ni shilingi 400,000; hii haiwezekani!

Mimi sipo tayari kuona mambo kama haya yanaendelea Jimboni kwangu. Ninamwambia Waziri mhusika, kwenye suala la ardhi, hata kama ni ku-*review* Sheria za Ardhi, hizi Sheria siyo Biblia wala Msahafu, zinabadilika. Kwa hiyo, hata kama ni ku-*review* Sheria ya Ardhi ili Wananchi watendewe haki, ninaomba hili lifanyike. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuna suala lingine Jimboni kwangu la maliasili. Sisi Mwanza tunavua samaki, makokoro yanatengenezwa na viwanda na Serikali hiyo hiyo ndiyo inayochukua kodi. Yanatengenezwa makokoro, wavuvi wanakwenda kuvua wanapata samaki, unakuta kuna mama amekwenda *FINCA* akachukua mkopo, anakwenda sokoni kuuza samaki, watu wa Maliasili wanamfuata kule, samaki wanachukuliwa sokoni eti ni wadogo! Kama wameshindwa kuzuwia kuanzia kwenye viwanda hizo neti ndogo zisitengenezwe, neti zikatengenezwa mpaka watu wakanunua wakapeleka huko kwenda kuvua samaki; wakavua samaki, akatoka mwanamke mwingine akaenda kununua samaki akapeleka sokoni, kama wameshindwa kuzuwia huko, hili suala la kufuata samaki sokoni litakuja kuleta fujo kubwa Jimboni kwangu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninaomba Serikali ijitahidi kuzuwia hizo neti zisitengenezwe kuanzia kwenye viwanda, pia iende izuwie kwa wale wavuvi kule, siyo kuja sokoni kuwanyang'anya akinamama ambao yeye hata hayo mambo hayajui; amekwenda sokoni kununua samaki kuja kuuza ili mtoto wake apate chakula. Kwa hiyo, hili pia ni tatizo kubwa kwenye Jimbo langu na ninaomba Serikali ilizingatie.

Mheshimiwa Spika, *issue* nyingine ni kwamba, katika Sekta ya Makazi, Tanzania imebaki huru kama *wall street* na *wall street* kulikuwa hakuna *checks and balances* na ndiyo maana uchumi wa Marekani ulipata shida kwa sababu kulikuwa hakuna *controls* kwenye *wall street.* Leo kwenye *housing industry,* Tanzania hakuna *controls;* mtu anajenga nyumba, yeye ndiyo anafanya tathmini ya nyumba yake na ndiyo anaamua alipishe kodi kiasi gani, na yeye ndiyo anaamua anataka kodi ya miaka mitano au kumi, hakuna Serikali inayoingia kufanya tathmini hata kidogo!

Mheshimiwa Spika, kwa mfano, leo katika maeneo ya Vyuo Vikuu, kuna malalamiko nimeletewa Ofisini kwangu katika Jimbo la Nyamagana, kutoka *Saint Augustine University.* Maeneo yanayozunguka Vyuo Vikuu, yana-*attract* watu wengi sana, siku hizi wanajenga maeneo ya Vyuo Vikuu, kwa sababu *hostels* hazitoshi; hivyo, wanafunzi wapate maeneo ya kupanga. Kodi kwenye maeneo haya, unakuta ni kubwa mno ukilinganisha hata na ile *accommodation allowance,* ambayo mwanafunzi analipwa na Serikali kutoka kwenye Bodi ya Mkopo.

Mheshimiwa Spika, sasa tunaomba ikiwezekana, Serikali iingilie, kama hatuwezi tuka-*control* suala la pango Tanzania nzima, basi tufanye hata *control* maeneo ambapo Vyuo Vikuu vipo. Wale watu wanao-*own hostels* maeneo ya Vyuo Vikuu, tuweke *control* ili angalau pesa wanayoi-*charge* iendane na *accommodation fees* ambazo wanafunzi wanapata kutoka Bodi ya Mikopo.

Waheshimiwa Wabunge, kumbukeni kwamba, hawa watoto wanaosoma, anayekuja kusoma Mwanza wakati mwingine ni mpiga kura wa Mheshimiwa Mkuchika,

lakini amekwenda kusoma Mwanza kwa sababu chuo kipo Mwanza. Kwa hiyo, siyo suala langu tu kama Wenje, siyo suala la Jimbo la Nyamagana, ni suala la Tanzania nzima. Kwa hiyo, ninaomba Serikali kwa dhati, tufanye *controls* kwenye *housing industry;* kama hatuwezi kufanya Tanzania nzima, basi tufanye katika yale maeneo ambayo yanazunguka Vyuo Vikuu.

Mheshimiwa Spika, ni kweli kwa kiasi kikubwa, alivyosema Mheshimiwa Beatrice Shellukindo, hata mimi ninaweza nikakubali kwamba, tuko ndani ya chupa. Tuko ndani ya chupa kwa sababu mambo hayaendi. *(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria muda wa mzungumzaji kwisha)*

**SPIKA:** Ahsante.

**MHE. EZEKIA D. WENJE:** Mheshimiwa Spika, siungi mkono hoja. *(Makofi)*

**MHE. MOHAMMED H. MISSANGA:** Mheshimiwa Spika, ninakushukuru kwa kunipa nafasi. Kwanza, nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu, Subhana Wataallah, kwa kunipa afya, uzima na kuniwezesha kuzungumza au kuchangia mada iliyopo mbele yetu.

Pili, nimpongeze sana Mheshimiwa Waziri Mkuu, kwa Hoja yake nzuri, iliyoandikwa vizuri, lakini pia nimpongeze kwa utumishi wake uliotukukuka kwa muda wote huu ambao amekuwa Kiongozi wetu. Sisi Watu wa Singida, tuna kila sababu ya kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri Mkuu, kwa sababu mara nyingi tunamwendea kwa ushauri, kwa maelekezo, kwa misaada mbalimbali na yeye amefanya hivyo kwa moyo mkunjufu. Tunamshukuru sana Mheshimiwa Waziri Mkuu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninaomba nitumie nafasi hii, kuwashukuru wapiga kura wangu wa Jimbo la Singida Magharibi, kwa kunipa heshima ya kuwa Mbunge wa Kwanza wa Jimbo la Singida Magharibi. Ninawaahidi kwamba, nitawatumikia kwa utumishi uliotukuka, kubwa ninaloliomba; wanipe ushirikiano unaofaa ili tuweze kuleta maendeleo tukizingatia kwamba, maendeleo yataletwa na Wananchi wenyewe na siyo watu wengine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, sikutaka kuzungumzia sana suala la amani ambalo limezungumzwa sana hapa, lakini wazungumzaji wawili, watatu, wa kutoka Vyama vya Upinzani, wananisababisha nizungumze kidogo kuhusu amani. Tumefikia miaka 50 ya Uhuru na kama kuna jambo ambalo tunaweza tukajivunia katika Tanzania hii, katika miaka 50 hii, ni amani na utulivu ulioko hapa nchini.

Huo ndiyo urithi mkubwa tunaoweza kujivunia, hiyo ndiyo rasilimali tuliyoachiwa na Waasisi wetu; Mwalimu Nyerere na wenzake na ndiyo maana tunapata mafanikio. Haya mafanikio ambayo tumeyapata, ambayo wenzetu wanayabeza ni kwa sababu ya rasilimali, ni kwa sababu ya hiyo amani na utulivu, kama siyo hivyo tusingefika hapa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninapomsikia mtu anasema hakuna amani na utulivu, ninataka nimfananishe na Watu wa Nabii Mussa, sisi tunamwita Nabiillah Mussa. Watu wa Nabii Mussa, walikuwa wanapata chakula kutoka juu kinateremka tu, nyama zinaporomoshwa, mikate inaporomoshwa, wanakula bila kuhangaika, Mwenyezi Mungu anawateremshia tu Watu wa Nabii Mussa. Walifika mahali wakamwambia Mussa, yaa Mussa, sasa sitaki niendelee kiarabu chake; ewe Mussa, tumechoka sisi kula mikate hii na nyama hizi, tuombee kwa Mungu wako, atuletee mbegu tupande katika ardhi ili tulime wenyewe.

Mungu hatishiwi nyau, akaipokea hiyo kauli na akasitisha habari ya mikate na nyama ambazo zilikuwa zinaporomoka watu wanakula bila kufanya kazi, bila kuvuja jasho na matokeo yake ndiyo tukaanza hali hii. Hiyo ni kufuru! Walikufuru Watu wa Nabii Mussa na Mwenyezi Mungu akawaonesha, anaweza kulifanya alitakalo bila matatizo yoyote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, wenzetu wanakufuru kwa kusema kwamba, hakuna amani katika nchi hii; hiyo ni kufuru. Mwenyezi Mungu, hatishiwi nyau, anaweza akaporomosha hapa, tukaingia balaa hapa, kama lilivyoingia katika nchi nyingine, sijui akina Somalia, akina Sudan, akina nani na sisi tukawa kama hao! Jamani hiyo ni kufuru, tusimkufuru Mungu, Mungu ana uwezo wa kufanya anavyotaka kufanya, ninawaomba sana.

Tuyaenzi mafanikio haya na rasilimali hii tuliyoachiwa ya amani na utulivu. Kama siyo amani na utulivu, hayo mafanikio ambayo tumeyapata, tusingeyapata. Hao wanaosemasema maneno haya mengi hapa ni mafanikio ya Serikali ya CCM. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tulipopata Uhuru hatukuwa na Chuo Kikuu, baadaye tukapata Chuo Kikuu kimoja, viwili, sasa viko vingapi? Wamesoma wapi hawa? Wamesomeshwa na nani hawa? Wamesomeshwa na nani? Hiyo ndiyo kufuru! Unaweza kumkufuru baba yako ukamwambia hata mimi ningezaliwa ningekuzaa; si ndiyo hawa! *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, tuache mambo ya kufuru tuendelee kuienzi hii amani. Upungufu kwa binadamu ni jambo la kawaida, kama lipo jambo limekosekana, upo upungufu, zipo taratibu za kufuata ukafanikiwa jambo. Mwenzangu mmoja anasema tutaendelea kuandamana!

Mimi ninasema hii ni Serikali ya CCM, CCM siyo legelege na Serikali yake siyo legelege, wote wale ambao wanaonesha dhahiri kama ilivyooneshwa hapa kwamba wataandamana, watafanya fujo, washughulikieni; mnawaacha wa nini? *(Makofi)*

**TAARIFA**

**MHE. EZEKIA D. WENJE:** Mheshimiwa Spika, taarifa.

**SPIKA:** Taarifa.

**MHE. EZEKIA D. WENJE:** Mheshimiwa Spika, ninaomba ieleweke kwamba, kwanza, hatukusema tutafanya fujo, tulisema tutaandamana.

Mheshimiwa Spika, ni kweli nimesomeshwa na Serikali.

**SPIKA:** Ninaomba mumsikilize tu. Ninaomba msikilizeni! Aah, umemaliza?

**MHE. EZEKIA D. WENJE:** Mheshimiwa Spika, taarifa ninayoitoa ni kwamba; ni kweli mimi Wenje, nimesomeshwa na fedha ya Serikali, pesa ya walipa kodi wa Tanzania na ng'ombe wa baba yangu pia walitolewa kodi wakiwemo humo. Kwa hiyo, sijasomeshwa na pesa za CCM.

**MHE. MOHAMMED H. MISSANGA:** Mheshimiwa Spika, ninaikataa katakata, sitaki wala kusikia habari yake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ngoja niendelee.

**SPIKA:** Endelea kujadili.

**MHE. MOHAMMED H. MISSANGA:** Mheshimiwa Spika, ninasema kwamba, ghasia na uvunjifu wa amani unawavuruga vijana wetu. Vijana wetu wamefukuzwa Chuo Kikuu, kwa sababu ya wanasiasa ambao tunakwenda kuwashawishi pale. Vijana hawa hawajapata *Degree,* wanaowashawishi wana *Degree,* wanakula kuku kwa mrija, vijana wetu sasa hivi wanahangaika kule barabarani! Sasa si wanawaonea, wanawaharibia bure! Jamani, chonde chonde, vijana msiwasikilize hawa; wenzenu tayari wameshaukata, wanataka ninyi mkose ili wao waendelee kufaidi! *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hilo la pili, ninaomba nizungumzie habari ya nishati. Nchi ipo gizani, Serikali imeeleza sababu za msingi na tumeendelea kuzikubali, lakini mimi ninadhani pia na sisi wanasiasa tumechangia. Yapo mambo mawili, moja; tumekithirisha sana siasa katika masuala ya uchumi. Tusiingize siasa sana katika masuala ya uchumi.

Kama Wabunge, tunastahili kuzungumzia habari ya uchumi, lakini tusizidishe sana kwa sababu hata chumvi ukiitia sana kwenye mboga, hiyo mboga hailiki. Sukari ukiweka sana kwenye chai, hiyo chai hainyweki. Tuzungumze habari ya uchumi, lakini tusizidishe sana kwa sababu tunavuruga uchumi. Suala la umeme tumeli-*handle* kisiasa, matokeo yake ndiyo tumefika hapa, nchi iko gizani. Ninaomba sana, tuzungumze masuala ya uchumi *constructively,* lakini tusiharibu mambo ya uchumi kwa sababu ya kuingiza siasa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, la pili, nchi ipo gizani, tumepuuza maelezo na ushauri wa wataalamu wetu. Dokta Idris Rashid, alituambia nchi itaingia gizani muda mfupi kuanzia sasa tukampuuza, tukamdharau na tukamkejeli; leo hii nchi ipo gizani sasa nani anayesema ukweli? Pia tulitia siasa na kadhalika na kadhalika. *(Makofi)*

Kwa hiyo, nasema nchi iko gizani. Pamoja na masuala ya msingi ambayo Serikali inachukua hatua, lakini na sisi tumechangia kwa kuzidisha siasa. Lakini vilevile kwa kupuuza ushauri wa wataalam wetu kama Dkt. Elishadai ambaye alituonya kwamba nchi itaingia gizani, tuchukue hatua. Tungechukua hatua kama kurekebisha yale aliyokuwa anataka, tungerekebisha, lakini kama tulivyofanya, ni kudharau na kukebehi ushauri wa kitaalam. Tuwazingatie wataalam na tuwaheshimu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, yako maoni kwamba uchumi unakua katika nchi hii, lakini wale wananchi wenyewe hawaoni na ni kweli wataalam wamesema uchumi unakua katika maeneo ambayo watu wengi hawapo, kwa mfano kama kwenye kilimo, mimi nakubali ni kweli.

Lakini lingine ambalo nataka Serikali waliangalie na mimi sikuliona vizuri katika hotuba za wakubwa hawa ni *population*. Kasi ya *population* ni kubwa mno, uchumi unaweza ukakua lakini haulingani na idadi ya kasi ya watu inavyoongezeka. Ni wajibu wa Serikali kutuelekeza huko. Nashauri elimu itolewe kwa wananchi wetu, athari za kuwa na idadi kubwa sana tunawatengeneza sana watoto kwa kasi kubwa sana. Kwa hiyo, nilitaka niseme kwamba ni kweli kwamba wananchi walio wengi hawajaona hiyo, lakini nadhani kuna mchango wa kasi ya *population* ilivyo na naomba sana Serikali yangu waliangalie hili ili kusudi linaweza likawa ni suluhisho.

Mheshimiwa Spika, narudia kwa kuishukuru Serikali kwa kutupa Wilaya mbili mpya, Wilaya ya Ikungi na Wilaya ya Mkalama. Mwanzoni nilikuwa na wasiwasi kwamba hazikutengewa bajeti, lakini baada ya kuwasiliana na Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Naibu wake, nimepata uhakika kwamba shilingi bilioni 80 zimewekwa kwenye fungu namba 21. Ni matumaini yangu kwamba Mheshimiwa Rais akitoa tangazo la kuanzishwa kwa Wilaya hizi, basi ujenzi wa Wilaya hizi pamoja na Wilaya ya Ikungi na Wilaya ya Mkalama, utafanyika haraka kwa sababu wananchi wanauliza, mlituambia Wilaya mpya ipo, mbona hatuoni? Kwa hiyo, wananchi naomba mfanye subira kidogo, lakini fedha ipo na nina hakika mwaka huu suala hilo la Wilaya mpya litakuwa limeanzishwa.

Mheshimiwa Spika, kimsingi, Singida sisi tunajilisha. Tukipata mvua nzuri, hatuna tatizo. Sisi tunapata mvua mara moja, na tukipata mvua kidogo tuna tatizo. Mwaka huu tumeathirika kwa mvua. Kwa hiyo, hali ya chakula siyo nzuri, nami naomba kueleza hapa kwamba katika mipango ya watu ambao wanahitaji kusaidiwa kwa chakula cha msaada wa njaa ni pamoja na Singida. Namwomba Mheshimiwa Waziri Mkuu na Waziri anayehusika naona yuko pale kwamba atuweke na sisi watu wa Singida katika Mikoa iliyoathirika na njaa, hali zetu siyo nzuri. Maeneo yale ambayo yanalima sana akina Garasoni, Mgungila ya kina Yumbu, yameathirika sana. Kwa hiyo na sisi kwa kweli tutahitaji msaada wa chakula wakati utakapofika.

Lakini vilevile kilimo chetu kimeathiriwa na ndege waharibifu na hili nalisema kila siku. Ndege waharibifu wapo, bahati mbaya sana iko ndege moja tu tena inamikiliwa na nchi tano ndiyo ambayo inatusaidia kuwaangamiza hawa. Unapoitaka Tanzania, sijui

iko wapi! Hivi Serikali ya CCM haiwezi kufika mahali ikanunua ndege yake kwa ajili ya kuangamiza ndege hawa? Ushauri wangu ni kwamba Serikali ifike mahali kama tunavyonunua mashangingi kwa wingi, basi vilevile tuangalie uwezekano wa kununua ndege ya kuangamiza hawa ndege waharibifu, itatusaidia sisi kupata chakula kwa watu wa Mkoa wa Singida.

Mheshimiwa Spika, naishukuru Serikali ya CCM kwa kutupa hospitali ya rufaa lakini yapo matatizo mawili. Kwanza ni upungufu wa Wataalam. Hospitali ya Rufaa yoyote ile ili iwe hospitali ya rufaa inahitajiwa kuwa na madaktari bingwa saba, *not less than seven.* Sasa hatuna hata mmoja. Majengo mawili tayari yameshakamilika, *OPD* tayari, upande kule kwa akinamama tayari. Kwa hiyo, tukipatiwa madaktari bingwa angalau wa kuanzia, wakati lengo likiwa siyo chini ya saba hospitali ile inaweza kuanza kufanya kazi. Hilo tatizo la kwanza la wataalam pamoja na wataalam wengine, lakini hawa madaktari bingwa ni muhimu.

Mheshimiwa Spika, vile vile kuna tatizo la maji. Mji wa Singida unakua haraka, maji hayatoshelezi. Naomba Serikali itusadie kuchimba visima pale katika hospitali ambavyo vinaweza vikakidhi haja ya kutupatia maji.

Mheshimiwa Spika, katika afya, Serikali imetoa maelekezo kwamba wazee na watu ambao hawana uwezo na makundi maalum yapate matibabu bure. Hili halitekelezwi. Hivi kuna kigugumizi gani cha Serikali kutokuchukua hatua ili wazee wetu hawa ambao wamefanya kazi kwa utumishi wa kutukuka wapate matibabu bure? Hili lipo, linaeleweka na kila siku tunalisema hapa, lakini *no action have been taken by the Government why?* Kwanini? Mimi naona kwa kweli Mheshimiwa Waziri Mkuu achukue hatua, wale ambao hawataki kutekeleza sera ya Serikali ya CCM kwamba wazee na makundi maalum akinamama, watoto na nini wapate matibabu bure, wachukuliwe hatua. Hatuwezi kuendelea kuwalea watu, tunawatesa watu wengine. Hilo ndiyo ambalo nasema lishughulikiwe.

Mheshimiwa Spika, kuna barabara ambazo zilipandishwa. Kule kwangu kuna barabara mbili. Moja ni ile ambayo inakwenda Mwakonko kutoka mpaka Mgungila na nyingine iko kwa Mheshimiwa Mchemba. Barabara hizi hazikupata pesa zilizopandishwa. Naomba sana Wizara inayohusika kuzitengea fedha za kutosha mwaka huu ili kusudi barabara hizo zitengenezwe. Hivi karibuni, nilikwenda na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (TAMISEMI) - Mheshimiwa Mkuchika ameiona barabara ile, ameona madhara ya barabara ile, ni barabara ya muhimu. Naomba sana Waziri Magufuli na Wizara yake watenge fedha kwa barabara hiyo na nyingine zile ambazo zilikuwa zimepandishwa daraja.

Mheshimiwa Spika, liko tatizo la watumishi, watendaji wa vijiji na watendaji wa Kata, wachache sana na kwa sababu tumeongeza Kata, wamekuwa wachache zaidi, naomba wale watendaji wa Darasa la Saba na la Nane, ambao ni *trainable material* wawe *trained.* Tunacho chuo pale Hombolo, tuwapeleke hawa tukawafundishe ili warudi waje wafanye hiyo kazi. Kutegemea vijana wa *Form Six* na *Form Four* peke yake hawakai katika mazingira ya vijijini. Kwa sasa utafika wakati watakaa, lakini kwa sasa kwa kweli

huwezi kumpata *Form Six* akakaa kule kijijini. Naomba sana hawa ambao ni *trainable material* wafundishwe ili warudi kule waje watusadie kuendeleza kazi yetu.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja, naomba Serikali ichukue hatua kwa wale ambao hawataki kuenzi amani ya nchi hii. *(Makofi)*

**MHE. RIZIKI O. JUMA:** Mheshimiwa Spika, kwanza naomba nitumie nafasi hii kumshukuru Mwenyezi Mungu ambaye amenijalia leo kuwa hai na mzima na nikawepo katika Bunge hili kuwawakilisha Watanzania.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru wwe kwa kunipa nafasi hii ili nami niwe miongoni mwa wachangiaji wa hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, lakini pia nikupongeze kwa kukalia Kiti hicho ukituwakilisha sisi wanawake, tunajivunia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba nikishukuru Chama changu kwa kunipa imani na kunirudisha tena katika Bunge hili kwa mara ya pili. Naomba Mwenyezi Mungu anipe nguvu na uwezo na nifanye kazi niliyotumwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba nianze mchango wangu kwenye hotuba ya Waziri Mkuu nikizungumzia suala la elimu. Serikali imejitahidi kwa kiasi kikubwa kufanya kazi ya kuboresha masuala ya elimu kwa ujenzi wa Shule za Kata, kwa ujenzi wa Shule mbalimbali, kuongeza idadi ya walimu, na pia kujaribu kuboresha pengine mafao au mishahara ya walimu. Lakini bado tuna changamoto kubwa katika suala la elimu kwa sababu inaonekana pengine labda tulijikwaa mahali hatupajui, basi ni vyema turudi nyuma tuangalie pale tulipojikwaa ni wapi mpaka tukafikia *stage* hii.

Mheshimiwa Spika, elimu ni jambo la msingi. Sote tuliomo humu ndani tumetokana na elimu, na sote tuliomo humu ndani tumetokana na walimu, lakini kinachoendelea sasa hivi walimu kila siku uchao unaonekana tuna upungufu mkubwa wa walimu. Hii inasababishwa na mambo mbalimbali ambayo yanatajwa kila siku na yanazungumzwa na vyombo mbalimbali hata Hakielimu ni watu ambao wanalipigia kelele sana suala hili la kuboresha Sekta ya Elimu.

Mheshimiwa Spika, uhaba wa walimu kwanza unachangiwa na mambo mengi sana. Tunavyopeleka walimu wetu katika mashule mbalimbali hasa vijijini, tunaonekana wengi sana tunakataa kwenda vijijini kufanya kazi ya uzalendo. Lakini kuna sababu za msingi NA changamoto mbalimbali ambazo zinachangia hiyo hali. Serikali inajitahidi kujenga shule, lakini nyumba za walimu bado ni haba mno.

Mheshimiwa Spika, hakuna mwalimu utakayempeleka aende akafundishe katika mazingira ambayo hajui atakwenda kuishi wapi. Hilo ni tatizo, na hayo majengo yanayojengwa, basi lazima tunapofanya tathmini ya kufaulu kwa wanafunzi au kufeli, basi tufanye na tathmini ya yale majengo ambayo yanajengwa kule kwa ajili ya nyumba za walimu. Majengo yanakuwa hayaendani na thamani ya fedha inayotolewa, kwa hiyo, ni jambo la kuzingatia.

Mheshimiwa Spika, tunabadilisha mitaala mara kwa mara. Ninashauri kwamba tunapobadilisha mitaala mara kwa mara ni lazima tuchukue *effort* ya kutoa taaluma au semina za mara kwa mara kwa wale walimu wetu, kwa sababu hata wanafunzi tunawababaisha tunawapowabadilishia mitaala mara kwa mara. Ni jambo ambalo linapelekea pengine kushuka ufaulu wao na kuwababaisha akili zao mara kwa mara, hilo ni jambo moja ambalo linachangia kufeli kwa watoto wetu.

Mheshimiwa Spika, kila siku sisi ni binadamu, tunazaana kwa hiyo, *population* inaendelea kukua. Hivyo, ni lazima *population* inapoendelea kuongezeka na sisi tujipange kulingana na hiyo *population* inayoongezeka katika kila hali. Kwa hiyo, hata katika Sekta ya Elimu nayo ni jambo ambalo lazima tulizingatie kwa kina.

Mheshimiwa Spika, idadi ya wanafunzi ambao wanaandikishwa na idadi ya wanafunzi ambao wanafikia, kwa mfano wanafunzi wanaoingia Sekondari halafu ukiangalia na idadi ya wanafunzi ambao wanafikia Vyuo Vikuu ni ndogo sana kulingana na idadi ya wanafunzi ambao wameingia Sekondari. Hii pengine inachangiwa na kwamba walimu tunaowaajiri hawana kiwango kizuri cha elimu na hii inatokana na kwamba huku chini hakuna msingi. Msingi ambao nimeukusudia ni kwamba *ratio* ya mwalimu na mwanafunzi, mwalimu mmoja sasa hivi tunasema ni wanafunzi 51, lakini zinatofautiana kidogo ukija kwenye taarifa ya hali ya uchumi.

Ukija na kwenye taarifa nyingine zinapingana kidogo. Lakini twende hapo hapo kwamba mwalimu mmoja wanafunzi 51, ni kwamba mwalimu hawezi kufundisha, hatatoa matunda mazuri na tutaendelea kudhalilika kila siku, elimu yetu inaendelea kuja chini badala ya kuboreshwa na ndiyo maana hatuwezi kutoa wanafunzi wazuri wanaofikia Chuo Kikuu. Mtoto ili akue vizuri, tunahitaji tumjenge chini kwenye msingi apate mwalimu ambaye ana kiwango kizuri, ambaye ana hamu ya kufanya kazi yake, tumwezeshe mwalimu, tumpe motisha, tumpe posho, tumpe mshahara mzuri, tumpe mazingira mazuri ya kufanyia kazi yake ipasavyo, vinginevyo tutakuwa tunazalisha Taifa ambalo ufahamu wake ni mdogo.

Mheshimiwa Spika, tukizigawa dakika ambazo mwalimu anafundishia darasani, kwa mfano, Darasa la Nne au la Tano, wanafunzi 51 mwalimu awe na vipindi viwili, kwa mfano awe ana *first and second period*, anafundisha *mathematics*, zigawe hizo dakika 60. Kama kipindi kina dakika 30, zigawe hizo dakika 60 umgawie mwalimu, anaweza kumsaidia mwanafunzi gani ambaye ni dubu? Kwa sababu kuna wanafunzi wengine tunawaita fungu la Mungu.

Mheshimiwa Spika, mpaka umwendee umsogelee umsaidie, umtengee muda yule, kama hatuwezi kumtengea muda yule tutakuwa tunamwacha, anaendelea, anamaliza Darasa la Saba, hana uwezo wowote kwa sababu hakupata huduma ya kutosha kutoka kwa mwalimu wake. Hilo ni tatizo. *Ratio* hiyo haiendani, bado ni mbaya. Tujitahidi angalau tufikie basi wanafunzi 30 mpaka 35. Hatuna budi, lakini vinginevyo tutakuwa tunazalisha Taifa ambalo halina watu wazuri au lenye wataalam. Hilo ni suala ambalo mimi linaniuma, linanikereketa sana kwa sababu hilo la upungufu wa walimu liko Tanzania nzima na linasababishwa na wengine kuacha kazi kutokana na kwamba

wamepelekwa mbali, mwingine anaacha kazi kutokana na kipato anachokiona ni kidogo kwa sababu siyo wote tuna uzalendo. Wengine tuna uzalendo, wengine hatuna. Kwa hiyo, lazima tuliangalie kwa umakini sana suala la walimu.

Mheshimiwa Spika, nikisema hilo nitalisema mpaka kesho, halimaliziki. Nije kwenye suala la afya. Tunazungumzia afya ya mama mjamzito au uzazi salama pamoja na afya ya mtoto au vifo vya watoto. Ukiangalia takwimu, zinaonyesha kwamba bado tunalo tatizo la vifo vya akina mama wakati wa kujifungua. Tukitoa hizo takwimu, mimi nikiwa ni mjamzito, basi najihesabu kwamba pengine huenda na mimi niko katika hilo fungu la wale ambao wametajwa katika asilimia ile ambao wanatarajiwa kupoteza maisha wakati wa kujifungua, napata uchungu, naanza kuvunjika moyo. Hiyo hali ni mbaya. Lakini kubwa zaidi ni kwamba tunapaswa kuajiri wafanyakazi wataalam, madaktari, manesi ambao pamoja na wajibu wao lakini wawe na upendo.

Mheshimiwa Spika, nimeona *issue* moja kwenye *TV* imenisikitisha sana. Kuna mama amejifungua watoto wawili, mmoja ana tatizo la sehemu ya haja kubwa. Kwa bahati mbaya sana yule ambaye amemzaa mzima ndiye Mwenyezi Mungu kamhitaji kamchukua haraka sana. Ni jambo ambalo halizuiliki. Yule ambaye ana tatizo bado amebakia na lile tatizo, anasumbuka, akienda hospitali anaulizwa: "Unazo fedha za kumfanyia *operation* mtoto ili aweze kutengenezwa sehemu ili naye aweze kwenda haja kikawaida?" Yaani, anaaulizwa, unazo fedha? Maskini, mnyonge, hawezi, hana uwezo, sasa hao watoto tunawasaidiaje? Ni mtoto mwenye chini ya umri wa miaka mitano, yaani tangu amezaliwa tunawasaidiaje watoto hawa ambao wako chini ya umri wa miaka mitano? Tunawasaidiaje? Naomba Serikali iangalie sana, bado tatizo la afya lina uzito hasa kwa mama wajawazito na watoto wachanga. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hapa zilitolewa bajaji, tukaambiwa zinapelekwa mahospitalini kwenye Vituo vya Afya ili ziwasaidie akinamama hasa wakati wa kujifungua, yaani waweze kufikishwa haraka hospitali haraka haraka. Mimi nilisema, jamani hii ngumu, haiwezekani! Mama anaumwa uchungu, umtie kwenye bajaji! Lakini tukasema *okay*, Mheshimiwa Waziri akasema ni bajaji ambazo zina muundo wa *ambulance*, sina hakika, sijaziona, lakini hadi sasa kuna hospitali ambazo bajaji zile zimepelekwa, zimeshindwa hata fedha za mafuta za kuweza kuwahudumia wale akinamama, tunawaambiaje akinamama? Akinamama ndio wazalishaji wakubwa, ndiyo walezi wa familia, ndiyo watunza familia, ndiyo wanaolea yatima, ndiyo kila kitu, tunawasaidiaje?

Mheshimiwa Spika, nije kidogo kwenye suala la Muungano kama muda utaniruhusu kidogo tu. Muungano umeshasemwa sana, lakini mimi naomba niseme kwamba nimekuwa Waziri Kivuli wa Muungano miaka mitano iliyopita. Nilisema sana kwa niaba ya Kambi iliyokuwepo. Tuna tatizo dogo ambalo hatujataka kuliona au tunalifumbia macho. Muungano ni mzuri sana, tunaupenda sana, na tunaomba udumu, lakini uwe Muungano ambao utaleta tija kwa pande zote.

Mheshimiwa Spika, kuna mambo ya msingi ambayo yametajwa na Kamati mbalimbali zilizoundwa na Serikali, lakini yamedharauliwa, hayakuchukuliwa hatua

yoyote, wametoa taarifa zao, wametoa mapendekezo yao hayakuchukuliwa tahadhari yoyote. Kuna jambo ambalo linawakera sana Watanzania, sisemi wa Zanzibari peke yao na hata wa Tanganyika wana kero zao, kwa sababu hili ni jambo la pande mbili.

Kwa mfano, akaunti ya pamoja ya fedha ambayo ingepaswa kwa mujibu wa Katiba huchangiwa na Serikali mbili. Hizi Serikali mbili ni zipi? Ni Serikali ya Tanganyika na Serikali ya Zanzibar, ambayo Serikali ya Tanganyika haionekani kuwepo ingawaje mimi nafikiria ipo, lakini haionekani, iko kwenye pazia. Zingepaswa kuchangia na Serikali hizo mbili ili mfuko huo uweze kutumiwa kwa mambo yanayohusiana na Muungano. Sasa ikiwa Serikali ya Tanganyika imo ndani ya Muungano fedha hizi zinatumiwaje?

La pili, ni mengi sana, lakini nitataja baadhi tu ambayo pengine yangetusaidia. Kwanza, ni kukiukwa kwa Mkataba wa asili wa Muungano. Tukirudi kwenye mkataba wa asili wa Muungano, hatuna tatizo. Muungano wetu utakwenda *smooth*, hatuna shida yoyote kwa sababu ule mkataba kama utarudiwa, na siku moja nilipendekeza hapa au niliomba kwa Mheshimiwa Waziri kwamba tuletewe Wabunge, tuna haki ya kuiona mikataba, basi tuletewe Waheshimiwa Wabunge humu ndani mkataba nasi tuuone, tujadili kwa pamoja tuone Muungano wetu unakwendaje kwa maslahi yetu sote kwa manufaa ya Watanzania.

Lakini pia kuna jambo ambalo mpaka leo limeshindikana nalo ni Mahakama ya Katiba. Hii ingetuondolea matatizo. Leo tunakwenda kwenye vikao vya SMT na SMZ ambavyo pengine wahusika wenyewe pengine siyo sahihi, lakini hata Mheshimiwa Rais nampongeza sana kwa kuunda Serikali yake, lakini Wizara ya Afrika Mashariki aliona ina umuhimu wa kuipa Wizara kamili, lakini Muungano wa Serikali yetu kubwa ya Watanzania umepewa kijisehemu kwenye Ofisi ya Makamu wa Rais, yaani ni kama kiidara tu na hata Mheshimiwa Waziri Mkuu naye kasema kidogo na ndiyo inavyokuja kila siku.

Hata katika hotuba ya Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira inasemwa kidogo, lakini sehemu kubwa inakuwa ni mazingira. Huku ni kuudharau Muungano wetu, hatuupi hadhi na heshima.

Mheshimiwa Spika, nakushuru sana, ahsante. *(Makofi)*

**MHE. THUWAYBA IDRISA MUHAMED:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuchangia hoja ya Waziri Mkuu. Lakini kabla ya hapo, natoa shukrani zangu kwa Mwenyezi Mungu kwa kunijaalia nami kupata nafasi hii leo ya kutoa mawazo yangu.

Pili, nakishukuru chama changu kwa kuniteua kuwa mmoja katika Wabunge wa Viti Maalum na juu ya hivyo natoa shukrani zangu kwa Mwenyekiti Prof. Ibrahim Haruna Lipumba pamoja na Mheshimiwa Seif Sharif Hamad ambaye ni Katibu Mkuu na wakati huo huo ni Makamu wa Kwanza wa Rais wa Serikali ya Zanzibar.

Mheshimiwa Spika, kwa kuanzia, nataka kujikita katika elimu. Sote tunaelewa kwamba elimu ni msingi wa maendeleo. Wakati huo huo elimu ndiyo inayoipa dira nchi kuendelea mbele.

Mheshimiwa Spika, sasa utaona kwamba Serikali ya Tanzania imefanya juhudi sana katika kuendesha elimu na kuendeleza elimu na hata maazimio mengi ya elimu wao huwa ni kwanza kuyakubali na kuyapaokea. Hili ni azimio la *UNESCO* ambalo linazungumza kwamba tukifikia mwaka 2015 watoto wote waliofikia umri wa kwenda shule waweze kwenda shule. Hilo wamelipokea vizuri sana na wameliweka katika sera na wamelihamasisha na wananchi wamelipokea na kuwapeleka watoto shuleni. Lakini hebu tujiulize: Je, tumejipanga? Je, tunataka *quality education* au tunataka *quantity*? Ikiwa tunataka *quantity* ni kweli watu wengi wamejitokeza kwa kuwapeleka watoto wao. Lakini ikiwa tunataka *quality* bado inabidi tuwe na hamasa nyingi sana za kuendesha elimu yetu.

Kwa mfano, nitaweza kusema kwamba Serikali haijatilia mkazo katika Shule za Awali. Shule za Awali bado Serikali haijazitilia mkazo, hata ukiangalia katika bajeti, Shule za Awali hazimo. Wanaanza *Standard One* mpaka *University*. Jamani, hebu tuangalie vizuri, Shule za Awali zina umuhimu wake. Ni shule ambazo utaweza kuwapata wanafunzi wenye vipaji na ukawaendeleza vipaji vyao. Unaweza kuwa-*bold* wanafunzi hawa ukawajua kwamba akina nani watakuwa *Ma-engineer, Scientists* na Walimu. Lakini sisi tumezidharau hizi Shule za Awali, hata ukitizama *ratio,* Mwalimu mmoja wanafunzi 71, kweli Mwalimu mmoja ataweza kusomesha wanafunzi 71, tena watoto na kuangalia vipaji vyao?

Halafu utaona kwamba wenzetu nchi za nje wanaziangalia sana hizi kwa sababu wanamchukua mtoto na kumwendeleza mpaka wanafikisha kule anakopaswa kufika, lakini hapa kwetu hili halipo.

Mheshimiwa Spika, mbali ya *ratio* hiyo, tuangalie pia hawa Walimu, wanafundisha kweli? Hawafundishi! Hawana sifa kwa sababu hawajasomea na hii elimu inatakiwa uisomee ili uweze kuwafundisha watoto na kuwatambua. Lakini hawana kitu kama hicho. Tutazame hizi Shule za Ualimu ambazo zinafundisha Walimu hawa, zipo? Hakuna! Sasa ikiwa hakuna vitu kama hivi, bado hatujajipanga. Inabidi sasa hivi sisi tujipange ili tuweze kufikia hiyo *quality education* kama kweli tunataka *quality education* nchi yetu isonge mbele.

Halafu isitoshe, mtoto akishasoma katika Shule za Awali, akija *primary* anakuwa ni mtoto mzuri. Walimu wanakuwa wanawagombania watoto kama wale kwa sababu wanakuwa wameshajengwa kutoka huko chini na wao wanawachukua wanawaendeleza vizuri zaidi. Lakini hilo hakuna. Pia tukitazama, utaona kwamba Mwalimu yule yule akipelekewa mtoto ambaye amesoma *nursery* na akipelekewa mtoto mwingine ambaye hajaanza *nursery* wanawagombea hawa waliotoka *nursery* na hawa wengine hawawataki kwa sababu wanaona kwamba wameshajengwa na wataweza kuwaendeleza katika vile vile vipaji vyao walivyotoka navyo *nursery*.

Hapa sisi wazazi tujitazame. Tunapokuwa na mtoto nyumbani, ukamnunulia gari ukampa, utaona anaikongoloa ile gari. Sisi tunawaambia hapana kufanya hivyo, kwani unaiharibu. Unafikiria pesa yako uliyotumia kununulia, lakini kumbe yule mtoto *talent* yake iko katika ufundi, anataka kujua ile gari imetengenezwa namna gani. Sasa inabidi na Serikali *by itself* iweze kuwasaidia kutafuta Walimu, kujenga Vyuo vya Ualimu na halafu kuwatafuta wakaguzi ambao wataweza kukagua hizi Shule za Awali kwa sababu ni lazima wakaguzi wawe ni watu wenyewe, yaani watu ambao wamesomea lile jambo, siyo Mwalimu wa *Primary* aende akasomeshe Shule ya Awali.

Mheshimiwa Spika, tukitoka hapo, tuje katika sehemu ya msingi kwamba wanafunzi wanaosoma Shule za Msingi, *ratio* yao pia ni kubwa, yaani Mwalimu mmoja kwa Wanafunzi 54. Hiyo ni katika vitabu, lakini *in reality* unampata Mwalimu mmoja wanafunzi 80 darasani. Mwalimu atafundisha vipi wanafunzi 80 wakati mmoja? Mwalimu ataweza kusahihisha madaftari ya wanafunzi ili aweze kujua mwanafunzi huyu kweli kaweza kusoma? Kweli amefahamu? Kwa sababu mwanafunzi anapofundishwa, Mwalimu anataka ampitie mwanafunzi mmoja mmoja, atazame kile alichokifundisha kimefahamika? Ndiyo maana pale Serikali inapokaa au sisi wananchi tunapokaa tukasema kwamba Walimu hawafundishwi, kumbe siyo kosa la Walimu, ni kosa la Serikali kuwaongeza wanafunzi darasani kuwa wengi.

Mheshimiwa Spika, tujiulize, sisi tuliopo humu ndani: Je, tulipokuwa tunasoma, tulikuwa wanafunzi 70 katika darasa? Je, tulipokuwa tunasoma, tulikuwa wanafunzi 51 au 57? Hatukuwa hivyo kwa sababu tumesoma wanafunzi wachache wachache, tukamwelewa Mwalimu alichokuwa anafundisha na tukafaulu, tukafikia hapa, wakati wengine ni Maprofesa lakini uprofesa ule hakuupata hivi hivi, uliupata katika kuwekwa katika hali nzuri, mazingira mazuri ya kufundisha na wewe ukaweza kuwa katika hali hiyo.

Sasa tukimchukua huyu Mwalimu tunamwonea bure, tutazame mazingira anayofundishia, wanafunzi wanakaa chini, Mwalimu hana meza, akishafundisha itabidi na yeye akae chini awatazame wanafunzi. Sasa hapa utakuwa humjui nani ni mwanafunzi na nani Mwalimu kwa sababu wote wawili mnagaragara chini katika kufundishana.

Ni vyema sasa hili darasa la wanafunzi 80 au 50 tukalipunguza. Kama hatuna maeneo, basi tuwaweke Walimu wawili kwa kila darasa ili mmoja awe anafundisha na mwingine awe anatazama wanafunzi namna wanavyoendelea na masomo yao. Isitoshe, hapo tumtazame huyu Mwalimu anafundisha madarasa mangapi kwa siku. Hayapungui madarasa matano kwa sababu wakati mwingine anatakiwa afundishe vipindi 30 au 25 kwa wiki. Vitabu anavyokuwa navyo kwa darasa moja wanafunzi 50, madarasa matano madaftari 250 na somo moja pengine, kama ana masomo matatu ana madaftari mangapi? Ndiyo pale utakapomwona mwalimu kwamba hashughuliki kufanya *marking* kwa sababu hana muda. Sasa inabidi tubadilike ili tuwawekee mazingira mazuri walimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia mitaala inayofundishwa iwe ni mitaala ambayo itawezesha, wakimaliza Darasa la Saba au Darasa la Kumi na Mbili au *University* waweze kufanya kazi, lakini siyo mitaalam hivi hivi tu kila siku. Tubadilike kwa kufanya

mapinduzi tuwe na mitaala ambayo tutaiwekea biashara, mambo ya kilimo, tuwe na mitaala ambayo tutaweza kuweka vitu tutakavyowasaidia.

Pia katika Sekta ya Afya, kwa sababu muda unakaribia kwisha, nije katika suala la maradhi. Hakuna maradhi ambayo ni mazuri. Maradhi yote ni mabaya, lakini kwa kuzidiana. Kuna maradhi ya Kansa ambayo yanawaathiri sana wanavijiji wetu na wananchi wetu. Sasa maradhi ya Kansa jamani matibabu yake ni ghali. Nimezungumza na mtu ambaye ana maradhi haya anasema kwamba unapokwenda kutafuta dawa ya *aspiration* inauzwa shilingi 20,000/=. Ukitaka kutolewa *lumb* ni Sh. 40,000/=, ukitaka kufanyiwa *surgery* ya mwanzo ni Sh. 150,000/=, ukitaka kuwekewa *calcium* katika dawa yako ni Sh. 120,000/=, sindano moja ni Sh. 14,000/= na unataka upigwe sindano mbili kwa siku, jumla yake ni Sh. 28,000/=.

Mheshimiwa Spika, kuna dawa nyingine wanasema hapa hakuna mpaka ukatafute nchi za nje ambayo moja inafika hata Sh. 200,000/=. Je, tunawasaidiaje watu hawa? Haya maradhi yanawaathiri, maana ni bora siku hizi uumwe UKIMWI kuliko Kansa kwa sababu UKIMWI unapata dawa, lakini Kansa hakuna dawa. Dawa ni ghali, ukienda *Ocean Road* wamejaa tena unaona imani, watoto wadogo, vijana, watu wazima wote wanaathirika na maradhi haya.

Jamani Serikali awasaidie hawa watu wa chini. Nchi za nje hutoa dawa bure kwa maradhi sugu, kwa hiyo, na sisi tufanye kila njia tuwape dawa bure wagonjwa ili tuweze kuwasaidia na angalau wapate nafuu, wahisi kwamba na sisi tupo katika jamii ya Kitanzania na wao wanatufikiria na wanatusaidia. La sivyo, tutakuwa kila siku tunawaweka mahali pabaya. Maana *psychologically* wameshakuwa *affected* kwa sababu nikishakuwa na maradhi haya, basi maisha yangu yameshapotea. Lakini tujaribu kuwasaidia na katika kuwasaidia ni kuwatafutia dawa tukawapa bure ili waweze kujiendeleza kimaisha.

Mheshimiwa Spika, nilisahau kitu kimoja katika shule, nacho ni Wakaguzi. Nimeangalia Wakaguzi, inaonyesha sekta hii ina Wakaguzi kidogo mno, kwa sababu haiwezekani shule ambazo wanataka kuzikagua wenyewe wamepanga shule 20,094, lakini zilizokaguliwa ni shule 9,960.

Mheshimiwa Spika, naomba sekta hii ipewe umuhimu.

**MWENYEKITI:** Ahsante.

**SPIKA:** Anayefuata ni Mheshimiwa Rukia Kassim Ahmed, maana ninyi mmejipanga.

**MHE. RUDIA KASSIM AHMED:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuchangia katika hotuba hii ya Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Spika, napenda nikipongeze chama changu kwa kuniteua mimi kuwa ni mmoja kati ya Wabunge wa Viti Maalum kupitia Chama changu cha *CUF* na pia

napenda kuwapongeza wajumbe wote wa Mkutano Mkuu wa Wilaya ya Chakechake kwa kunichagua mimi kwa kura nyingi sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, napenda pia nikupongeze wewe kama mwanamke wenzetu kwa kupata nafasi hii adhimu ya Uspika na hii inaonyesha wazi kwamba wanawake tunaweza na inatuthibitishia kwamba kumbe wanawake tunaweza, hata tukichagua Rais mwanamke na tunategemea baada ya muda mfupi akina mama tutajipanga kugombea nafasi hiyo.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, nataka niende katika kuchangia hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu. Nataka nijikite kidogo katika suala la ajali za barabarani. Niliona katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, alisema kwamba ajali za barabarani zinachangiwa na ulevi. Ikiwa hili Serikali kweli imeliona kama ajali kwa kiasi fulani zinachangiwa na ulevi wa madereva, hivi tujiulize, kwa nini pale Ubungo pana baa nyingi sana na bado Serikali inaacha zikiendelea?

Mheshimiwa Spika, hatuwezi kuwazuia watu wasistarehe wakanywa pombe kama wanavyopenda, lakini pia ipo haja ya kuelimisha umma kuwa wakati wa kazi, basi wasinywe pombe, wafanye kazi.

Mheshimiwa Spika, mamia ya Watanzania wanateketea, watu wanakufa, tunaongeza idadi ya walemavu wakati tukijua kama pale pana baa, madereva wanalewa kwanza ndiyo wanaendesha mabasi kwenda mikoani. Tuna jukumu kubwa mbele ya Mungu kwa sababu sisi ni viongozi, hili jambo tunaliona na tunalifumbia macho.

Mheshimiwa Spika, nawashawishi Wabunge wenzangu kwamba tuishawishi Serikali ikubali kufunga baa zilizopo Ubungo.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, nataka nijielekeze kidogo katika Jiji la Dar es Salaam. Inavyoonekana kwa dhahiri, hakuna *town planners,* yaani wapangaji wa miji katika Jiji la Dar es Salaam na kama wapo, basi inaonekana dhahiri hakuna ushirikiano mzuri kati yao na Halmashauri ya Jiji na wananchi kwa sababu katika utafiti niliouona, kuna baadhi ya majengo yamejengwa, watu wanapewa vibali vya kujenga, lakini watendaji wa Jiji inaonekana hawajui kazi zao kwa sababu, iweje mtu apewe kibali cha kujenga mpaka anafikia ghorofa sita au saba ndiyo anakuja kupigwa *stop*, anaambiwa wewe umezidi umekiuka, maana umekaribia barabara na mambo kama hayo. Hao watendaji walikuwa wapi? Hii ni dhahiri kwamba hakuna ushirikiano au ni rushwa huwa inatembea mpaka inakuja kuonekana mambo yameshafikia katika *stage* kubwa.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, nataka nijielekeze katika jiji hilo hilo kwa sababu linaonekana lina matatizo makubwa na sisi wenyewe hatujayaona. Katika Jiji la Dar es Salaam mikokoteni imezidi mno. Sijawahi kuona jiji lolote ulimwenguni katika miji niliyofika mikokoteni mingi kama Jiji la Dar es Salaam.

Mikokoteni hii inahalalishwa na watu wa Halmashauri ya Jiji, kwa sababu iweje pembezoni mwa barabara utakuta watu wana mikokoteni wanafanya biashara na watu wa

Halmashauri ya Jiji wanawatoza kodi? Ina maana wanahalalisha wale watu wafanye kazi maeneo hayo. Hii inasababisha foleni kuzidi katika Jiji hili, gari zinashindwa kupita kwa mikokoteni ilivyozidi, mikokoteni mingine inachuna magari na jeuri tele, ukiwaambia wanavyokutolea maneno huwezi kuamini. Lakini hii inasababishwa na watendaji wa Jiji. Mimi naishauri Serikali, hawa wenye mikokoteni wanaofanya biashara ya mikokoteni, basi wawapangie sehemu maalumu za kufanya biashara.

Mheshimiwa Spika, Jiji hili la Dar es Salaam ni uchafu mno na linanuka. Utakuta takataka zimesambaa hovyo, ile kampuni inayoshughulika na uzoaji wa taka inaonekana hawajui kazi zao kwa sababu hakuna ma-*dustbin*, hakuna vizimba vya kuwekea taka, wanaopita kuchukua taka wanachelewa mpaka wakienda taka zimeshaoza, ukiangalia mitaro ya maji machafu inaziba ikinyesha mvua, mifuniko ya mitaro ya maji machafu inaibiwa watu wanakwenda kuuza chuma chakavu. Kwa nini basi watendaji wa Jiji hawatafuti *means* nyingine ili kusaidia tatizo hili?

Hebu tumwangalie Mheshimiwa John P. Magufuli na timu yake baada ya kuona mabango ya barabarani yanaibiwa, watu wanakwenda kutengeneza Maseredani pamoja na majiko ya kupikia, basi Mheshimiwa Magufuli katengeneze alama za barabarani kwa kutumia zege na Saruji. Mimi nilikwenda Shinyanga kutembea, niliziona hizo alama za barabarani na watu hawaibi tena, wataiba vipi? Sasa na wao wawe wabunifu watengeneze kwa kutumia saruji na nondo kufunika ile mitaro, kwani ni hatari. Wanaotembea kwa miguu wanaweza wakatumbukia, ni hatari kwani watoto wadogo wanaweza wakapoteza maisha yao na pia ni aibu katika Jiji kama lile.

Mheshimiwa Spika, mambo madogo madogo kama haya ya kuweka mji katika hali ya usafi, hivi jamani tunasubiri tupate mshauri mwelekezi atuelekeze kufanya hili? TV tunazo, redio tunazo, wao wanakwenda zaidi kwenye mambo ya anasa, michezo ya kuigiza na visura, wanaonesha visura lakini hawatoi taaluma kwa watu wetu namna ya kuuweka mji katika hali ya usafi. Naomba sana Serikali hili ilione *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia twende katika barabara. Barabara za Dar es Salaam ni chafu mno, ni mbovu. Ikinyesha mvua, ni mashimo matupu. Pale Burugurni Rozana, nilipita nikaona handaki kama mwaka mmoja nyuma, utafikiri labda tuko katika vita vya Idd Amini siku zile. Handaki kubwa, gari zinapita pembeni zinashindwa kupita pale, foleni inazidi. Hivi kweli jamani hawa watendaji wa jiji wanashindwa hata kufukia mashimo? Au pia wasubiri wapate mshauri mwelekezi katika hili? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ukija hapa Bungoni, barabara mashimo matupu utafikiria bao la soo. Hivi kweli jamani niwaambieni wao hawaioni ile hali? Shule ya Uhuru, Msimbazi mashimo matupu, aibu katika mji kama huu, mji mkubwa, mji unakuja wageni, hivi hata kufukia yale mashimo tunasubiri tupate mshauri mwelekezi? Jamani naishauri Serikali hawa watendaji wa jiji waitwe na waelekezwe wajue wajibu wao. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, kuhusu *packing* za Dar es Salaam, hakuna sehemu maalum ya kuegesha magari. Magari yanaegeshwa pembezoni mwa barabara, gari zinashindwa kupishana mbili, wanasababisha foleni, wanazidisha, wanasababisha ajali na halafu watu wa Halmashauri ya jiji wanachangia kulihalalisha hili, kwa sababu wale ukiweka tu gari,

tayari wameshakuona. Watu wa jiji wanakuja wanakupa kiristi eti ulipie kodi, ina maana wana kuhalalisha wewe uweke gari pale ili uzidishe msongamano. Sasa nahoji, wao pesa wanazozikusanya zinakwenda wapi hata wakashindwa kutengeneza *packing*?

Mheshimiwa Spika, ukiiweka gari, hata uiweke juu ya kichwa cha mtu, basi watakuja kukupa risiti, watakwambia ulipe, wanaiona haraka mno. Sasa nashauri Serikali, jamani, hawa watendaji wa jiji, waitwe waelekezwe namna ya kuliendesha jiji katika hali nzuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, nitakuwa mchache wa fadhila kama sitawashukuru au kuwatakia Madiwani maslahi mazuri, kwa sababu watu wanasema aisifuye mvua imemnyea. Kwa sababu mie nilikuwa Diwani, nayajua vizuri majukumu ya Madiwani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nayajua majukumu ya Madiwani, wana kazi nzito sana, Madiwani wana majukumu makubwa. Kwa hiyo, naiomba Serikali na nawaomba Wabunge wenzangu tushirikiane katika hili, tuwatetee walipwe mishahara. Kuna baadhi ya Wabunge humu walikuwa ni Madiwani, inaonekana wenzangu wamejisahau kule walikokuwa au yawezekana wenzangu wamepitiwa na hilo, lakini nawaomba kila aliyekuwa Diwani ambaye kaingia katika mjengo huu tushirikiane kuwashawishi Wabunge wenzetu ili Serikali iwalipe mishahara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, nataka niendelee kwenye kero za jiji la Dar es Salaam. Katika jiji la Dar es Salaam huduma za kiafya katika mashule hazitoshelezi. Kwa mujibu wa Serikali, lengo la Taifa walisema, kama kutakuwa na mpango wa kutengeneza choo kimoja cha shimo kwa ajili ya watoto wasichana 20 na choo kimoja cha shimo kwa ajili ya wavulana 25. Lengo hili linaonekana liko mbali sana kufikiwa, kwa sababu sasa hivi kuna uwiano wa choo kimoja cha shimo kutumiwa na wanafunzi 90.

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa utafiti uliofanywa katika shule 40, inaonekana shule 11 tu ndiyo kidogo ziko afadhali na hizo zina uwiano wa kutumia choo kimoja watoto 47. Katika shule hizo 11, inaonekana ni shule sita tu ndizo zilizojitosheleza katika huduma ya afya. Kwa mfano, Gerezani, Buguruni Viziwi, *Oysterbay*, Mnazi Mmoja na Amana. Kwa hiyo, nilikwenda katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri kama kuna mpango wa kuongeza kutengeneza vyoo katika mashule. Nashauri hili lipewe *priority* katika mji wa Dar es Salaam kwa sababu watoto wakipata haja wanakwenda nje na kwenye kuta. Ukipita katika mashule ni aibu. Harufu mpaka njiani. Jamani mtu aisitiri ile aibu yake, lile jiji ni kubwa, wageni ni wengi, tujitahidini jiji hili liwe katika hali nzuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo naomba kukaa. *(Makofi)*

**MHE. CLARA D. MWATUKA:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi hii ili nami niweze kuchangia hotuba hii ya Waziri Mkuu. Awali ya yote, naomba nimshukuru Mwenyezi Mungu, ambaye amenijalia kufika siku hii ya leo na kunipatia

nafasi ya kuweza kusimama hapa. Pia kwa sababu ni mara yangu ya kwanza kusimama hapa, napenda nitoe shukrani zangu kwa uongozi wangu wa Chama, nikianzia na Mwenyekiti wa Taifa, Katibu Mkuu na Kamati yake yote. Hawa ndio walionifikisha hapa, kwani niligombea Jimbo na nilikuwa na matumanini kwamba ningepata safari hii, lakini kwa bahati mbaya inajulikana, nikatemwa, lakini Chama kikanionea huruma kikanipa nafasi hii. Kwa hiyo, sina budi niwashukuru hawa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nitakuwa nazungumza machache kwa kila sehemu kwa sababu mengi yamezungumzwa na waliotangulia ila kwa kuwa tunaachana kutokana na maeneo, mengine nitakuwa naongezea.

Mheshimiwa Spika, nikianza na Iidara ya Elimu, tumekuwa na tatizo lile la kusema kwamba kulikuwa na matokeo mabaya katika mitihani kwanza ya Darasa la Saba (VII) kwenda Kidato cha Kwanza, na wa Kidato cha Nne. Kwa kweli matokeo haya yamestahili kutokana na jinsi tunavyowaweka. Elimu hivi sasa ipo, lakini kidogo utaratibu unakuwa unaendeshwa kwa kusuasua, kivipi? Lile lililosemwa na wenzangu kwamba mitaala inabadilishwa mara kwa mara, hivi sasa utakuta kwamba wanafunzi wa Darasa la Saba wanaweza kuanzia tangu mwezi wa tatu au wa nne, wanawekwa makambini, wanaandaliwa kwa ajili ya mitihani, wakati huo huo walimu wanaokwenda kufundisha kule wana vipindi katika madarasa ya chini haya, la tatu mpaka la sita.

Sasa vipindi vile vingine ni vya kupokezana tu, sasa utaratibu unaoendelea pale unakuwa kidogo haukamiliki kutokana na mapungufu ya walimu wale maana inawezekana masomo mengine yalikuwa na walimu maalum ambao wana vipaji na masomo yale. Sasa wanapotoka wale wakaenda kule kwenye makambi, huku nyuma tunashikiana tu, wewe shika darasa hili, wewe kashike darasa lile sasa pale kidogo ndiyo panatupelekea kupata matokeo mabaya.

Mheshimiwa Spika, tukienda kwenye Kidato cha Nne, sehemu nyingi hasa kutokana na shule hizi za Kata, walimu wanakuwa wachache na shule nyingine tangu zilijengwa zikafunguliwa zimekuwa hazina walimu wa kutosha. Nikichukulia mfano, shule ya kijijini kwangu Nanganga, ilianza ikiwa na walimu watatu, wanne, kutoka hapo wengine wakaenda kusoma akabaki mmoja ambaye ameshika nafasi ya utawala na wa pili huyu ndiye pekee sasa wa kufundisha. Madarasa manne atakwendaje peke yake, afundishe darasa gani aache darasa gani, kwa masomo yapi?

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, pale kwa vyovyote vile huwezi kumpata mwanafunzi ambaye anaweza akafaulu mtihani kwa sababu masomo mengi hakuyasoma. Hivyo, hili limechangia sana kuwafanya wanafunzi washindwe kwa sababu Baraza la Mitihani linapotunga mitihani halichagui kwamba kuna shule ambayo wanafunzi hawakusoma baadhi ya masomo katika baadhi ya madarasa, wote mtihani ni ule ule, uwe umesoma, hukusoma kazi kwako.

Mheshimiwa Spika, pamoja na hayo, kumekuwa na michango mingi ambayo ni ya msingi, lakini sasa kulingana na hali duni ya maisha, wazazi wanashindwa kupata michango ile. Kinachoendelea pale ni walimu kuwarudisha watoto wale nyumbani mpaka

pale wazazi wao watakapotoa pesa kwa ajili ya michango ile. Sasa angalia mwanafunzi anakosa masomo kwa kipindi hiki, mzazi hajui lini senti itapatikana ili aweze kupata vifaa vile vinavyotakiwa, sasa mtoto huyu anapokwenda atakuta wenzake wako mbele na mwingine anashindwa kabisa kwa sababu baba yake hawezi kupata tena. Mwenyewe maisha yake yako hohe hahe, hana kwa kupata, anashindwa na hivyo mtoto anaacha masomo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naiomba Serikali iliangalie sana hili, itambue kwamba kuna hao wanashindwa kabisa na wengine ni wale wenye mazingira magumu ambao hawana wazazi wa kuwalipia ada. Nakumbuka zamani katika Halmashauri kulikuwa kunapatikana msaada wa kuweza kuwasomesha hawa ambao wapo kwenye mazingira magumu. Lakini hivi sasa kulingana na Halmashauri zetu kukosa pesa, nao wanashindwa kufanya vile. Hivyo, watoto hao wanabaki wanazagaa mitaani.

Mheshimiwa Spika, pamoja na hilo, kuna Padre Mmisionari mmoja pale katika kijiji cha Nangoo, kuna shule moja ambayo ni ya Nanganga kilomita kama tatu au nne hivi kutoka Nangoo kwenda Nanganga. Wanafunzi wanatoka pale kila siku, wanategemea usafiri, walio na baiskeli, sawa wanakwenda kwa baiskeli, wanaotegemea usafiri wa mabasi wakati mwingine wanachelewa wanafika shuleni vipindi viwili vimepita. Sasa Padre huyu akawaonea huruma, akaamua kuwajengea shule pale Nangoo ambayo imekamilika. Mwenyewe nimekuwa shahidi, nilikabidhiwa kwamba shule hii imemalizika anatukabidhi pamoja na nyumba za walimu mbili zimejengwa, akaomba kwamba wanafunzi wale wanaochelewa masomo waende kule. Sasa hii shule hapa ifunguliwe wale wanafunzi warudi wasome hapa katika jengo hili. Ni jengo zuri tu, wakaguzi wa elimu wamekwenda pale wameliangalia limekamilika, kilichobaki ni kupelekwa walimu tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa naiomba Serikali ili tusimvunje moyo Mmisionari huyu mwenye huruma kwa watoto wetu, tuwapeleke walimu pale wakafungue shule hii ili kutimiza azma yake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, zaidi ya hayo, nahamia sasa kwenye Wizara ya Afya. Kwa masikitiko makubwa, Wizara ya Afya sijui niiweke katika hatua gani! Kwanza naisikitikia yenyewe kwamba uwezo wa kupata wahudumu mahospitalini mwetu ni mdogo, kila hospitali ukienda wahudumu ni wachache.

Mheshimiwa Spika, nyumba za waganga pale ni shida, wanakaa kwenye majumba ya watu binafsi. Sasa hali kama hii inapelekea huduma vile vile kutokwenda vizuri. Naomba Serikali iliangalie hilo. Pamoja na hilo, hospitali kwenyewe ukienda kwanza utauziwa cheti au pengine uchukue karatasi wewe mwenyewe, huduma utakayoipata pale ni daktari kukuhoji ugonjwa wako na kukuandikia madawa. Kitakachoendelea pale, nenda dukani kwa fulani ukapate dawa hizo. Nasikitika kuona kwamba hospitalini pale, popote sijui kama hospitali nyingine wenzetu wanakuwa na utaratibu gani, lakini naamini kwamba kila hospitali pesa zinahitajika, hakuna dawa za bure. Sasa pesa hizi zinafanyiwa nini kiasi kwamba haziwezi kununuliwa dawa ili ziwepo pale hospitalini? Kwanini wanataja na wengine wanadiriki kabisa kusema nenda dukani kwa fulani? Huko kwa

fulani kwanini anatambua kwamba kuna kwa fulani? Ina maana huko kuna mpango unaofanyika?

Mheshimiwa Spika, naiomba sana Serikali iliangalie hilo na pengine kwa sababu hata wafanyakazi wenyewe mshahara ni mdogo, hali ukifahamu kwamba mpishi anashiba jikoni na hawa wanaweza kujisaidia kwa sababu mshahara ni mdogo. Hivyo watazamwe pia kwa upande wa maslahi.

Mheshimiwa Spika, vile vile kuna wahudumu wengine ambao walipata mafunzo yao miaka mingi iliyopita, mpaka leo bado muda wa kustaafu upo, wanaendelea. Sasa hawapelekwi kwenda kupata masomo. Mambo ya siku hizi madawa mengi mapya yanaletwa, lakini hawa wapo na elimu ile ile ya mwanzo. Sasa hawa bila kupelekwa kwenye misasa wanaweza wakatoa madawa ambayo wanaweza kuhatarisha maisha ya wagonjwa, hivyo watazamwe.

Mheshimiwa Spika, kuna hospitali ya Ndanda ambayo ni ya misheni. Hospitalii hii ni tegemeo kubwa katika Wilaya ya Masasi. Wahudumu pale vile vile kama ilivyo Serikalini ni wachache. Sasa ningeomba Serikali kwamba angalau baadhi ya wahudumu hawa wachache wa Serikali wawe wanapelekwa pale wakasaidie kazi, walipwe na Serikali kwa sababu pale ndipo huduma ya afya inapotegemewa na ukienda kutibiwa pale na dawa unapata, kuliko ilivyo kwa hospitali zetu za Serikali.

Mheshimiwa Spika, vile vile mwaka 2003 hadi 2004 ulizuka ugonjwa wa kipindupindu katika Tarafa hiyo ya Chikundi kuanzia Ndanda yenyewe, Nangoo na Nkwera pakajengwa na makambi ya wagonjwa wa kipindupindu. Wahudumu wa Serikali walikuwa wachache, wakaazimwa na wa pale Ndanda 13 wakashughulika kwenye makambi yale.

Mheshimiwa Spika, ninasikitika kueleza kwamba malipo walikuja kupata wale watumishi wa Serikalini tu, wale wa hospitali ile ya misheni walipata kwanza shilingi hamsini hamsini tu na nyingine wakaambiwa watalipwa baadaye. Wamedai mpaka wakafika kwa Mheshimiwa Dkt. Mary Nagu akiwa Waziri wa Afya wakati ule na yeye akatoa tamko kwamba Mkuu wao aandike barua wapate malipo yao, lakini mpaka leo bado. Hivyo, Serikali iwatazame hawa, isije ikawavunja moyo kwa sababu ndiko tunakotegemea.

Mheshimiwa Spika, niende sasa kwenye hospitali mama ya Wilaya. Nasikitika kukueleza kwamba hospitali hii kwa kweli inatia huruma. Huduma pale ni ndogo.

**SPIKA:** Inaitwaje?

**MHE. CLARA D. MWATUKA:** Mheshimiwa Spika, inaitwa Nkomaindo. Hata leo, toka juzi, jana napigiwa simu na watu kwamba jamani zungumzeni huko Bungeni, maji ni shida hasa kwenye kliniki ile ya wazazi ambako kunahitajika maji. Ukienda, unaambiwa kwamba madumu yamejaa, kwa sababu maji yanatoka majumbani. Pale

hospitalini pana kisima, lakini hakina hata tone la maji. Tunafanyaje sasa? Hapa kipindupindu kikija, wa kushughulikia ni sisi. Sasa ni hasara kwa Serikali. Naiomba Serikali pale tatizo la maji tumelipigia kelele toka siku nyingi, nimepita mpaka kwa wahusika, wahandisi wa maji, nimepita mpaka kwenye vyanzo vyenyewe tukalijenga, hili likawezekana.

Nashangaa, hivi sasa napata taarifa kwamba hali ni mbaya. Ni nini? Maboza ya wakubwa yanachukua maji maili sita, yanauzwa pale Sh. 500/= au Sh. 400/= nyuma walikuwa wanauza Sh. 1,000/= nikapigania wakapunguza bei ikafika Sh. 300/= kumbe imekaa muda mfupi tu, sasa imerudi pale pale. Jamani twende wapi sasa? Tukamlilie nani? Tukamwombe mlinzi gani atakayetusaidia katika haya?

Mheshimiwa Spika, mama mzazi anahitaji sana huduma. Jamani tunawadharau akina mama. Mwenyekiti wangu amezoea kusema, anayemdharau Mama mzazi kwa kweli anatenda dhambi iliyo kubwa, kwa sababu wote tusingekuwepo kama siyo mama. Sasa tunapompuuza mama, anakaa pale anatafuta watoto watakaokuwa Marais wa kesho, Mawaziri wa kesho, leo tunamweka katika mazingira magumu, anashindwa kupata huduma pale, tatizo liko wapi? *(Makofi)*

Masasi vyanzo vya maji viko karibu tu, na vingi tunashindwa nyenzo tu. Tulijaribu kumwandikia Sabodo alisema kwamba anasaidia visima. Mimi waniambie hata kwa kujitolea senti yangu hiyo hiyo ndogo nitoe angalau igharamie kichimbwe kisima cha hospitali ili kiwasaidie wananchi. Kwa kweli inasikitisha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, niende kwenye kilimo. Masasi, wakulima wanaitii sana amri ya Serikali.

*(Hapa kengele ya pili iligonga kuashiria muda wa mzungumzaji kwisha)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Sasa namwita msemaji wetu wa mwisho asubuhi hii, Mheshimiwa Elizabeth Batenga.

**MHE. ELIZABETH N. BATENGA:** Mheshimiwa Spika, naomba nikushukuru kwa kunipa nafasi ili nami nichangie katika hoja ya Waziri Mkuu ambayo iko mbele yetu.

Kwa heshima kubwa, nawashukuru sana Wanawake wa Mkoa wa Kagera, Chama cha Mapinduzi kwa kunipendekeza na Tume ya Uchaguzi ikaniteua kuwa Mbunge katika jumba hili Tukufu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba nikupongeze wewe kwa kuteuliwa na Bunge hili Tukufu kuwa Spika wa Bunge. Ni heshima kubwa sana kwa sisi Wanawake na sisi tunakuombea Mwenyezi Mungu akujalie hekima na busara katika kuendesha mikutano na vikao vya Bunge hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba nianze kuchangia kwa kuangalia matatizo yaliyopo Mkoani kwetu Kagera. Ni jambo la kusikitisha, linatia huruma, lakini pia linaitia aibu Serikali yetu kwamba katika baadhi ya maeneo kuna matukio yanayoashiria kuvunjika kwa amani, kuna matukio yanayoashiria unyanyasaji wa wananchi wetu. Katika Kata za Murusagamba na Kasulo, Wilayani Ngara, yamejitokeza matukio ya kujirudiarudia ya wahamiaji wanaoitwa ni wahamiaji haramu ambao wamehalalishwa kwa vibali bandia vya Idara ya Uhamiaji, wakahamia katika maeneo ya wananchi na kuanza kuwasumbua, wanalisha mifugo yao katika mashamba ya wananchi na wananchi wanapojaribu kujitetea, kinachofanyika ni mauaji. Mpaka hivi sasa napozungumza katika matukio hayo ya kujirudiarudia wananchi 16 wamekwishauawa katika Kata ya Murusagamba, kijiji cha Murubanga.

Mheshimiwa Spika, nimesema kwamba ni kitendo cha aibu kwa sababu Wilaya ya Ngara ina Kamati ya Ulinzi na Usalama, Mwenyekiti wake ni Mkuu wa Wilaya lakini Mkuu huyu wa Wilaya nashangaa kwa sababu amelalamikiwa na wananchi hadharani tunaona hata katika *TV*, amelalamikiwa hata na Chama cha Mapinduzi na wakamdai avue gamba, lakini hatuoni Serikali inachukua hatua gani. Hivi wananchi hawa watanyanyasika mpaka lini katika maeneo yao kutokana na wahamiaji haramu hawa wanaoingia na mifugo yao? Si katika maeneo haya tu, ni maeneo mengi ya Mkoani Kagera, mapori ya Mkoani Kagera yamejaa wahamiaji haramu waliohama na mifugo yao kutoka nchi jirani. Kwa hiyo, bila hata kuzungumzia sana, najua Serikali inafahamu lakini tunapenda tujue ni hatua gani zinazochukuliwa za kukomesha matukio haya. Tunaomba tujue na Mheshimiwa Waziri Mkuu namwomba atakapokuwa anahitimisha basi atueleze ni hatua gani zinazochukuliwa kukomesha vitendo hivi, ni vitendo vya aibu kwa Serikali yetu. Ni vitendo ambavyo vinatia huruma kwa wananchi wetu kuwa wakimbizi katika nchi yao, kunyanyasika katika maeneo yao badala yake wahamiaji haramu wanalindwa na kutetewa na wale ambao tulifikiri wangewatetea wananchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, la pili, naomba kwa kifupi nizungumzie kuhusu mradi wa Kabanga *Nickel*. Huu mradi uko Wilayani Ngara katika Kata ya Bugarama. Ni mradi wa siku nyingi. Mimi najaribu kuuita labda ni ile hadithi ya Mradi wa Kufikirika kwa sababu ni miaka mingi sana tumeusikia mradi huu. Mradi huu unakwama kwa sehemu kubwa kutokana na Serikali kutoweka miundombinu inayouwezesha kuanza. Mradi utakapoanza itachimbwa *nickel* nyingi ambayo itabidi isafirishwe, sasa itapita wapi, hewani na hewani kwenyewe hata ndege zitatua wapi? Kwa hiyo, inahitajika au ni barabara au reli, lakini pia umeme pale unahitajika.

Mheshimiwa Spika, sisi tunafikiri kwamba mradi huo ungeanza, ingekuwa ni msaada mkubwa sana kwa wananchi wa Mkoa wa Kagera lakini hususan Wilaya ya Ngara na Kata husika ya Bugarama vijana wakapata ajira lakini na wananchi pia wakapata sehemu ya kuuzia mazao yao ambayo yatawawezesha kujiinua kiuchumi. Ombi letu, Serikali imefikiria kwa muda mrefu, imepanga kwa muda mrefu sasa tunataka kuona kazi, tunataka kuona utekelezaji, hiyo reli inayosemwa basi tuone inaanza. Huo

umeme utakaotoka Geita unaosemwa basi na umeme huo tuone kazi inaanza kwa sababu ni miaka mingi, nadhani nimesikika.

Mheshimiwa Spika, jambo la tatu, naomba nizungumzie kuhusu barabara. Tunatoa shukrani kwa Serikali yetu kwamba barabara nyingi hata za vijijini Mkoani Kagera zinapitika kwa kipindi cha mwaka mzima na hilo kwa kweli tunaishukuru sana Serikali Kuu na hata Halmashauri zetu. Sasa tunaomba ahadi ya Rais kuhusu ujenzi wa barabara za kiwango cha lami kutoka Bugene kupita Nkwenda na kuelekea Kaisho mpaka Murongo, tuone inaanza kujengwa. Barabara ya Mgakorongo kupita Rwambaizi, Businde hadi Murongo na yenyewe ijengwe. Hizi barabara zinapita katika maeneo ya uzalishaji mkubwa wa kahawa, maharagwe, ndizi, ulezi na vitu vingine. Kwa hiyo, wananchi watanufaika kwa kupata urahisi wa kusafirisha mazao yao.

Mheshimiwa Spika, ujenzi wa barabara ya Kyaka hadi Bugene umeanza lakini tunapenda uende kwa kasi zaidi na ijengwe hadi Kasulo Wilayani Ngara kwa sababu ni ahadi ya Rais. Barabara ya Kagoma hadi Lusahunga ilikuwa imesuasua katikati, mwaka huu nashukuru fedha imetengwa, kwa hiyo, tunaomba hiyo barabara ikamilike tujue kwamba imekamilika na sisi tusherehekee.

Mheshimiwa Spika, napenda kuwashukuru sana wananchi wa Mkoa wa Kagera, Wanawake wa Mkoa Kagera ni watu wanaojituma, wanafanya kazi zao kwa bidii sana, akina mama wanalima, wanazalisha, wanafanya shughuli zote za ujasiriamali kwa lengo la kujitegemea. Kwa hiyo, napenda niwapongeze sana na nizidi kusema kwamba wasonge mbele, wasitetereke na sisi tuko pamoja nao na Serikali yao iko pamoja nao.

Mheshimiwa Spika, naomba nikushukuru tena kwa kunipa nafasi hii na niseme kwamba ubarikiwe sana na naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, naamini kabisa anayefuatia dakika 10 atakataa tu labda kama atakubali. Mheshimiwa Madabida, unaweza au usubiri mpaka mchana?

**MHE. ZARINA S. MADABIDA:** Tusubiri mchana Mheshimiwa Spika, dakika hizo hazinitoshi.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, kama nilivyosema dakika hazitoshi, kwa hiyo, tukirudi mchana ataanza kuongea Mheshimiwa Benardetha Mushashu atafutiwa na Mheshimiwa Maria Hewa, Mheshimiwa Maria Hewa nasikia amepata taarifa ya matatizo nyumbani kwake amepata msiba, lakini mchana atakuwepo. Atafuatia Mheshimiwa Zarina Madabida, Mheshimiwa Riziki Said Lulida ajiandae na wengine watatajwa na Mwenyekiti atakayeshika nafasi jioni.

Waheshimiwa Wabunge, sasa nasitisha shughuli mpaka saa 11.00 Jioni.

*(Saa 7.50 Bunge lilisitishwa mpaka saa 11.00 jioni)*

*(Saa 11.00 jioni Bunge lilirudia)*

*Mwenyekiti (Mhe. Sylvester M. Mabumba) Alikalia Kiti*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, kama tulivyotangaziwa mchana kwamba wafuatao ndiyo wataanza. Tutaanza na Mheshimiwa Benardetha Mushashu na wafuatao wajiandae. Mheshimiwa Maria Hewa, Mheshimiwa Zarina Madabida, Mheshimiwa Riziki Said Lulida na Mheshimiwa Abdulkarim Shah, Mheshimiwa Benadetha Mushasha!

**MHE. MHE. BENARDETHA K. MUSHASHU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi niweze kuchangia.

Kwanza kabisa na kwa uzito wa pekee, nalishukuru Bunge lako Tukufu, kwa kunichagua niwe Mbunge wa Afrika. Nachowaahidi ni kwamba nitaliwakilisha Bunge vizuri na nitajitahidi kuwakilisha nchi yangu ya Tanzania vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimpongeze Mheshimiwa Waziri Mkuu, Mawaziri wote walio chini ya Ofisi yake, Naibu Mawaziri, Makatibu Wakuu na Watendaji wote, kwa Hotuba iliyoandaliwa vizuri ambayo inatia matumaini Watanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niipongeze Serikali kwanza kwa kudumisha amani katika Tanzania. Wote tunatambua watu wengi wanaitamani Tanzania kwa sababu ya hali ya amani tuliyokuwanayo. Kwa hiyo, niwaase ndugu zangu wale wanaojaribu kuindoa amani hii tusikubaliane nao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile naipongeza Serikali kwa mipango mingi na mambo mazuri na mafanikio mengi tuliyoyapata. Kwa mfano, tumeweza kujenga shule za Sekondari kila Kata, tumeweza kuweka mtandao wa barabara za kila Mkoa, hongera Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kuchangia kuhusu mishahara ya watumishi. Naipongeza Serikali kwa mkakati uliowekwa sasa wa kujaribu kuwapunguzia wananchi makali ya wa maisha. Ili mkakati huu uweze kufanya kazi, inabidi hata mishahara ya watumishi iangaliwe upya. Kwanza, ni midogo sana, haitoshelezi mahitaji lakini vilevile kwenye mishahara hiyo kuna kodi nyingi, vilevile mfumo wa kodi wa Tanzania unamminya mno mfanyakazi kuliko mfanyabiashara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni jukumu la kila mtu kulipa kodi, wote tunatambua jukumu hilo kwa sababu bila kodi huwezi kuendesha nchi. Wafanyabiashara wanalipa kodi lakini anachofanya mfanyabiashara mwanzoni mwa mwaka anatakiwa kuandika hesabu, anaonesha mapato na matumizi, anaonesha hasara na faida na analipa kodi kufuatana na faida atakayopata, ikifika mwisho ikaonekana amelipa zaidi anaweza kurejeshewa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile wako wafanyabiashara wakubwa wenye mauzo ya kama milioni 40 na kuendelea unakuta hao wanasaidia Serikali kukusanya Kodi ya *VAT*, wanaponunua mali za kupeleka kwenye maduka yao wanalipa *VAT*, wanapouza zile mali basi wanachangisha *VAT* lakini mwisho wa mwaka ikionekana alilipa zaidi kuliko alichokusanya Serikali inaweza ikamrejeshea. Kwa hiyo, yeye halipi *VAT* lakini anasaidia Serikali kukusanya ile *VAT* kwenye mali anayouza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumuangalie mtumishi sasa. Mtumishi anakatwa kodi kufuatana na mshahara anaopata, *Pay As You Earn*, wanakata tu asilimia bila kujali matumizi yake. Kwa hiyo, unakuta mtumishi huy huyu ni mlaji wa mwisho analipa na kodi kama *VAT* na kadhalika. Mwisho wa siku kale kamshahara kameshakuwa kadogo kiasi kwamba hakakidhi yale mahitaji yake. Ili kumsaidia huyu Mtumishi wa Umma, kwanza napendekeza Mfumo wa Kodi unaotumiwa Tanzania uangaliwe upya. Inawezekana isiwezekane katika Bajeti hii lakini kwa mwaka kesho na kuendelea ili na mtumishi alipe kodi *yes*, lakini naye aoneshe matumizi yake, mshahara wangu ni kiasi hiki, ndiyo mapato yangu, atoe matumizi yake kwa maana ya chakula, kwa maana ya nauli, kwa maana ya pango, kiasi kinachobaki ndiyo kama faida, ndiyo kitozwe kodi, kuna nchi nyingine wanafanya hivyo. Kwa kufanya hivyo, ndiyo tutakuwa tumemsadia Mtumishi wa Umma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni utamaduni mzuri wa Serikali ya Awamu ya Nne kuwa mara kwa mara wanawaongezea watumishi mishahara. Je, ni lini sasa Serikali itaongeza mishahara ya watumishi ili kuwapunguzia huu ukali wa maisha uliopo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na hilo, watu wengi wameongea, miaka iliyopita tumeongea, kuna watu wanaitwa Madiwani. Sasa hivi tunapeleka hela nyingi, Halmashauri inamhitaji huyu Diwani awepo kila siku aweze kusimamia miradi kwenye Kata, aweze kusimamia Halmashauri na aweze kwenda kwenye mikutano ya maamuzi ndani ya Halmashauri, inaonekana itakuwa *full time job. Therefore,* kama wengine walivyopendekeza, naomba Serikali iliangalie upya suala hili ili Madiwani sasa walipwe mishahara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, madeni yaliyotokana na mtikisiko wa uchumi. Mtikisiko wa Uchumi wa mwaka 2008/2009 ulitikisa nchi nyingi na kila nchi ilikaa ikajiwekea mkakati wa kupunguza hayo makali kusudi uchumi wake usianguke. Kwa sababu ya mtikisiko huo, sisi Tanzania wale wanaofanya biashara ya kununua na kuuza kahawa, kununua na kuuza pamba, waliathirika vibaya sana kwa sababu walinunua kwa bei ya juu, walipokwenda kuuza kwenye soko la dunia bei ikawa imeporomoka sana wakapata hasara. Kwa hiyo, kama nilivyosema, kila nchi iliweka mpango wa namna gani wa kunusuru uchumi wake hata Amerika waliweka mkakati lakini wao walikwenda *step further* kwa sababu pamoja na mkakati huo waliutungia Sheria ambayo kwa kifupi inaitwa *The Stimulus Act, 2009.* Wakachukua hela wakaweka kwenye mfumo wa uchumi wao sasa hivi tunaambiwa kwamba uchumi unaendelea vizuri na ajira zimeanza kuongezeka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi hapa Tanzania tunamshukuru Mheshimiwa Rais kwa sababu na mwenyewe aliridhia ukapitishwa mpango wa kunusuru uchumi, *The Economic Stimulus Package* ya mwaka 2009. Bunge hili wakatuletea maombi ya shilingi trioni 1.7 tukaridhia ili kusudi hizi fedha ziingizwe kwenye uchumi wa Tanzania ziweze kuwanusuru hawa ambao wamepata hasara kubwa kutokana na bei za soko la dunia. Hizi fedha zilipaswa kwenda kusaidia Vyama vya Ushirika, makampuni ya watu binafsi na asasi zote zilizokuwa zinashughulika katika kuuza na kununua pamba. Hizi fedha zilikuwa ni kwa ajili ya hasara walizopata lakini vilevile kuwalipia madeni ya Benki kwa sababu wangeshindwa kuyalipa kwani walikuwa wamepata hasara kubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, upande wa kahawa, Serikali haikufanya vizuri sana, kwa sababu ni makapuni machache sana na Vyama vya Ushirika vilivyolipwa hiyo fidia. Kwa mfano, Kagera *Cooperative Union (KCU)*, wao walipata hasara kubwa, Serikali iliwataka wapeleke mahesabu yao, wakayapeleka, wakawa wanaomba shilingi bilioni 1.3. Serikali ikapeleka Wakaguzi wakakagua hayo mahesabu ikaonekana wanastahili kulipwa milioni 734,369,379.49 na Serikali ikawaandikia barua, ikatoa ahadi na barua hiyo iliandikwa na Hazina mwaka 2010.

*(Hapa kuna Waheshimiwa walikatisha kati ya Kiti na Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI**: Samahani. Bahati mbaya majina sijayafahamu lakini Mheshimiwa aliyepita mbele ya Mushashu na Mheshimiwa Halima Mdee, mmefanya makosa ya kukatisha baina ya Mwenyekiti na Msemaji kwa hiyo mtunze utaratibu ule unaozuia kupita kati ya Msemaji na Kiti. Haya endelea!

**MHE. MHE. BENARDETHA K. MUSHASHU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nitaomba muda wangu unirejeshee.

Kwa hiyo Hazina iliji-*commit* kama Serikali ikawaandikia *KCU* kwamba watawalipia hizo milioni zaidi ya 700 zilizotokana na mtikisiko huo mwaka 2010. Hadi leo ahadi hiyo haijawahi kutekelezwa. Vilevile na makampuni ya watu binafsi na wao waliomba, Serikali ikafanya uhakiki makapuni kama ya Amri Hamza Ltd na mengine yaliyopata hasara na wao waliandikiwa barua mwaka 2010 kwamba watapata hizo fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *KCU* wamefuatilia, mashirika yamefuatilia sisi Wawakilishi wao tumefuatilia lakini hadi leo ahadi hiyo haijalipwa. La kushangaza basi, juzijuzi hivi, April mwaka 2011, Hazina hiyohiyo imewaandikia barua kwamba wanasitisha kuwalipia fidia hizo na sababu walizozitoa ndiyo wananishangaza. Kitu cha kwanza wanasema ni kwa sababu Hazina haina fedha, lakini sababu ya pili waliyoitoa wanasema hilo zoezi lilishaisha tangu mwaka 2010. Sasa kosa ni la nani, nashindwa kuamini kwamba ni Serikali hiyohiyo iliyoandika barua kutoa *commitment* na Serikali hiyohiyo inawezaje kuwageuka wananchi wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi kama Bunge tuliidhinisha shilingi trilioni 1.7 kwa nini hawa wakulima wa kahawa wasilipwe? Ikumbuke kuwa *KCU* ni Chama cha Ushirika kikongwe Mkoani Kagera, kinachonunua kahawa za wakulima wote wa Muleba

Wilaya nzima, Bukoba Vijijini, Bukoba Mjini na Wilaya nzima ya Misenyi. Kwa sasa hivi Serikali imetumia fedha nyingi kuhakikisha kwamba hivi Vyama vya Ushirika vinazidi kuboreka kusudi viendelee kuwahudumia wakulima, sasa hivi *KCU* ina madeni makubwa yaliyotokana huo mtikisiko, watashindwa kununua, kahawa za wakulima zitaenda kwa walanguzi na zitapelekwa Uganda watu watapata hasara na Tanzania itapata hasara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeamua kuchangia suala hili kwenye hotuba ya Waziri Mkuu nikitambua kwamba Waziri Mkuu ni mtoto wa Mkulima na ana mapenzi makubwa sana na wakulima na anawathamini sana. Kwa hiyo, ni mategemeo yangu kwamba atakapokuja ku-*wind up*, atatoa jibu zuri litakalowatia matumaini, awaambie Serikali sasa itawalipa lini hilo deni pamoja na kampuni nyingine zilizokuwa zimeombwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, umaskini Mkoa wa Kagera. Mkoa wa Kagera haupaswi kuwa maskini kwa sababu ni Mkoa mkubwa na una ardhi mkubwa, una watu wengi, mvua zinanyesha kati ya miezi mitano mpaka minane kwa mwaka na Mkoa wa Kagera uko *strategically positioned* kwa sababu umepakana na nchi nyingine kama Burundi, Rwanda, Uganda hata kwenye maji tunapakana na Kenya. Katika miaka ya 1960, 1970 na 1980 na 1990 mwanzoni, Mkoa wa Kagera ulikuwa kati ya ile Mikoa mizuri mikubwa inayofanya vizuri kiuchumi na kielimu, ilikuwa kati ya ile Mikoa mitatu ya kwanza lakini sasa hivi Mkoa ule umerudi nyuma haijapata kuonekana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa miaka mitano mfululizo Mkoa wa Kagera uko kati ya Mikoa mitano maskini sana humu ndani ya Tanzania. Serikali imejitahidi, pato la Mtanzania wastani wa Taifa ni 770,000/- lakini hebu angalia, mkazi wa Karagwe, Mkoa wa Kagera ni 425,000/-, Bukoba Vijijini ni 386,000/-, Bukoba Mjini ni 385.000/-, Muleba ni 150,000/-, Misenyi ni 430,000, Biharamulo pato ni 420,000/-, Ngara ni 245,000/- Chato ni 360,000/-, pato la Mkoa kwa ujumla ni 453,000/- wakati pato la Taifa la jumla ni 770,000/-, Mkoa wa Kagera uko chini kiasi hicho. Hali hii inasikitisha, wanakoelekea sio kuzuri kwa sababu Mkoa unaendelea kuwa maskini kila kukicha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, takwimu hizi zilipotolewa mbele ya Mheshimiwa Waziri Mkuu akiwa ziarani Mkoani Kagera nilimwona alisikitika lakini akasema kama takwimu hizi ni sahihi basi awatake wale wote waliopewa dhamana kwamba kila mtu akae chini, ajipange, aone atawezaji kuutoa Mkoa au Wilaya hapa ili uweze kusogea mbele. Mimi nasema haiwezekani, tatizo hili limeshakuwa kubwa sana hatuwezi kumwachia Mkuu wa Mkoa na Wakuu wa Wilaya na Wakurugenzi waliopo. Hatuwezi kuendelea na *business as usual* kwa hali Mkoa ulipofikia. Mfano Mkoa wa Kagera kilo moja kahawa inauzwa mpaka shilingi 1,300/- hadi 1,500/- wakati Moshi inauzwa mpaka shilingi 3,800/- na kuendelea, kwa nini? Je, aina ya mibuni wanayopanda ni mibaya? Je, soko la kahawa wanakouza ndiyo hakufai? Je, labda *processing* ndiyo mbaya? Tunaomba Serikali itusaidie. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, zao la chakula ni ndizi. Hizi ndizi ukiona wakulima wa Uganda ambao wamepakana na Kagera wao wanauza mpaka nje, wana soko Uingereza,

wana soko Uarabuni. Serikali inafanya nini kumsaidia huyu mkazi wa Kagera ambaye anaonekana uchumi umeporomoka kusudi aweze ku-*access* hayo masoko ya nje na kuuza ndizi zake kule?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mkoa wa Kagera umeshambuliwa na magonjwa mengi, magonjwa ya ndizi, magonjwa ya mibuni, wataalam wanatumbia ukiona mgomba umeathirika kata, ukiona mbuni umeathirika kata, atakata mpaka wapi? Hivi kama wataalam humu ndani wameshindwa kutafuta dawa basi tutafute wataalam nje waje wasaidie Mkoa wa Kagera kwa sababu haya magonjwa yapo zaidi ya miaka saba sasa. Kwa hiyo, naiomba Serikali kama wanaweza watusadie wataalam kutoka nje waweze kutusaidia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nachosema ni kwamba haiwezekani tukafumba macho wakati Mkoa ulikuwa kati ya Mikoa ya kwanza, Mkoa wa Kwanza ulikuwa Kilimanjaro, Mbeya na Kagera yote inacheza namba moja mpaka namba tatu, sasa umeporomoka mpaka Mikoa mitano ya mwisho tena sio kwa mwaka mmoja *for five consecutive years, there is a problem.* Tunaomba Serikali, tunajua ina wataalam wengi, ina watafiti, waletwe Kagera waangalie tatizo ni nini na baada ya kupata tatizo, uwekwe mpango kabambe na mradi makini wenye fedha nyingi wa kuweza kunusuru Mkoa wa Kagera. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, MV Bukoba ilizama…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MHE. MHE. BENARDETHA K. MUSHASHU:** Dakika zangu? Naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MHE. MARIA I. HEWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipatia nafasi hii walau na mimi nizungumze kuhusu suala zima la Hotuba ya Waziri Mkuu katika jioni hii ya leo. Nilikuwa nimetoka kwa ajili ya matatizo ya kidunia, nimerudi na nimemaliza kazi niliyokwenda kuifanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa, nipende kuipongeza Serikali ya Chama cha Mapinduzi kwa hatua iliyofikia, sasa hivi tuko mbele na nafasi yetu ni nzuri tu kimaendeleo. Mimi nilishangaa wakati Mheshimiwa Wasira alipozungumza kwamba nchi hii tulipewa uhuru na umeme wa *diesel*, nilichoka! Nikasema ama kweli, kumbe tumetoka mbali hivyo! Pamoja na umri wangu huu kumbe tumetoka mbali hivyo? Hongera Serikali ya Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kuzungumzia suala zima la Mwanza. Katika Hotuba ya Waziri Mkuu wametaja Manispaa ambazo zimepitishwa ikatajwa ya Lindi. Kipindi kilichopita tu katika Bunge hili walitamka Mwanza pia imo katika kupewa Manispaa. Kwa kweli nilishikwa na butwaa, nikatetemeka, nikasema tutawaambia nini wana Mwanza, kwamba tumeanza hatua zote, tangu wadau tukafuata Baraza, tukafuata *RCC* na mpaka tukafikisha kila hoja hapa Taifani na mpaka Taifa likatamka, kuna nini?

Kama kuna kitu, sisi tupo tayari kukifuatilia na nimeshaanza kusikia watu wanataka kuhodhi madaraka kuitwa wanajiji fulani na nani wa jiji, tutayaleta humu na sisi tutasema. Mwanza inataka maendeleo katika maeneo madogo, hatutaki kuwa na maeneo makubwa yanayotushinda, tunataka maeneo ambayo yatakuwa muafaka ili tuweze kuendelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata usafi wa Mwanza tulikuwa tunapambana na Moshi tukiwa bado ni Manispaa, sisi usafi umeanza tukiwa Manispaa, mimi nikawaambia wana-Mwanza sisi ni lazima sasa tuweze kuwa wa kwanza, tukipambana na Manispaa ikiwemo Manispaa ya Moshi. Wakati huo mimi nikiwa Naibu Meya, nilimwambia Naibu Meya mwenzangu sasa Mwanza inachukua ushindi, leo tumekuwa washindi wa usafi kwa mara ya sita mfululizo, kwa sababu tumedhamiria. Leo tumedhamiria kuwa na Manispaa tufanye mambo yetu inatokea nini? Nahitimisha katika hilo kwamba tunataka Manispaa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili ni kuhusu maji katika Mji wa Mwanza. Bomba kuu lile linalotoa maji *Lake Victoria* linapeleka Shinyanga mpaka Kahama kwa binadamu kama sisi sina tatizo kabisa cha kushangaza kilio cha wana Mwanza wanaozunguka Ziwa Victoria hawana hata tone la maji ya bomba. Ukianzia Ihelele pale na wananisikia, Kwimba yote haina maji hayo ya bomba, hivi kweli tuwe tunaangalia kwa macho tu maji yanakwenda? Sisi mnadhani hatupendi kuona maji ya bomba yakoje, yanapitiliza tu!

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwamba ngoma huvutia kwake, hebu na sisi mtufikirie katika hili, hawa watu wa Kwimba hawana kabisa maji, wanaliona hilo bomba linapita. Lingekuwa ni la plastiki tungeshawishi vinginevyo, lakini kweli inatia uchungu sana. Tunaomba na sisi linamopita bomba basi watuwekee mabomba ili hao akina mama wa maeneo yale wapate maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, huwa kuna majibu yanayotoka kwamba ninyi mna Ziwa karibu, hivi mnaifahamu Kwimba ilivyo? Kuna sehemu inaitwa Kinduru ni kilomita sijui ngapi tena inawezekana hata Ziwa hawalijui lakini linapita kwake, tunaomba Serikali iliangalie suala hili kwa mara ya pili. Mimi naelewa kabisa Waziri wa Maji Mwandosya ni mwamba kweli, ana sifa zake za kipekee kabisa katika Wizara hii ya Maji, siwezi nikambeza hata kidogo, anatosha kabisa lakini atufikirie, wale watu wapate maji. Natoa ombi rasmi wapate maji, maji yanapita kwao wanabaki wanaduwaa Wasukuma hawa. Tunaomba maji ya bomba hilohilo kubwa tupate na sisi maji yanayokwenda kwa wenzetu. Tunapongeza Serikali imefanya vizuri sana lakini hebu irudi nyuma sasa ifanye hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti jambo la pili ni maji ya visima, visima hivi vimechimbwa vingi sana hongera sana, lakini visima hivi ni vya muda mfupi siyo vya mwaka mzima. Nadhani lengo la kisima kinapochimbwa sehemu kihudumie mwaka mzima, lakini kisima kinakaa miezi mitatu kinakauka maana yake ni nini? Ukienda vijijini huko ni uyoga wa visima ambavyo havina maji kabisa, maana yake nini? Napendekeza, kama tulifanya makosa mwanzo, vile ambavyo havitoi maji mwaka mzima

Halmashauri ya eneo lile ifanye sensa ya hivyo visima ivizibue tena viweze kufanya kazi kama inawezekana kwa gharama ya Halmashauri kwa sababu miradi hii inapitia huko. Maana kila kitu ukizungumza unaambiwa sijui kuna *NGOs* gani inazungumzwa kila kitu kinapelekwa Halmashauri, sasa kama hata hivyo visima vinapitia Halmashauri na Halmashauri siyo makini basi walijue hilo. Waripoti kwenye *WDC* zao kwamba visima kadhaa vilikabidhiwa Halmashauri, tuzungumze upya juu ya mauyoga ya visima ambavyo havitoi maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, akina mama wanateseka, akina mama wa Tanzania sasa hivi nao ni wastaarabu tu kwa sababu wanatengeneza vinywele vyao halafu bado mnawabebesha ndoo vichwani kwa misingi ipi? Anataka na yeye ashinde kutwa tangu asubuhi mpaka jioni akiwa msafi, leo mnataka tena akahemee maji sijui kutoka wapi. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, anapita huko visima vimekauka, anaenda kutafuta maji mbali, tulifanye zoezi hili na shauri hilo kabisa kila Halmashauri ijue inawajibika vipi na visima na je vinafanya kazi au havifanyi kazi na kama havifanyi kazi ni vingapi, je tuna mikakati gani ya kuvifufua visima hivi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo linalofuata ni kuhusu njaa...

**MBUNGE FULANI:** Muwe mnalima!

**MHE. MARIA I. HEWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, najibiwa huku na wanaopita, wachelewaji, wanasema eti tuwe tunalima. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi Mwanza huwezi ukatufundisha jembe, hata hayo matrekta lete tu tena wanawake wa Kisukuma wanasukuma *power tillers* wala hawatishiki katika hilo, lakini ni Mwenyezi Mungu hakuleta mvua. Watu wa Kusini wanatamba hapa wana mahindi ambayo hayana kazi, wamekula wameshiba hayana kazi, yapandishwe yaende Kaskazini huko. Tunangoja nini mpaka tunazungumza wenyewe humu na wananchi wanatusikia na njaa zao kule. Watu wa Kusini wanatutangazia hapa Serikali inasema nini juu ya suala hili? Sisi tutaendelea kusema kwamba Serikali imekaa lakini chakula kipo Kusini. Hatutaki kusema hivyo, Serikali ya Tanzania ni sikivu, naomba mlisikie jambo hili mpeleke chakula hiki kiweze kutumika kwenye maeneo ya watu wenye njaa. Tanzania hii imegawanyika katika mkondo huo, wengine wanapata na wengine wanakosa, wanaopata basi wawape wanaokosa. Serikali ilifanyie kazi suala hili na kama ndiyo hali halisi hiyo, sasa nadhani tutakwenda vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kwa ufupi sana nizungumzie suala la umeme. Mheshimiwa Simbachawene hapa nilisikia sehemu akisema kwamba hatuhitaji kuzungumza zaidi, sisi tunataka umeme, Mwanza imejaa viwanda, viwanda bila umeme ni magofu, tunataka umeme hatuhitaji tena historia. Fikiria mpaka Wabunge wanafikia hatua ya kusema hatutaki semina, ujue uchungu walionao kuhusu suala zima la umeme, kwa hiyo, leteni umeme. Umeme una gharama gani, yatajitokeza mbele ya safari, weka

umeme basi, sisi tunataka umeme. Jamani katika maeneo yanayoathirika na umeme ni pamoja na Mwanza, tunataka umeme.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, Watanzania tunaomba tutunze amani. Msemo wangu siku zote ninasema kwamba amani ina gharama ikitupotoka na hasa sisi akina mama ndiyo wenye mateso makubwa. Mwanamke ni jasiri lakini mwanaume ni mwoga. Katika njaa mwanaume atakimbia, katika vita mwanaume atakimbia, sasa anayebaki anasota ni mwanamke na familia. Huwa wanatuambia ingia humu jifungie na watoto wako! Kwenye matatizo watoto wanakuwa wa mwanamke kwenye starehe hawa ni watoto wangu tena anaweka besi kama ya kwangu. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba tuitunze amani ili familia zidumu na familia ikidumu yote haya tunayoyaongelea hapa katika kuchangia Serikali yetu itafanya kazi katika amani, upendo na katika utulivu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kuzungumza hayo, naunga mkono hoja, Serikali yangu endeleeni kuchapa kazi. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Sasa nitamwita Mheshimiwa Zarina Shamte Madabida na Mheshimiwa Ruziki Said ajiandae, pia Mheshimiwa Abdulkarim Shah ajiandae.

**MHE. ZARINA S. MADABIDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza naomba nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa wasaa huu wa kuchangia katika hotuba ya Waziri Mkuu pamoja na ofisi zake zote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa, naomba nimpongeze Waziri Mkuu, Mawaziri na Watendaji wote wa ofisi ya Waziri Mkuu kwa hotuba nzuri sana ambazo zinajieleza zenyewe na zimepangwa kuendena na mpango mzima wa maendeleo kwa Mtanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba pia nichukue fursa hii kuipongeza Serikali ya Chama cha Mapinduzi, kwa kazi nzuri ambayo imekuwa ikiifanya kwa awamu zote. Mtu aliyeondoka Dar es Salaam miaka miwili, mitano au kumi na tano iliyopita akirudi leo anapotea jinsi kulivyojengeka, barabara, shule, kila kitu kipo pale. Unashangaa labda pengine wenzetu waliozaliwa juzijuzi hapa, lakini kwetu sisi tuliosoma wakati huo kulikuwa na shule za sekondari za wasichana nne tu, mwanamke kama hukuenda Jangwani umekwenda Zanaki, kama si Zanaki, Kisutu, kama si Kisutu, *Goan School* ambayo sasa hivi wanaita Kibasila. Leo Kata 74 kila moja ina shule na mtoto wa kike ana fursa ya kwenda shule, leo kuna hospitali, leo kuna vyuo, zamani hizo shule ninazosema hata *private* hakuna, siyo kwamba umeshindwa utakwenda *private* hakuna! Shuleni kwetu mimi nakumbuka tulifaulu watano tu, leo nimesoma kwenye kabrasha watoto wote waliofaulu wameweza kwenda Sekondari, mimi naipongeza Serikali ya Chama cha Mapinduzi, Waswahili wanasema “asiyekuwa na macho haambiwi tazama na asiyejua maana haambiwi maana”. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Jiji la Dar es Salaam ni Jiji Kuu la biashara, wote tupo kule. Hata hapa Waheshimiwa Wabunge wana nyumba, yupo Mbinga, yupo na Dar es Salaam, yupo Isamilo yupo na Dar es Salaam, yupo Lushoto yupo na Dar es Salaam, kokote aliko na Dar es Salaam yupo. Wafanyabiashara ndogodogo wanaingia kila siku na sisi tunasema karibuni wote kwa sababu ndiyo Jiji la biashara hata ningekuwa mimi ningekuja. Nina kaka yangu ameenda baada ya miezi sita sisi tukiwa na shida yeye ndiye tunampelekea atusaidie, ningeacha kwenda? Hata na mimi ningekwenda. Sisi tunawaambia karibuni tuje tufanye biashara maana huko ndio kukua kwa uchumi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na hali hiyo magari yamekuwa mengi sana, msongamano mkubwa, uharibifu ni mkubwa sana wa barabara, ukichanganya na mvua ya mwaka huu Dar es Salaam pamoja na kwamba tuna mashamba nje ya Mji, lakini magari yameharibu barabara kwa kiwango kikubwa sana. Ikiwa kama tutaachiwa peke yetu, itatuchukua muda mrefu sana kuzirudisha pale tulipokuwa na kuziendeleza. Ninaiomba ofisi ya Waziri Mkuu itusaidie. Pamoja na kwamba nimeona kuna mapendekezo mazuri ya kujenga barabara za juu lakini barabara za ndani, za katikati zimeharibika sana kiasi kwamba nyingine hazipitiki. Inachukua masaa kutoka eneo moja kwenda eneo lingine. Mimi naomba Serikali itusaidie siyo tu zile barabara ambazo zipo chini ya *TANROAD* lakini na zile zingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niipongeze Serikali kwenye upande wa elimu imefanya kazi kubwa sana, imetoa sera ya kujenga shule katika kila Kata na zimejengwa, kwa kweli kama nilivyosema sasa hivi watoto wetu wanasoma lakini inasikitisha watoto hawa wanasoma wakiwa wamekaa chini. Dar es Salaam kuna upungufu wa madawati zaidi ya laki mbili, lakini siyo Dar es Salaam tu ni Tanzania nzima, ukiangalia watoto sehemu wanazokaa kusema kweli watoto wanasoma katika hali ya shida sana. Tutasherehekea miaka hamsini vipi wakati watoto wetu wanakaa chini wakiwa wanasoma? Naomba Serikali ilione hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sipendi kutoa matatizo bila kutafuta angalau na majawabu kidogo. Serikali ya CCM ni sikivu, Serikali ya CCM ina mipango, tupange na tujitolee tuseme kwamba kukaa chini watoto sasa basi. Kama tulivyosema kwamba tunataka shule na tumeweza, mimi nina hakika kama tukisema kwamba tunataka watoto wetu wakae kwenye madawati watakaa. Naomba kila Wizara, Waziri Mkuu ziko chini yako, utuombee *ten percent* ya *hospitality*. Bajeti iliyowekwa ya *hospitality* ile ya chai na kadhalika tupunguze hata kwa asilimia kumi tu. Nimefanya hesabu ninajua pale tutapata kama bilioni moja na kitu lakini na sisi Siasa ya Ujamaa na Kujitegemea tumeanza nayo kutokea enzi ya Mwalimu Nyerere, tusiulize tu Serikali itatufanyia nini, sisi wenyewe tutafanya nini. Mimi naomba kuwaambia ndugu zangu Watanzania na sisi tujitolee, wanaokaa chini ni watoto wetu, naomba kila nyumba moja kwa muda wa miezi sita tutoe japo shilingi elfu moja tu. Wabunge humu ndani kila mmoja kwa mwezi tutoe japo shilingi elfu hamsini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, soda kwenye mahoteli makubwa zinauzwa shilingi elfu moja wakati bei yake sehemu zingine wanauza shilingi mia tatu na hamsini, kwa nini tusiombe shilingi mia moja kutoka katika kila chupa ya soda kwenye mahoteli makubwa,

siyo hela nyingi. Tumepunguza tozo kwenye *petrol*, mimi nasema *diesel* ina *direct effect* na wananchi wote, *diesel* ndiyo ambayo inatumika kwenye matrekta, malori na sehemu za uzalishaji lakini *petrol* tunatumia kwenye magari yetu, tuweke shilingi mia moja kwa kila lita ya *petrol* ili tupate hela za kununua madawati ya watoto. Tukifanya hivyo, nafikiri tunaweza tukasaidia angalau kidogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niende kwenye suala la Watendaji. Manispaa zina Watendaji wazuri sana lakini wapo wachache wabovu. Sisi Kinondoni tulikuwa na tatizo kubwa sana lakini Watendaji hawa wapo TAMISEMI hatuna mamlaka nao, pamoja na kwamba tunataka kuwadhibiti. Mheshimiwa Lukuvi aliweka Tume, hatujajua bado Tume hiyo ilisemaje, lakini hata wale walioondolewa wanajaribu kurudi kwa mlango wa nyuma na ninyi TAMISEMI ndio mtakaowarudisha. Naomba chondechonde msiturudishie hao watumishi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini na Serikali iangalie kwa sababu hawa watumishi wakati mwingine hata akiwa mkorofi kule kwenye Manispaa anashindikana kuchukuliwa hatua kwa sababu mwajiri wake anaripoti TAMISEMI. Naomba hilo tuliangalie.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini nasema tuangalie pia makusanyo, pamoja na kwamba yanateteleka katika Manispaa lakini vyanzo vingine *TRA* ndio wanakusanya. Lakini nasema suala hili tungelirudisha ili kusudi wakusanye Waheshimiwa Madiwani, kwenye Manispaa. Pia hawa Madiwani, wanafanya kazi kubwa sana, lakini maslahi yao ni duni. Tuwalipe mshahara, tuwape malisho ili waweze kutufanyia kazi. Dar es Salaam kuna mahekalu, kuna nyumba nyingi ambazo ziko katika *squatter* lakini ni mahekalu ambayo hayakusanywi kodi.

Nashukuru Serikali imeamua kuongeza vyanzo vya kodi, kuna Wamachinga wengi tu ambao hakuna hata senti kumi wanayotoa, lakini barabara wanatumia, shule wanatumia. Nimeona hata wakilipa sh. 200/= kwa siku, nimepiga hesabu itatupa bilioni nane, je, tutakuwa hatujajenga barabara? (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kengele yangu imelia na bado nina maneno. Dar es Salaam tunapima viwanja lakini viwanja hivi ni mashamba ya watu yamechukuliwa. Mashamba haya tunapima viwanja vinauzwa *square meter* moja sh. 6,000/= mpaka sh. 10,000/=. Kiwanja kimoja sh. 3,600,000/= mpaka sh. 20,000,000/= kilipwe katika mwezi mmoja, kijengwe katika miezi 12 au 24. Mmachinga gani au mwanamke gani mwenye kipato cha kawaida anayeweza kulipa sh. 3,600,000/= katika kipindi cha mwezi mmoja? Matokeo yake ni kwamba siku zote tutaendelea kuwa wanyonge kwa sababu hivyo viwanja ndio mashamba yetu. Kwa hiyo, naomba suala hili liangaliwe kwa ndani sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nisimalize kabla sijasema kuhusu amani. Watanzania tusichoshwe na amani, maneno haya tunaambiwa ya mtaani siyo kweli ni uongo, hizi posho tunazoambiwa sijui posho watu hawazitaki siyo kweli na sisi tunajua na hata huko kwao zinaleta mtafaruku kwa sababu wamewaambia kama tukikataa posho hizi Chama kitufidie. Sasa ninyi kama posho hamzitaki kikweli kweli mnasemaje Chama

kiwafidie? Watanzania wasiongopewe, siyo kweli posho hizi zinafanya kazi kubwa sana. Nikiondoka hapa leo nikienda Dar es Salaam kusaidia tu akinamama wale siyo chini ya milioni tatu au milioni nne kabla sijarudi tena Bungeni. Je, posho sijaiacha huko huko Dar es Salaam? Sasa tusiwaongopee, pengine wenzetu wana vyanzo vingine vya mapato ndio maana wanasema hivyo. Kwa hiyo, niwaombe Watanzania waangalie sana kuna watu tunajua kuzungumza, kuna watu wanajua kuongopa, ndimi mbili jamani moja ya ukweli moja siyo ya ukweli. Kwa hiyo, naomba Watanzania wawe waangalifu na maneno haya wanayoletewa. Maneno ya kuambiwa changanya na ya kwako mwenyewe ndio akili. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, nasema Hotuba ni nzuri, naiunga mkono kwa asilimia mia kwa mia. Chama chetu, Mawaziri wote ni mahiri, wanachapa kazi, wanajua wanachofanya, songeni mbele. Kelele za mlango zisiwafanye wenye nyumba mshindwe kulala. Lakini mpate akili za kufanya mambo ya mapinduzi ya maendeleo kwa Watanzania. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja hii. (*Makofi*)

**KUHUSU UTARATIBU**

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Kuhusu utaratibu kanuni ya 64(1) ambayo inasema kwamba bila ya kuathiri masharti ya Ibara ya 100 ya Katiba inayolinda na kuhifadhi uhuru wa mawazo na majadiliano katika Bunge, ni marufuku kabisa kusema uongo Bungeni kwa Mbunge yeyote anapochangia hoja. Kama akisema ana wajibu wa kuthibitisha. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa Mheshimiwa Spika, alishatoa mwongozo wa lugha za kutumia ndani ya Bunge. Lakini pili, mwongeaji aliyetangulia kuchangia amezungumza maneno yanayohusiana na posho na kukielekeza kwa Chama ambacho kinazungumzia kupinga posho ambacho ni Chama cha CHADEMA.

**MBUNGE FULANI:** Mligombania posho Jumamosi.

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba unilinde.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mbunge, kaa chini. Ninapokuwa nimekaa hapa nasikiliza mazungumzo yote ambayo mchangiaji anakuwa anaongea. Mheshimiwa Mbunge, aliyemaliza kuchangia hakutaja jina la Chama chochote kwamba hiki Chama kinashabikia masuala ya posho. Mheshimiwa Mbunge, ulichokifanya hapa ni kutafsiri, pengine una hisia fulani, lakini hakuna mmoja katika sisi tuliyemsikia anaongea kuhusu CHADEMA, unapotosha Bunge.

**MBUNGE FULANI:** Taarifa.

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kitumie kiti chako vizuri.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mbunge, naomba ukae chini. Waheshimiwa Wabunge, naomba tuwe wakweli, msijaribu kuyumbisha kiti kwa sababu mimi nimesikiliza mazungumzo ya mchangiaji aliyemaliza kuzungumza sikusikia kutaja chama chochote ambacho kinashabikia mambo ya posho humu Bungeni. Tafsiri aliyoitoa Mheshimiwa Halima Mdee, hiyo ameitoa mwenyewe kwa hisia zake. Naomba Waheshimiwa Wabunge, tutumie muda wetu wa majadiliano kwa manufaa ya nchi yetu. Taarifa, miongozo naomba tusifanye kama mchezo hapa ndani. Naomba tuendelee.

**MBUNGE FULANI:** Taarifa.

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiendesha Kiti kwa ushabiki kitakushinda.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mbunge, sijakuruhusu kuongea.

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Chama gani ambacho kinazungumzia posho, usitake kupindisha mambo, akiseme ni kipi?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Halima J. Mdee, kaa chini.

**MBUNGE:** Kaeni kimya acheni fujo.

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Maana yake unapindisha mambo kwa sababu umepewa Kiti.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mbunge, kaa chini. Naomba unitajie ni mahali gani Mheshimiwa Zarina Madabida alitaja CHADEMA kama ni chama kinachoshabikia mambo ya posho katika mazungumzo yake? Ukishindwa kuthibitisha utoke nje.

**MBUNGE FULANI:** Ametoka kuvuta huyo.

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninachosema ni hivi, Vyama vinavyopinga posho vinajulikana CHADEMA, *NCCR* Mageuzi, hana haja ya kusema yeye *by implication* alichokizungumzia kinaashiria kwamba anavisema vyama hivi. Kwa hiyo, hana wajibu wa kutunga maneno kwa kukisemea CHADEMA wakati hana uhakika wa analolizungumza.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mbunge, nakuomba ukae chini. Waheshimiwa Wabunge, *order in the House*. Naomba msiyumbishe Kiti, hisia zetu tuweke pembeni, hakutaja Chama isipokuwa tunajaribu kufanya hisia zetu, angetaja Chama ningemtaka athibitishe. Lakini kwa bahati hakutaja chama. Naomba mchangiaji anayefuatia aendelee, Mheshimiwa Riziki Said Lulida aendelee.

**MBUNGE FULANI:** Huyo atoke nje.

**MHE. RIZIKI S. LULIDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote, napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu, *Allah Subhanah Wataala* aliyenijalia leo hii afya njema na hivyo kuweza kuchangia katika Bunge lako Tukufu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, siku ya Jumamosi kulikuwa na semina, siku ya Jumapili kulikuwa na semina na baadhi ya Wabunge tulikuwepo pale na tulichukua posho, hakuna hata Mbunge mmoja ambaye aliingia pale kwa kuangalia vyama vyote ambao walikataa zile posho, alikataa kuchukua.

**MBUNGE FULANI:** Hiyo ni Semina.

**MHE. RIZIKI S. LULIDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, napenda kusema kitu kimoja, tuko katika nchi ya Tanzania ambayo tunahitaji umoja, heshima na amani kwa unyenyekevu kabisa ningependa kuwaambia Wabunge wenzangu kuwa heshima ni kitu cha bure na tuendeleze amani ili tujengee heshima katika nchi yetu ya Tanzania kwa ujumla. Leo amani hii tuliyokuwa nayo ndio sasa hivi imetufikisha hapa kuwa na hekima fulani, kuonekana Tanzania ni nchi yenye amani, yenye utulivu, watalii mbalimbali wanakuja katika nchi hii wakijua nchi ya Tanzania ina amani. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, napenda kumpongeza Mheshimiwa Waziri Mkuu, kwa hotuba yake nzuri na yenye hekima ndani yake ambayo ameileta katika Bunge la Jamhuri ya Muungano. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, napenda kumpongeza Mheshimiwa Spika, mama Anne Makinda, ni Spika wa kwanza mwanamke ambaye amechaguliwa na Bunge hili kutuongoza. Kwa upendo kabisa mama Spika tulikuwa naye katika muda wa miaka mitano akiliongoza Bunge la Jamhuri ya Muungano akiwa Naibu Spika. Kwa kweli aliendesha vizuri na aliendesha Bunge hili kwa utulivu na amani. Hivyo kama kuna wachache walijaribu kupotosha amani au utulivu ndani ya Bunge hizo ni sababu zao binafsi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hivyo napenda kusema kitu kimoja, napenda kuchangia katika Mkoa wa Lindi. Hotuba hii imejaa mambo mazuri ya maendeleo na kadhalika. Lakini penye maendeleo hapakosi changamoto. Leo hii nauangalia Mkoa wa Lindi, kama Mkoa ambao uko nyuma hapa Tanzania. Lakini Mkoa wa Lindi kwa ujumla haupaswi kuwa Mkoa wa nyuma. Kijiografia Lindi Mwenyezi Mungu ametujalia kuwa na *natural resources* zote ambazo zinatuwezesha Lindi kuwa mbele kama Mikoa mingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano, leo hii Lindi tunapata *gas* asilia kutoka Songosongo, ile *gas* asilia ingeweza kusaidia kuanzia Kilwa, Mkoa wa Lindi, kwa ujumla mpaka imefika Dar es Salaam kusaidia Taifa kwa ujumla. Lakini changamoto inayopatikana Kilwa hawapati fedha za mrahaba kama Mikoa mingine wanavyopata kutokana na rasilimali zao. Kwa kutumia uwekezaji katika *gas*, Kilwa ingeweza kupata angalau laki mbili kwa mwaka. Hivyo inachangia Halmashauri ya Kilwa, kurudi nyuma kimaendeleo. Hivyo namwomba Mheshimiwa Waziri Mkuu, tuiangalie hii mikataba

angalau iwe mizuri, iwasaidie wale wawekezaji wawajibike kuisaidia Kilwa. Tumeona Kilwa imeweka nguzo za umeme kupeleka Dar es Salaam lakini leo ukitoka Nangurukuru kwenda Mbwemkuru hakuna umeme, wako gizani. Leo tunaambiwa kabisa umeme ni maendeleo na maendeleo ni umeme. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningemwomba Mheshimiwa Waziri Mkuu, kwa kupitia Waziri wa Nishati na Madini, aliangalie hilo suala la kupeleka umeme angalau katika Wilaya zinazozunguka Kilwa na vijiji vyake vipate ili na wao waone uwekezaji uliofanyika, Kilwa haijafanya makosa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la Lindi kupata fedha kidogo, nimejaribu kuhoji kwa muda wa miaka mitano lakini sijapata jibu ambalo linaniridhisha. Wengine wananiambia kuwa kuna *population* ndogo, ndio maana tunajikuta tunapata makadirio kidogo ya maendeleo na matumizi ya kawaida.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hebu niende katika hoja za msingi, hili tatizo linatokana na watendaji kule Lindi wanatukadiria matumizi madogo au Serikali katika Wizara ya Fedha au Waziri Mkuu kutukadiria matumizi madogo. Kwa mfano, leo naangalia Ruangwa, tuna Hospitali haina *x-ray* wala *Ultra sound*, haina wigo na magodoro, wazazi wanalala chini. Sasa unapotuletea bajeti ndogo kama hii wananchi wa Ruangwa wanajiuliza kulikoni kupata bajeti ndogo ambayo haikidhi mahitaji? (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo hii barabara za Lindi nyingi hazipitiki, ni mbovu. Leo natamani kwenda Liwale lakini Liwale nitakwenda wakati wa kiangazi. Lakini wakati wa masika inabidi nizunguke kutoka Lindi mpaka niende Nachingwea nikamate Liwale. Lakini kwa bajeti hii ndogo bado ninapata mashaka kulikoni. Kuna mikoa mingine kwa upendeleo wa makusudi wanapewa fungu la kutosha ili kukidhi mahitaji yao. Napenda kuhoji ni kwa nini na naomba nipate jibu la kueleweka. Mkoa wa Lindi, fedha za maendeleo bilioni 20, ni Mkoa wa mwisho, fedha za matumizi ya kawaida bilioni 56, Mkoa wa mwisho. Hata ule unaofuatia tunapishana kwa bilioni 18, hizo bilioni 18 zingetusaidia na sisi kuweza kujenga barabara, kupeleka katika maendeleo ya shule. Hatuna mabweni tunahitaji mabweni, tungeweza kununua madawati na kusaidia wananchi wa Mkoa wa Lindi angalau na wao wakaweza kuruka. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitaizungumzia Lindi katika suala la utalii. Sitaki kuzungumzia Ngorongoro wala wapi kwa vile tayari wanajitosheleza. Leo Mkoa wa Lindi tuna Selou ambayo theluthi mbili iko Lindi, Selous ya Kaskazini inaboreshwa. Lakini Selous ya Kusini imeachwa kama ilivyo, miundombinu mibovu, barabara hazipitiki na watalii watashindwa kwenda ili kuendelea kutupatia kipato na kuisaidia katika Mkoa wa Lindi. Kwa hali hii naona Serikali itoe dhamira ya makusudi kurekebisha ili hali hii isiendelee kwani ni kero na inaudhi kuona Mikoa mingine inapewa changamoto na kuweza kufanikisha miradi na maendeleo kiujumla, Lindi kulikoni? (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa leo uchumi wa Tanzania unakuwa kwa asilimia 7.2, lakini kama hujaisaidia Lindi utakimbiza wachache waende mbele Mkoa wa Lindi utabakia nyuma vile vile, kulikoni? (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nizungumzie suala la kilimo, leo hii usiangalie Lindi kwa kupita barabarani kutoka Dar es Salaam mpaka Lindi ukaiona Lindi ndivyo ilivyo. Lindi ina maeneo mazuri ya kilimo na naomba Waziri wa Kilimo atakapotaka kwenda Lindi tufuatane nikamwonyeshe maeneo mazuri ya kilimo. Maana yake pengine anapita barabarani hajaona mabonde mazuri, hajaona maeneo mazuri ambayo sasa hivi yanafaa kwa kilimo na kutuletea maendeleo katika Mkoa wa Lindi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na mazingira hayo hawaoni Lindi kwa nini isiingie katika (*SAGCOT) Southern Agricultural Growth Corridor* of Tanzania . Unapotaja *Southern* lazima utaje, Lindi, Mtwara na Ruvuma. Lakini katika *SAGCOT* haipo. Sasa hata kama mnataka kutuendeleza kwa makusudi lakini je, tutafikaje katika maendeleo kwa mfumo huu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tulikuwa na *Mtwara Corridor* ambayo hata sielewi kama ipo au imekufa maana hata bajeti yake ya *Mtwara Corridor* haipo. Tulikuwa na *Mtwara Corridor* Rukwa ilikuwepo, Mbeya ilikuwepo, Iringa ilikuwepo, Lindi ilikuwepo na Mtwara ilikuwepo na Ruvuma. Kwa nini kwenye *Southern Agricultural Growth Corridor of Tanzania* mmetutenga mmetuweka pembeni na wakati ndio mradi mkubwa ambao sasa hivi ungeweza kutusaidia katika kilimo? (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo hii nimepata mstuko lakini swali hili niliwahi kuliuliza karibu mara mbili au tatu, suala la *AGOA*. Mtaona ni vitu vidogo lakini vinakera na vinaudhi. Leo Kenya katika suala la mauzo na ku-*export* mazao yao Marekani wame-*export* kwa dola milioni 200, Tanzania tume-*export* kwa dola milioni moja tu. Sababu za msingi zinaeleweka, wafanyabiashara wakubwa wa mazao, wanachukua mazao yetu kwa bei ndogo kupeleka India. Leo korosho ya Lindi inapelekwa India, ufuta wa Lindi unapelekwa India na baadhi ya mazao mengine yote yanapelekwa India.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kule India ndio wanasafirisha mali hizo kupeleka Marekani kuonekana wao ndio ma-*export* wakubwa. Je, hawa wafanyabiashara wanaitakia mema Tanzania na wengine tunao humu humu ndani, wafanyabiashara wakubwa wa mazao. Kwa hali hii inabidi wao wawajibike kuhakikisha kuwa Tanzania nayo inafanya biashara kwa kupeleka *direct* Marekani na sisi tuingie katika soko kubwa la *AGOA* kuliko kuwa tunazunguka mpaka twende India kwa nini na kwa faida ya nani? Maana yake kuwa wao wanalihakikishia kuwa zao la korosho na mazao mengine ya ufuta yananunuliwa kwa bei ndogo na kumkandamiza mkulima. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo hii Lindi kuna mgogoro mkubwa wa ufuta, lakini sababu za msingi ni kuwa wananchi wanalalamika kuwa hawapati pesa za kutosha, lakini kutokana na mazao mchanganyiko kutokuwa na Bodi, inashindikana kuwasaidia wananchi wale kujiwezesha na kupata bei nzuri katika zao lao. Wananchi sasa hivi sio kama wa zamani, wanaona wenzao wa Mikoa mingine wanauza ufuta wao kwa bei

kubwa wakati wao wanauza kwa bei ndogo. Namwomba Waziri wa Kilimo haraka iwezekanavyo aanzishe Bodi ya Mazao Mchanganyiko kuondoa utata huu, itakuwa tayari kuwasimamia wakulima wa ufuta na kuweza kupata pesa za kutosha na kuweza nao kujikimu katika maisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia napenda kuchangia katika suala la madini. Nilihoji humu ndani na kuuliza swali, Mkoa wa Lindi kuna nini? Wakaniambia kuna dhahabu, *gypsum* na *germs* mbalimbali zinapatikana. Lakini cha kushangaza leo hii viwanda vyetu vya Simba *Cement* wanaagizia *gypsum* Pakistan na Muscat, je mchimbaji mdogomdogo atanufaika na nini kwa suala hili? Tubadilike Watanzania, tusiwe kila kitu kuchukua nje wakati malighafi tunazo humu humu ndani. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii hali itawasaidia wachimbaji wadogo wadogo wa Kilanjelanje, Makangaga, Mandawa, Mtandani na kadhalika kufaidika na madini yao waliyokuwa nayo na viwanda vilivyokuwepo hapa Tanzania katika uwekezaji huu na wao waweze kufaidika kimaisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunakuja katika suala la dhahabu, leo Nachingwea, Nditi, Ikungu, Kiegei wana dhahabu ya kutosha. Unakuja Ruangwa, Mandagala, Ndambilanji kote kuna dhahabu, lakini mpaka sasa hivi pamekuwa kimya, Wizara haiwasimamii wachimbaji wadogo wadogo wale kuhusu dhahabu yao ili baadaye waje wachimbaji wakubwa kuwatoa wale na wawe wageni katika migodi yao. Naomba Mheshimiwa Waziri mhusika kwa hili, aliangalie kwa huruma ili baadaye anipe majibu maana yake nataka nijue kwa nini wafanyabiashara wanakwenda wanachukua dhahabu ile kirahisi rahisi halafu wanaondoka lakini taratibu za kutosha hazijawekwa? Hivyo, naomba na hili aliangalie kwa jicho la huruma ili wale wananchi wa Ruangwa na sehemu zingine waweze kufaidika kwa hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kweli napenda kuunga mkono hoja kwa asilimia mia moja. (*Makofi*)

**MWENYEKITI**: Mheshimiwa tunakushukuru sana. napenda kuwataja wafuatao wajiandae, Mheshimiwa Shah, Mheshimiwa Mchungaji Dokta Getrude Rwakatare, Mheshimiwa Sanya, Mheshimiwa Richard Ndassa, Mheshimiwa Juma Sereweji, Mheshimiwa Magalle John Shibuda na Mheshimiwa Kange Ndege Lugola. Sasa tunaanza na Mheshimiwa Shah.

**MHE. ABDULKARIM E.H. SHAH:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutumia fursa hii kukushukuru kwa kunipa nafasi hii na kwanza kabisa naomba nimshukuru *Allah Subhanah Wataala* kwa kunijalia na kunipa uzima wa afya na hatimaye leo kuweza kusimama hapa na kuchangia kuhusu Wizara hii kubwa, Wizara inayoongozwa na Kiongozi wa Kiserikali hapa Bungeni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa, sina budi kutoa shukurani zangu za dhati kwa wananchi wa Kisiwa cha Mafia wote wa Chama cha Mapinduzi na wa vyama vyote waliojaliwa kunipa kura zao na kuweza kufika hapa kuwawakilisha, bado naamini

kwamba wana imani na mimi, lakini nawahakikishia kwamba imani waliokuwa nayo juu yangu, *Inshallah* nitajitahidi kwa kadiri ya uwezo wangu na uwezo wa Mwenyezi Mungu kuhakikisha kwamba mategemeo yao yanawafikia, yale ambayo wanayataka. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, naomba sana kwa sababu kuna hadithi moja katika dini ya Kiislamu inasema "*Maa lam yashkuru llah laa yashkuru nnasi, maa lam yashkuru nnasi laa yashkuru laah.* Mtu asiyeweza kumshukuru binaadamu mwenzake yeyote kwa jambo dogo basi hawezi hata kumshukuru Mwenyezi Mungu ambaye haonekani. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa maana hiyo, naomba sana kutumia fursa hii kuwashukuru sana Viongozi wangu wa Serikali, viongozi ambao waliojalia Mafia leo kutuweka katika kuhakikisha kwamba ile adha tuliyokuwa tunapigia kelele miaka yote, sasa inakaribia kutatulika kwa maana ya ujenzi wa Gati. Sina budi kutoa shukurani kubwa sana kwa Serikali na kuwatakia kila la heri wale walioasisi ujenzi huu wa gati, kwa maana Serikali ya Awamu ya Tatu ya Chama cha Mapinduzi na hatimaye ukamilisho katika Serikali hii ya Awamu ya Nne, nawashukuruni sana kwa pamoja na Wizara na Idara yote hasa Mamlaka ya Bandari.(*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sina budi tena kutoa shukurani kwa ujenzi wa *airport, phase one* ambao umekamilika na tunategemea kupata lami ambapo uwanja wetu utakuwa mzuri wa kisasa na naamini baada ya mwaka mmoja na nusu Mafia itakuwa kama Singapore, tunataka kuiita ni *mini* Singapore katika nchi yetu. Lakini pia sina budi kutoa shukurani zangu za dhati kabisa kupitia wananchi wa Mafia kuishukuru Serikali pamoja na Serikali ya Marekani kupitia mradi wao wa *MCA*. Pia mradi huu, naomba sana kutumia fursa hii kuwashukuru viongozi wangu wa Kiserikali wa Mkoa wa Pwani, Hajat Amina na secretarieti yote, lakini bila kumsahau *DC* ambaye tuliweza kukaa nae na kuongea na yule Mjumbe wa Bodi ya *MCA* na hatimaye akakubali kutoa pesa katika zile zilizotolewa na Mfuko huu, zaidi ya milioni mia saba na sisi Mafia tukaweza kupata kwa ajili ya ujenzi wa hicho kiwanja, lakini pia kwa kutumia pesa zetu kwa masharti ya kujenga barabara, hivi sasa tunategemea kuanza ujenzi wa barabara ya lami ya zaidi ya kilomita kumi na nne, tunasema Serikali ahsanteni sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia, naomba sana nimshukuru Waziri Ngeleja, yuko mbele yangu na yeye mwenyewe amenidhibitishia kwamba Mafia kutokana na tatizo kubwa la umeme tuliokuwa nalo, mwaka huu ndiyo mwisho. Mashine zile zilizokuwepo pale ambazo yeye mwenyewe anazifahamu kuwa ni mbovu ametuahidi kutuletea mashine nyingine za kuanzia, mashine zenye uwezo wa kuzalisha megawatt mbili katika Kisiwa hiki. Ni faraja kubwa na naomba nitumie fursa hii kuwashukuru sana Viongozi wetu hawa ambao wamejaliwa tuone kwamba Mafia sasa tuondokane na ule pweke ambao tumejitenga kijiografia tuliokuwa nao, nakushukuruni sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini juu ya mafanikio haya yote, ziko changamoto nyingi sana ambazo bado zinatukabili sisi wananchi wa Mafia. Mafia mazao yetu makuu ambayo yanatusaidia sisi katika kula kwetu na kufanya yetu kwa maana pamoja na kusomesha watoto wetu na kujiendeleza kijamii ni mazao mawili; la kwanza ni bahari na

la pili ni nazi. Sasa nazi, pamoja na korosho kidogo. Tunashukuru kwamba Serikali imeunda Bodi ya Mazao Mchanganyiko, naomba sana kwa kuwa siwezi kusema sana kwa kuwa Bodi hii bado ni mpya, lakini naomba sana wasione ujinga kwa hii Bodi ya Mazao Mchanganyiko kwenda kupitia nchi zile ambazo nazi ni zao ninaloleta tija katika nchi yao kwa maana linachangia hata pato la Taifa. Mafia tuna nazi nyingi sana na ukanda mzima kuanzia Tanga mpaka Mtwara tuna nazi nyingi sana kwa maana Bodi hii, kama atakuwepo mtu ndani yake maana yake tatizo ni *interest* za watu, inaweza ikaundwa hii Bodi, lakini kwa kuwa ametokea kwenye maeneo mengine basi atashughulika na mazao mengi. Naomba sana Mheshimiwa Waziri Mkuu atusikie, ndani ya Bodi hii lazima awepo mtu mwenye asili ya kulifahamu zao la nazi, ni zao ambalo linaweza likaleta tija kubwa sana kwa wananchi wa ukanda wa Pwani na maeneo mengine ambayo nazi zinapandwa na zinaleta tija. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nendeni Vietnam mkajionee jinsi wananchi wenye mashamba madogo madogo ambao wanafaidika na kutajirika kwa kupitia zao hili la nazi, naomba sana hili muweze kulichukua na si vibaya mkatuangalia na sisi Wabunge tunaotokea kwenye ukanda huu, mkapata mawazo yetu, hii Bodi nadhani imeundwa, mje kukaa na sisi tuwaelezeni yale ya kiuzoefu sio ya kisomi, ninyi wasomi, sisi tutatumia uzoefu, tukuelezeni ili muweze kujua ni vipi zao hili linaweza likachangia Taifa na kumsaidia mwananchi wa ukanda mzima hususan watu wa Mafia.(*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo la pili ni bahari, ukichukua kitabu hiki cha Mheshimiwa Waziri Mkuu, ukurasa wa 26 *paragraph* ya 42, inaelezea katika sekta hii ya uvuvi, ukiyasoma haya sina haja ya kuchukua muda utaona wenzetu wa Idara ya Uvuvi, mipango yao katika kuliendeleza zao hili, ni kuweka doria, kaza kamba, asiende mtu baharini ni balaa, maana yake hakuna chochote kitakachofanyika, halafu leo tunasema kwamba zao la uvuvi ndiyo linachangia asilimia 1.4 ya *GDP* hivyo litapanda vipi. Naomba sana Mheshimiwa Hamad Rashid alielezea hapa wakati akichangia ule Mpango wa Miaka Mitano pamoja na bajeti na baadhi ya Wabunge wengine wamelielezea. Alitoa mfano wa Maldives, nami nilikwenda na tulikuwa pamoja na Mheshimiwa Zakia Meghji. Tulikwenda na tukaona jinsi wenzetu walivyoweza kuhakikisha kwamba uvuvi ndiyo zao la pili baada ya utalii katika kuchangia pato lao la Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni nchi nyingi sana ambazo zinapata mapato yake makubwa kupitia sekta hii. Lakini mipango yetu katika nchi hii, katika ukanda hasa wa Pwani, mipango ya wenzetu wa Idara ya Uvuvi kila siku ni kupanga doria na kuwabana wavuvi na kuchoma moto nyavu. Sasa utaona, nyavu zenyewe zinatolewa kwa kupitia mradi wa *MACEMP* ambazo ni nyingi sana, pesa za Watanzania, wakopaji, zilichukuliwa, zikanunuliwa nyavu zikaenda, bila elimu wavuvi walewale ndiyo wakawa wanazitumia, wengine wanazizungukia tena Idara ya Uvuvi na kuweza kuzikamata na zinachomwa moto, hasara inakuwa ya nani? Naomba sana, mnisamehe wenzangu mnaotoka Bara, sisemi haya kwa roho mbaya au kwa jambo lolote lakini naongea kwa uchungu inaelekea *mind sets* za wenzetu wa Idara ya Uvuvi kwa kuwa wengi wao hawakutoka Pwani, hawaelewi matatizo ya watu wa Pwani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utaona hata katika kuboresha maendeleo ya mvuvi katika kitabu hiki, Mheshimiwa Waziri Mkuu amesema kwamba tutachimba mabwawa na kuweza kuendeleza ufugaji wa kambare na perege, hivi Mmafia gani, Mzanzibari gani, mtu wa Tanga gani, mtu wa Pwani gani Mkuranga, Rufiji, Pangani akale kambare. Hatutukani, lakini kambare kwetu kama vyura, hatuli madude yale. Nakuombeni sana mwangalie, naomba sana, kambare kwetu ni zao, ni samaki anayeliwa Bara, kwetu Pwani wako samaki wa aina nyingi. Tuitumie bahari yetu kwa faida ya nchi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusoma hotuba hii, nikampigia simu rafiki yangu mmoja nikamwambia ebwana eeh! Kuna mradi wa ufugaji wa perege akaniambia Mheshimiwa kama unataka kuja kutukanwa sasa Mafia walete, hatuelekei. Kwa hiyo, tunaomba sana, watu wa Idara ya Uvuvi, naleta mapendekezo kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu ikiwezekana, japokuwa wenzetu wanasema ukubwa wa Baraza la Mawaziri ni kubwa, lakini naomba kwa hili pia liangaliwe, atafutwe Naibu Waziri kumsaidia Mheshimiwa Waziri ambaye anaelewa masuala ya uvuvi, kwa sababu hebu angalia waliochaguliwa kipindi kile, lakini na kipindi hiki tuangalie wote ni watu ambao wanasimamia na kuufahamu zaidi ufugaji, si mambo ya uvuvi na ndiyo maana kila wanachoandikiwa na watendaji wao kazi yao kubana, hivi uharibifu wanaoharibu hawa watu wa Pwani na mashimo wanayoharibu hawa watu wa madini, wachimbaji wadogo wadogo nani anaharibu mazingira ya nchi yetu, nani anayeharibu ardhi ya nchi hii, nenda Tanga. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, wenzetu wakipiga kelele basi pale panakwenda na anapewa *licence* na wanamilikishwa na wanaweza na kusaidiwa, lakini leo mtu wa Pwani anabanwa sana. Naomba sana kupitia nafasi hii, kuiomba sana Serikali mumshauri na Mheshimiwa Rais ananisikia, naomba tusaidie kwa kumweka Naibu Waziri ambaye anafahamu masuala ya uvuvi, bila ya hivyo wavuvi wa Pwani ya bahari wataendelea kuwa maskini na wataendelea kubanwa na hakuna chochote tutakachofanya na bahari yetu itaendelea kuliwa na Mataifa ya nje. Tumekamata meli moja, meli ngapi ziko baharini? (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba tutumie mfano wa Maldives, achana na kuchukua meli za nje, hizo *licence* tunapata shilingi ngapi? Lakini leo tukiweza kuweka kiwanda hapa cha *fibre* tuwawezeshe wavuvi wetu, wananchi wetu kuweza kupata meli zile ili waweze kwenda kuvua katika bahari kuu tena kwa kutumia *trawler*, hatutumii nyavu tutaweza kufaidika, watu wataondokana na umaskini na nchi yetu itaweza kupata pato kubwa na zaidi ya asilimia tano au saba mpaka kumi uvuvi unaweza ukachangia katika pato la nchi hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine la mwisho, tumezungumza masuala ya umeme, naomba sana Waheshimiwa Wabunge wenzangu tunajua kila siku hii michango inaleta adha, lakini nina wazo, wataalam ninyi mtaliangalia, naomba sana kuwashawishi na wananchi kwamba, katika mpango mzima wa kusaidia upelekaji wa umeme vijijini tuweze kukubali na kuishawishi Serikali, mimi naishawishi Serikali ichangie katika kila *unit* moja ambayo sisi tuliojaliwa kupata umeme huu, basi tuchangie japo shilingi tatu tu

wala sio nyingi kwa kila *unit* moja pesa hizi ziweze kwenda kule ili ziweze kusaidia na wenzetu ambao hawajapata, waweze kufanikiwa kupata umeme huu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia, dada yangu Madabida amesema shilingi mia moja kwa kila lita, naomba Mheshimiwa shilingi tatu tu kwa kila lita kwa sababu kwa mwaka hapa tuna matumizi ya *petrol* yote kwa ujumla mafuta ya aina yote ni karibu *metric tone* 1.7 milioni ukijumlisha kwa shilingi tatu ni pesa nyingi sana. Tukiweza kukusanya pesa hizi kupitia simu zetu, shilingi tatu tu, wala sio nyingi kwa kila dakika sio sekunde, pesa hizi shilingi tisa au wakizitengeneza tunaweza tukapata *trillions of money*, tukaweza kuwasaidia wenzetu wa umeme vijijini, wakaweza kupata, lakini pia nusu ya pesa hizi, ziundiwe Mfuko Maalum ambao pia utaweza kuhakikiwa na pesa hizi ziweze kusaidia pia katika kuondoa adha kubwa waliokuwa nayo Watanzania, hasa wa vijijini katika kujenga vituo vya afya japo vya Tarafa kwa zile Wilaya ambazo hazina, tutaweza kusaidia. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini la mwisho ninausia: "Enyi ndugu zangu wa Mafia mliojaliwa kupata elimu hivi karibuni, nakuombeni sana Mafia kipindi kirefu hatujawahi kupata elimu kubwa, naomba sana kwa heshima zote, naomba tusome, tusichanganyike na makundi ambayo yanaweza yakatupotezea muda na sisi tukarejea kuchunga ng'ombe, tukarejea kuendelea kuwa wapara samaki na tukaendelea kuwa wapanda punda. Naomba sana tusome, wazazi wenu wameuza minazi yao, mifugo yao, wakaenda baharini wakanusurika kufa ili kukusomesha wewe. Naomba sana twende tukasome, tuachane na ushabiki mwingine ili tuweze kuja Mafia na sisi tuweze kutambulika, Kitaifa na hata Kimataifa."

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, nikushukuru sana, lakini la mwisho wazee wangu wote Waheshimiwa Wabunge nikushukuruni kwa imani yenu kubwa Wabunge wote wa vyama vyote kwa kunichagua kuendelea kuwa Kamishna katika Bunge hili la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Nakushukuruni sana na imani yenu ambayo mmenionesha, nitahakikisha kwamba yale mliyoyategemea mambo yenu yatakuwa mazuri. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja kwa asilimia mia na kuwatakia heri Wanaserikali wote chini ya Dokta Jakaya Mrisho Kikwete, watendaji hakikisheni yale tunayoyasema, yale yanayozungumzwa na Wabunge basi yatekelezwe, nakuombeni sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho kabisa, kuna suala la Waheshimiwa Madiwani, nakuombeni sana wale ni wasaidizi wetu, naomba sana Serikali hebu kilio hiki cha Wabunge kisikieni, wasaidieni walipwe mshahara, hivi viposhoposho kila siku, mbona sisi tunaingia mikataba ya miaka mitano na wao waingizwe, lakini si Madiwani pekee yake, wapeni na Wenyeviti wa Vijiji, Wenyeviti wa Vijiji wanahangaika, wale ndiyo wanatusaidia, tusijali vyama, wale wote ni msaada wa kwetu, wapeni mishahara au posho, asilimia tatu anazopewa tena mpaka wakusanye kitu fulani, zitawasaidia nini? Lakini leo wale wakipata posho zikaweza kuwasaidia, naamini watatusimamia vizuri na hatimaye shughuli zetu vijijini zitaweza kufanyika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana, naendelea kusema, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MHE. MCH. DKT. GETRUDE P. RWAKATARE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nikushukuru kwa kunipa nafasi hii ili niweze kuchangia hotuba ya Waziri Mkuu. Lakini awali ya yote naomba nimshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema, Mungu anayetupa afya, Mungu anayetupa ulinzi, unasafiri huku na kule anatulinda na mpaka sasa hivi ametuingiza Bungeni. Tunasema Mungu atukuzwe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni dua yangu na sala kwamba, kila Mbunge aweze kufunikwa na ulinzi wa Mungu ili tuweze kulitumia Taifa letu na wananchi wetu. Ni dua yangu na sala kwamba, umoja wetu na ushirikiano uweze kudumu. Ni dua yangu kwamba umoja uonekane na tuheshimiane kwa utukufu wa Bwana. Amina. *(Makofi)*

**WABUNGE:** Amina.

**MHE. MCH. DKT. GETRUDE P. RWAKATARE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nichukue nafasi hii kuishukuru Serikali ya CCM kwa mambo mengi mazuri ambayo wameyafanya, shule, vyuo, hospitali, zahanati na barabara nzuri, mnyonge mnyongeni lakini haki yake mpeni. Tunasema Serikali yetu ahsante kwa kazi nzuri, mwendelee kuwa imara, Mungu awabariki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sasa nichukue nafasi hii niweze kumshukuru Mheshimiwa Waziri Mkuu na Mawaziri na watendaji wote waliokuwa chini yake ili waweze kupata nafasi nzuri ya kuchangia hotuba hii nzuri ambayo wameileta kwetu, inakidhi mahitaji ya Watanzania na hata kwa maendeleo yetu kwa miaka ijayo. Kwa kweli ni hotuba nzuri. Hongeni sana na ahsanteni kwa kazi nzuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabla ya kuchangia, ningeomba nichukue nafasi hii niweze kuishukuru Serikali yetu na hasa Ofisi ya Waziri Mkuu na hasa kile Kitengo cha Maafa kwa kutukimbilia Wilaya ya Kilombero wakati tulipopata mafuriko mabaya sana, ambayo yameacha vijiji vitatu bila mahali pa kukaa wala chakula. Tunashukuru kwa mahindi, tani 239. Tungeyapata wapi, tunashukuru kwa sukari kilo 18,200 tungepata wapi. Tunashukuru kwa ajili ya chumvi mkatukumbuka kwa tani moja na nusu chumvi kila mtu aweze kupata chumvi na wao waweze kula vizuri. Maharage tani 30, lita za mafuta ya kupikia hamkutusahau na yenyewe lita 18,000. Kwa kweli jamani kitengo hiki tukiombee, kitengo hiki ni kizuri sana, kinatukimbilia katika shida, tulijisikia hakika na sisi tu watoto wa Tanzania. Kwa kweli mmefanya kazi nzuri sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, akinamama wa Kilombero wamenituma, useme tena uwaambie kabisa kwamba, bwana karibuni kwetu pia, mle samaki, mle mchele, mle pepeta, mle njugu, kwa kazi nzuri nzuri mliyoifanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, kwa kweli nitakuwa nimekosa fadhila kama sitaweza kushukuru Wizara ya Afya kwa kuweza kupandisha hadhi hospitali yetu ya Kilombero, St. Francis Ifakara na kuwa Hospitali ya Rufaa. Ilikuwa ni kero kubwa kwa akinamama hasa wakati wanapotaka kujifungua au wanapotaka kufanya mambo mbalimbali ambayo yameshindikana kwenye hospitali ndogo. Sasa hivi tunashukuru Rospitali ile ni ya Rufaa, inatufaa sisi na hata wenzetu wa Ulanga pia. Hospitali ile kwa hivi sasa imekuwa ni mkombozi, hata watu jirani wanaokaa pembezoni mwa Wilaya wanakuja pia kupata huduma mahali pale. Hili ni jambo la busara. Nataka kumtia moyo kaka yangu wa Afya ya kwamba, hakika anapokuwa msikivu na sisi tunajisikia vizuri. Anapokuwa anakaa chini na kutushauri na sisi tunafurahia aendelee na kazi nzuri anayoifanya. Wizara ile kwa kweli ni ya muhimu na kwa kweli tunaipongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatu, naomba pia nishukuru kwa niaba ya wananchi wa Kilombero na hasa akinamama kwa kuleta Chuo Kikuu cha Madaktari Bingwa pale Ifakara Mjini. Jambo hili siyo rahisi, mara nyingi vitu vizuri kama hivi vya Kimataifa vinakwenda kwenye miji mikubwa. Lakini mahali pale Ifakara kwenye Wilaya ya Kilombero kumekuwa na hospitali kubwa, hospitali ya Kimataifa, kuna Wazambia mahali pale wanasoma. Kuna Madaktari wa kutoka Rwanda, kuna wengine wanatoka Uganda, nimeona wengine kutoka Kenya na Watanzania. Kwa hiyo, kwa kweli ni mahali pazuri, wamechangamsha Wilaya ile, pamekuwa sasa na hadhi nyingine. Tunajisikia vizuri sana na hakika kabisa tunafarijika na tunasema Mungu awabariki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa naomba basi niende moja kwa moja kwenye kuchangia hoja hii. Kwanza kabisa, naomba nijikite na daraja la Mto Kilombero. Mheshimiwa Waziri Mkuu, Ofisi hii ya Waziri Mkuu naomba iliangalie suala hili kwa jicho la huruma. Jamani tuna tabu Kilombero. Jamani tuna shida, mtusaidie katika Ilani ya Uchaguzi 2005/2010, Rais aliahidi kwamba daraja lile litajengwa katika Ilani ya Uchaguzi tena 2010/2015, tukaahidiwa tena ya kwamba hakika daraja lile litajengwa. Lakini mpaka sasa bado, tunaomba chonde chonde kwa sababu mahali pale panaturudisha nyuma kimaendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa asilia ni kwamba Wilaya ya Kilombero na Wilaya ya Ulanga ilikuwa moja. Lakini tulipogawanya Wilaya, sasa unakuta wengine tuna ng'ambo ya Mto na wengine wanalima kwetu ng'ambo ya Mto. Sasa wakati wa kubeba mazao inakuwa ni shida. Kwa mfano, hivi karibuni Mawaziri wetu wawili walikwama kwa sababu kivuko kile kilishindwa kubeba watu. Ilikuwa ni sherehe kule Mahenge ya watoto kwa hivi watu wengi wakubwa wa dini na watu wakubwa wa Serikali walikwenda kule kushiriki. Lakini kumbuka Mawaziri wetu Mheshimiwa Celina Kombani, Waziri wetu Mheshimiwa Mponda, walikwama, walishindwa kurudi kwa sababu pantoni ilizidiwa, ikashindwa na tena kile kivuko ni kibovu, jamani mtuangalie, kama ni kibovu tusaidieni. Imeshatokea ajali watu wakafa, msingoje mpaka wakati wa hatari ndiyo mnatukimbilia. Jamani tukimbilieni sasa, tunahitaji msaada.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama daraja hili litajengwa basi uchumi wa Ulanga na Kilombero utaimarika. Kama daraja hili litajengwa hakika kabisa kutakuwa na wepesi wa watu kusafiri na hasa akinamama. Kwa hiyo, naomba kabisa hili jambo lifanyiwe

kazi mara moja kwa maana kila kitu kiko tayari, sasa tunangoja nini? Watu wa Ulanga, watu wa Kilombero wanataka daraja la Mto Kilombero, mtuangalie. Nina uhakika kabisa kilio hiki kimefika na kazi itafanywa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba tena niweze kuangalia tatizo la pili. Tatizo la pili, ni tatizo la mifugo. Jamani Kilombero tuna shida. Mifugo iliyopo inazidi wakazi wa Kilombero. Mifugo mnajua kwamba ni adui wa kilimo. Kwa hivi sisi asili yetu ni kilimo na uvuvi. Tuna mito 79, lakini kwa sasa hivi mito 39 yote imekauka tumebaki na mito 40. Tuna njaa kwa sababu ya mifugo, inakunywa maji yote. Mito inakauka, ng'ombe wako wengi kuliko watu, tusaidieni, muwe mnasikia vilio. Tuna mabwawa mazuri yenye samaki, yaani hivi ninavyosema kwa kweli sisi tulikuwa kwa asilia tuna kilimo mara mbili. Ukisha vuna mpunga mara ya kwanza, mpunga unachipua tena, halafu tunapanda mahindi, hiki kinaitwa kilimo cha chakula.

Mheshimiwa Mwenyekiti, siku hizi kilimo cha chakula hakuna kwa sababu ukipanda tu mahindi, ng'ombe wanakula. Kwa hiyo, hatuna kilimo cha mara ya pili, wala kuvuna mara mbili, mpunga hatuvuni tena. Kwa hiyo, tuna njaa, mahali ambapo kuna mito 79, mahali ambapo kuna mabwawa yasiyokuwa na hesabu, hatutakiwi kabisa kuhangaika. Kwa hiyo, tunaomba jamani ninyi mnajua kwamba, tumeshapiga kelele sana, hata Mheshimiwa Rais Mstaafu, Rais Mwinyi alisema jamani iondosheni mifugo kwa wakulima. Kwa maana hawa watu wasingekuwa wanachunga, wangekuwa labda wanafuga kwa maana ya kuwaweka ndani. Lakini sasa wanachunga na wanachunga kwenye mashamba. Sasa Kilombero imekuwa ni mahali pa kunenepeshea ng'ombe, wakati pale siyo *ranch,* pale wenyewe tupo, msifanye mahali pale *ranch* jamani. Sisi kwa kweli tunawapenda Wasukuma, tunawapenda Wamasai, wakija pale, njooni wenyewe lakini mifugo muiweke mbali. Mtusaidie hilo. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunapenda wageni lakini jamani tuhurumieni. Sasa hivi hatuwezi tena kula samaki anayeitwa mgundu. Tulikuwa na samaki mmoja mjongwa, samaki mnjuju, wote tumewasahau sasa hivi kwa sababu maji yamekauka kwenye mito na wale samaki hawapo. Zamani ukienda Kilombero mtoni ilikuwa ndiyo *beach* yetu, unakwenda kule unakaangiwa samaki, unakulaaa na watoto wako unarudi. Siku hizi ukienda samaki hamna, kwa sababu mito ile inayoleta maji Mto mkuu Kilombero yote imekauka. Sasa samaki watatoka wapi? Kwa hiyo, tunashindwa, tunaomba mtuangalie sana sana kwa jicho la huruma. Jamani msingoje mpaka tuuane. Watu wamechoka tena tatizo ni kwamba wale wenzetu ni warefu, wamepanda, wanene, sisi watu wa Wilaya ya Kilombero au Ulanga ni vijeba, halafu ni wembamba. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sasa hivi ninavyosema, kuna mtu mmoja amepigwa fimbo machoni, amekuwa kipofu. Hatuwezi kupigana nao kwa sababu sisi ni wadogo, wenzetu ni wakubwa, wanatuniga tu mara moja, basi mwenyewe unasalimu amri. Huwezi, kwa hiyo, inakuwa ni ngumu sana. Imekuwa ni ngumu kwa kweli mtuhurumie. Hata kama tukipeleka kesi Mahakamani. Wenzako wanachukua ng'ombe mmoja tu, analipa faini, sisi mpaka uuze mpunga wote uliolima kwa mwaka, sasa kweli inakubalika hiyo? Kwa kweli tunashindwa. Tulikuwa tunavua samaki, sasa hivi nyavu

tumeziweka juu, kwa sababu hakuna samaki wa kuvua. Sasa hivi wamepiga marufuku kwamba, miezi sita tuwaache samaki wazaliane, sasa sijui ng'ombe nao watasikia! Maana ng'ombe lazima watakunywa maji kwa hiyo, samaki watakufa, kitu ambacho kinaumiza. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaomba Ofisi ya Waziri Mkuu mtuangalie sana kwa jicho la huruma, kwa kweli tuna shida wenzenu. Hata kama wakisema haya marufuku inatolewa, unakuta angalau Wamasai wanatii, wanaondoka. Lakini hawa Wasukuma hawakubali, wanasema hawa ni watani wetu, sisi tutakaa hapa hapa. Kwa hiyo, tuna shida, wanakaa pale pale, wanasema tutabanana hapo hapo. Nyinyi ni watani wetu, inakuwa ni ngumu. Naomba mtuangalie, jamani mtuhurumie kwani tuna nia njema. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumzie tatizo la barabara. Mahali pale kila kitu ni cha muda, madaraja yetu ni ya muda, barabara zetu ni za muda, miundombinu mibaya, mibaya, mibaya. Walikuja Waheshimiwa mbalimbali kule kwa ajili ya kutusaidia na kuwapa pole wale waathirika wa mafuriko, wenyewe walijionea. Walishindwa, wengine walibebwa kwenye malori ya jeshi. Ilikuwa ni ngumu, hata kupeleka chakula, hatuna barabara kabisa, kabisa, kabisa. Barabara zilizopo ni za Halmashauri ambazo ni za changarawe. Sasa barabara za changarawe yaani sumu yake ni mvua. Mvua ikija changarawe zote zinasombwa, sasa hapa si umepoteza hela bure. Kwa hiyo, unakuta kila mwaka wanaweka changarawe, mvua ikija inasomba, hela zimekwenda. Hicho ni kitu ambacho hatukipendi.

**MWENYEKITI:** Nakushukuru sana muda umekwisha.

**MHE. MCH. DKT. GETRUDE P. RWAKATARE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MHE. IBRAHIM MOHAMED SANYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi hii. Kwanza kwa heshima zote kabisa nina furaha kubwa, leo natangaza katika Bunge hili kutembelewa kwa *suprise* yaani *invension in the camp* na mke wangu mpenzi Bi. Sharifa Ali Abdulatwif. Narudi hoteli namkuta *reception* na *bag* lake, jiandaeni wenzangu. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, uwezo wangu na kazi nzuri ninayoifanya katika Bunge hili la Jamhuri ya Muungano unachangiwa sehemu kubwa na mke wangu mpenzi Sharifa Ali Abdulatwif pamoja na wapiga kura wangu wote wa Jimbo la Mji Mkongwe na sitawaangusha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Taifa lolote duniani hupimwa kwa maendeleo yake na siyo kwa maneno yake. Tukiwa na tabia ya kuanza kuusahau uzalendo wa nchi hii, tujue kuna mamilioni ya watu walikaa foleni kutuchagua sisi kuja kuwatetea wao, tuwaondoshee dhiki zao walizonazo za kila siku. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Abraham Lincon alisema: "*The house divided can not stand"*. Ina maana pana sana hii kama utaifanyia *analysis*. Ninachotaka kusema hapa ni kwamba, sisi Wapinzani nguvu zetu, nidhamu zetu tuzielekeze katika kujenga hoja zitakazowafanya wananchi wakaamua kuwachoka hawa CCM, tukakaa sisi madarakani. Kama CCM wanasema wanatoa vyandarua vya mbu sisi tuseme tutaua mazalia ya mbu, wao watapima baadaye yupi anafaa kuwaongoza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, unapojiona huna meno kibogoyo, jaribu sana usicheke mbele ya wenye meno. Tafuta watoto wadogo waliokuwa hawana meno wanaweza wakakuweka rika yao wakasema huyu ni mtoto mwenzetu. Msitubeze Wanzibari kwa kuungana kuunda JNU, mtaona matokeo yake na sasa hivi tuko pale *we are committed to the national development. (Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Muungano upo na utadumu. Kasoro za Muungano na matatizo ya Muungano dawa yake ipo tutakaporekebisha Katiba ya Jamhuri ya Muungano na ya Zanzibar kuwa na Muungano madhubuti utakaoleta faida kwa pande zote mbili za Tanzania. Kama kuna mtu au kikundi kwamba walitegemea Zanzibar ibakie kuwa *the land of broken dreams* yamekwisha. Zanzibar tuko kitu kimoja na tutaijenga Zanzibar na itakuwa faida kwa Zanzibar na kwa Tanzania nzima. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Taifa makini lazima likope. Tanzania tusijidanganye kwa kusema tuna madeni, hatukopi tena. Tuwe na sifa nzuri sana ya kukopa, lakini tuwe na nidhamu ya kulipa. Wizara ya Ulinzi juzi ilichukua mkopo wa dola milioni 40 kutoka India wakanunua matrekta kuyaleta Tanzania. Nawapa hongera kwa hilo. Haya ndiyo mambo ya kuongea na wali-*negotiate* vizuri sana baina ya Serikali yetu kwa dhamana ya Benki Kuu na Wizara ya Fedha kwamba mkopo huo ulipwe kwa muda wa miaka *20, just imagine* kwa *1.5 percent* na tukapata *grace period* ya miaka mitano yaani miaka mitano ya mwanzo kabisa hatuulizwi na India mpaka miaka 15 inayokuja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ina maana wakati wa Kikwete, Mheshimiwa Rais atamaliza muda wake na Rais atakayechukua madaraka mengine atamaliza muda wake wa vipindi viwili miaka kumi na bado hatujamaliza mkopo huo kwa sababu ni *soft loan.* Wahindi wana fedha nyingi sana, Wachina wana fedha nyingi sana, lakini wanataka watu madhubuti, watu wakweli, Tanzania tumechukua mkopo, sasa matrekta yale yapelekwe katika *slogan* yetu ya Kilimo Kwanza ili tuondokane na njaa na tusafirishe bidhaa kupeleka nchi za nje. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuwape magereza, tuwape *SACCOS*, vikundi mbalimbali, Wabunge na tukope ili tuweze kuzalisha zaidi, tuweke heshima ya Kilimo Kwanza, tusije tukazalisha tukashindwa kusafirisha, tukashindwa kutengeneza bidhaa! Badala ya kuwa Kilimo Kwanza, ikaja ikabadilika ikawa ni Kilio Kwanza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, juzi nimepata taarifa kwa *Tanzania Cotton Board, Managing Director* wake anasema kwamba katika msimu huu wa pamba anategemea kuvuna tani 250,000 *well and good. And the price* imekwenda juu mara mbili kutoka shilingi 600/= mpaka shilingi 1,100/=. Lakini je, tumejiandaaje katika uzalishaji wa pamba hii? Ni kweli mara zote tusafirishe pamba ghafi? Hapana! Kilo tatu za pamba,

unaweza ukazalisha shati moja, sasa kitu ninachotaka kui-*advise* Serikali, baada ya kukopa hizo shilingi 40,000,000/= tukapata matrekta kwa ajili ya kuzalisha, sasa na tujiandae kukopa kiwanda cha nguo kutoka India ambacho gharama yake ni kuanzia dola 60,000,000 mpaka dola 70,000,000. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kwa nini nikasema hivyo? Mwanza, Kagera, Shinyanga na Mara, pamba yao kama tutawawekea kiwanda pale, tutaongeza thamani. Hatutasafirisha tena 80% ya pamba, badala yake tutatengeneza nguo, wanajeshi wetu hao hao nguo zao hawataagizia tena kutoka China wala Egypt, watatengenezewa kutoka katika hicho kiwanda, polisi wetu watatengenezewa *uniform* katika hicho kiwanda, ma-*bed sheet* yetu ya mahospitali ya Tanzania yatatengenezwa katika hicho kiwanda; tutaongeza thamani, watapata pesa zaidi wale wakulima na pamba yetu itabakia ndani kwa kutengenezea bidhaa na tukiwa makini tunaweza tukateka wataalamu kutoka ama Thailand, India na Bangladesh, tukatengeneza mashati, suruali, *t-shirts,* tukaingia katika soko la *AGOA* na tukaongeza thamani, haya ndio ya kuyafanya hapa Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tusikae tukasema kwamba sisi tulumbane kwa maneno wakati wananchi wanateseka. Tukumbuke Watanzania wa nchi hii wa vijijini, wanazaliwa wengine mpaka wanakufa *audhubilah mindhalika*, hawana hata kiatu cha kuvaa! Kwa nini tusiwajengee mazingira wakapata viwanda vya kutengenezewa nguo? Wakapata bidhaa zao kwa wakati? Wakapata rasilimali yao kutumika vizuri kwa wananchi wa Tanzania? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nitakupeni mfano mmoja mdogo tu; tunategemea kununua pamba kwa shilingi bilioni 275 pesa za Serikali. Leo ukiongeza 10% tu katika utenegezaji mzima wa nguo, nyuzi na vitambaa una shilingi bilioni 27.5 inawezekana ni nusu ya Bajeti ya Wizara moja katika Jamhuri ya Muungano.

Mimi nasema hivi na ninashauri kwamba sisi Watanzania kwanza tuwe kitu kimoja, tuwe na uzalendo. Tukiwa ndani humu, tujue tumo ndani kwa fedha za walipa kodi, kuwatumikia walipa kodi waelewe tunawatetea nini katika nchi hii; hakuna atakayekuja humu akasema huyu *CUF*, huyu CCM, huyu CHADEMA. Atakachokisema, huyu ni *Honorable Member of Parliament. (Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka 1984 wakati Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed, alipokuwa Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani, alikwenda kwa Baba wa Taifa Mwalimu Nyerere, akamwambia nipe matrekta 100 uone nitafanya nini na nikishindwa nitajiuzulu; alifanya nini Mheshimiwa Hamad? Hajui kama hata mimi ninaelewa, ninafanya *research* zangu mwenyewe; alianzisha *irrigation scheme* Bagamoyo, akazalisha mchele tena mitaro ya kumwagilia iliichimbwa na vijana wetu wa JKT. Songwe pale palikuwa na heka 2,000, Boko muhogo ulizagaa Kariakoo mpaka wale wakulima wa muhogo wadogo wadogo wakaanza kupiga kelele kutokana na bei kushuka na kama ni uongo, mtafuteni Kamanda Dilunga, atawapa taarifa za muhogo aliokuwa anazalisha yeye. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kingolwira wakitoa maziwa yakitosheleza kwa kambi na mengine kuuzwa ya ziada, kulikuwa na *surplus. Lake Victoria, Lake Tanganyika* Kigoma, alikuwa anazalisha dagaa wakazagaa nchi nzima, *started with only 100 tractors!* Mpaka Baba wa Taifa Mwalimu Nyerere wakati wa Sokoine akamwambia *if I get only five Hamad's, this country will move.* Sasa matrekta yamekuja haya, tuyatumie, tena nasikia ni bei rahisi kuliko yaliyokuwepo katika soko. Wakopeshwe watu, yapelekwe JKT, wapewe magereza wana ardhi chungu nzima, ili tuweze kuzalisha na tuwakomboe wananchi wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo akinamama ndio wakulima wakubwa wa nchi hii. Unapokwenda vijijini wao ndio wakulima, waoteshe, wapalilie, wavune na wauze barabarani na chakula watupikie wao! Na fadhila zetu tukitoka kwenye vilabu vya pombe, tuwapige hadi kuwaua! Ni wanawake, wapewe hii mikopo! Mimi nasema nchi hii kama inataka kwenda viongozi wengi wawe wanawake! Viongozi wengi wajikite kuwatumikia wanawake kwa sababu wanawake ndio wazalishaji wakubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho lakini sio kwa umuhimu, ninampongeza JK, Mheshimiwa Kikwete. Mheshimiwa Kikwete, ni mvumilivu sana! Amevumilia mengi na hatutamjua wema wake na uzuri wake, lakini hapo atakapomaliza muda ndio tutakuja kumkumbuka Kikwete, alikuwa ni wa aina gani. Tusianzishe malumbano ya kejeli na kuondosha nidhamu, sisi ni viongozi wa nchi hii, watu wanatutegemea sisi! Sisi tuna akili timamu, tujadiline mambo ambayo yataondosha dhiki za Watanzania katika nchi hii! Kiongozi gani anayemtakia raia wake mabaya? Na kila siku tukisema sungura mdogo, hatageuka! Sasa tumgeuze mwakani tukirejea hapa, badala ya kuwa na sungura, tuwe na kondoo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. HAJI JUMA SEREWEJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru kwa kuniruhusu kuchangia hotuba hii. Kabla sijaendelea kuchangia hotuba hii, ninaiunga mkono asilimia mia kwa mia pamoja na wananchi wangu wa Jimbo la Mwanakwerekwe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaanza kuchangia Muungano. Muungano tunaupenda sana na kwanza tunaupenda kwa sababu una historia nzuri, tumeonesha mfano mzuri katika nchi zetu za Kiafrika, lakini tutazidi kuupenda Muungano huu ikiwa kasoro ndogo ndogo zote zitaondoshwa na sioni sababu ya kuundwa Kamati ambayo mpaka leo kero hizo hazijaondoka. Sasa ningependa ili Muungano huu uende vizuri zaidi, kero hizo ziondoke haraka iwezekanavyo kabla hata hii Katiba haijafika. Wakati Katiba inazinduliwa kero zote ziwe zimemalizika, ili wale waliokuwa wako upande wa mfumo wa Serikali tatu tuwavute wawe na hamu waje katika mfumo wa Serikali mbili ambao ndio Sera ya Chama cha Mapinduzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuna sekta zetu au Wizara za Muungano. Lakini Wizara zile zote zijue wazi kwamba Wazanzibari wana haki yao ya peke yao. Haki ya mwanzo kabisa, kama kuna sehemu ya kazi, kunatakiwa wafanyakazi, lazima Zanzibar wawe na

fungu lao na liheshimike. Kwa upande wa Jeshi la Polisi, Jeshi la Ulinzi, kama wanatakiwa wanajeshi 50 au polisi 50 kutoka Zanzibar, lazima tuhakikishe fungu lote lile la watu 50, wametoka Zanzibar na wala sioni sababu kwamba wanajeshi wanakuja kupimwa na wanamaliza huku Tanzania Bara kila kitu wakati pana hospitali nzuri tu ya Bububu. Hata kama hakuna kuchakachuliwa, tutasema kumepita kuchakachuliwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili tunapendekeza baada ya wafanyakazi wote wa sekta za Muungano wakishastaafu wasitaabishwe kupata haki yao. Lakini utakuta wanataabishwa mpaka tunawasidia sisi Wabunge! Wanakuja Bara na kurudi mpaka wanaishiwa na nauli! Sasa yale yote nasema ni kero, ambazo sio vizuri wakati Muungano tunaupenda na Muungano tunataka uendelee na utaendelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hivi naingia upande wa Madiwani. Nadhani Madiwani ni wamojawapo ambao tunakwenda sambamba kwenye Uchaguzi Mkuu, lakini baada ya kumaliza Uchaguzi Mkuu Madiwani tunawasahau! Kwa hivyo, tunapendekeza na wao wapate mshahara, Madiwani wa Zanzibar pamoja na wa Tanzania Bara, pamoja na Wenyeviti wa Serikali za Mitaa na Wenyeviti wa Vijiji. Ninaipongeza Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa sababu kule Wenyeviti wa Serikali za Mitaa wanaitwa Masheha, Masheha wote wanalipwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nakuja upande wa nishati na hasa nitazungumzia umeme. Kwanza lazima niishukuru Serikali ya Jamhuri ya Muungano kwa kuweza kueneza umeme sehemu nyingi tu, vijijini, Wilaya na sehemu chungu nzima. Lakini tumekabiliwa na mgao, mgao ambao hatuwezi kuuepuka. Kwa hivyo, mgao ule unazidi kuathiri wakati wananchi wa sehemu fulani wameanza kuanzia saa 12.00 mpaka saa 12.00 jioni hawakupata umeme! Lakini ikifika saa 12.00 wanapata umeme kwa muda wa robo sasa, unazimwa tena pengine mpaka saa 12.00 kesho jioni. Ukiuliza kuna sababu gani, unaambiwa *transformer* mbovu! Na kumbe *transformer* ile ina matengenezo ya dakika tano tu au tatu, *fuse* zina matatizo. Na ushahidi tosha upo katika eneo la Mtoni Mtongani mpaka njia iliyoelekea Temeke, uondoke pale pande zote mbili matatizo hayo huwezi kukaa siku tatu hayajatokezea!

Sasa wananchi badala ya kupata saa 12 za mgao, wanapata saa 36, jambo ambalo ni la usumbufu, kwa hiyo, hili nalo naomba lirekebishwe. Wafanyakazi wa umeme waende kama wafanyakazi wa hospitali, waende kama wafanyakazi wa Jeshi la Polisi, kuwe na watu wa *stand by* kutafuta matatizo kama haya na wayatatue haraka sana ili wananchi wasizidi kuibughudhi Serikali yetu ya Chama cha Mapinduzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa hivi kidogo nitaingia kwa upande wa hotuba ya Kambi ya Upinzani. Nadhani Bunge ni Wabunge na Wabunge ni Bunge. Jumba hili kama halina Wabunge, utaitwa Ukumbi au Jumba la Wabunge. Lakini Wabunge wapo katika mihimili mitatu ya dola, Rais, Mahakama pamoja na Bunge, sasa mimi ukiniambia kwamba au ukituambia kwamba Wabunge waende katika *economy class,* halafu hawa Mawaziri upendekeze waende *business class,* mimi nitakushangaa! Kwa sababu Mbunge yeyote kama chama chake kinaongoza, yeye anakaa kama Waziri mtarajiwa na Katiba yetu ya

Jamhuri ya Muungano huwezi kuwa Waziri mpaka uwe Mbunge; sasa wewe kwa nini unajiteremsha katika mihimili mitatu ya dola, unasema kwamba uende katika *economy class? (Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hii ninai-*challenge* moja kwa moja, kwanza hakufuata Katiba yetu ya Jamhuri ya Muungano. Lakini la pili, kajiteremsha hadhi yeye mwenyewe, la tatu wananchi wetu wa Tanzania wanatuthamini. La nne, nasema vizuri tu sina lugha mbaya wala sikukusudia vibaya, hata viumbe ambao wale tulioambiwa tuwatawale wana viongozi wao na wanawaheshimu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama utaenda kuuchoma mzinga wa nyuki, yule *queen* humpati. Anakuwa *escorted* na nyuki wenzake mpaka anafika mahali maalum, wanamlinda. Nyuki mmoja tu akifanya matatizo, anakwenda maktaba, sembuse sisi Wabunge wa Jamhuri ya Muungano ambao tumechaguliwa! Leo tunajiteremsha hadhi wenyewe! Kwa nini? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ulimwengu ulipoundwa kulikuwa hakuna silaha, lakini baada ya watu kuonekana matata sana zinakwekwa silaha, lakini silaha hizo zimewekwa mafungu mawili mpaka matatu. Kuna sehemu moja, tena nawaambia wananchi wanisikie, kuna sehemu moja ni wale ambao wanafanya fujo mle mle nchini mwao nao ni raia. Kuna sehemu nyingine ya nchi kama wanakuja kutaka kuichukua nchi kama Idd Amin, wale hatuendi na gari la maji machafu yanayowasha, tunatafuta mizinga mizito mpaka tukishaingia ndio wanatumika askari wa miguu wanaotumia *Semi Automatic Rifles.* Sasa ninalolisema, mimi nitawashangaa sana jeshi la polisi kama wataondoka hapa kwenda kuwinda tembo, sambamba na nini sijui, wakachukua gari la maji machafu! Lakini nitawashangaa sana polisi kama wataondoka hapa kwenda kuwinda tembo kwa mabomu ya machozi! Yale yote wananchi nawaeleza yameundwa rasmi kwa wale ambao watataka kuhatarisha amani ya nchi, wakati wowote na mahali popote na polisi ni lazima watumie. *(Makofi)*

Sasa wewe ukisema kwamba polisi wanaua hovyo bila kutoa sababu hata wananchi wenyewe wanashangaa kwa sababu makundi mengi wanakaa hawajapingwa, sehemu nyingi tu zimo hawajapita wakamwaga maji machafu lakini yale yanafanywa baada kuona kwamba hapana amani na utulivu na amani haipatikani kama pana fujo lazima utumie ncha ya upanga. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hivyo nawatahadharisha wananchi ambao wale wanaorubuniwa kwa kufanya maandamano, kwa kuleta fujo, nawatahadharisha watumie akili tuitetee amani yetu iliyopo daima dumu ambayo nchi zote zinatuonea wivu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakuja upande wa Vyuo Vikuu, mimi napendekeza kuanzia sasa Serikali itoe tamko Vyuo Vikuu wakienda wanafunzi kuanzia sekondari, *primary,* Vyuo Vikuu na sehemu zote za elimu uende pale kwa kusoma, mambo ya siasa yamalizike wakishakuwa kule tena watafute nyanja zao za siasa kama vile majeshi yetu, polisi na jeshi la polisi na la ulinzi lakini kama tutakwenda hivi nchi yetu itawekwa

pabaya na itawekwa pabaya kwa sababu vijana wetu hawajui historia na wanahadaika upesi. Na wapo watu wanaotaka kuleta umaarufu wajulikane kwa fujo ndogo ndogo, kwa hivyo, mimi napendekeza kuanzia sasa litoke tamko Vyuo Vikuu na sehemu zote za elimu, madarasani kusiendelee na mambo ya kisiasa ili kuleta amani na utulivu katika nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho kabisa nawashukuru sana wanachama wangu wa Chama cha Mapinduzi na wananchi wa Chama cha Mapinduzi wa Jimbo la Mwanakwerekwe kwa kunileta hapa na kama mtihani basi wamefaulu kwa sababu uchaguzi wangu haukufanyika tarehe 30 Oktoba, umefanyika tarehe 14 Novemba, lakini wana CCM jimbo la Mwanakwerekwe wakasema hapa lazima tutabanana mpaka Sereweji aende kwenye mjengo hongera sana. Kwa hiyo, nawahakikishia wananchi wangu wa jimbo la Mwanakwerekwe sitowaangusha kama walivyokuwa hawakukiangusha Chama cha Mapinduzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya hayo kwa heshima na taadhima naunga mkono hoja hii mia kwa mia, ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. JOHN S. MAGALLE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kupata fursa hii na mimi niweze kuchangia hoja ya hotuba Mheshimiwa Waziri Mkuu ambayo ipo mbele yetu sote. Mchango wangu utakuwa mtambuka kwa kutambua kama Mheshimiwa Waziri Mkuu ndiyo msimamizi Mkuu wa Serikali, mshauri mkuu na ndiyo mwelekezi wa Wizara zote wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kabla sijasema hilo la mchango wangu napenda vilevile nitumie nafasi hii kutoa angalizo lifuatalo kutofautiana kifikra siyo usaliti bali ni utafutaji na upekuzi na udadisi wa hoja iliyopo mbele yako hatimaye ukaamua kutofautiana nayo kwa nguvu za hoja, kwa hiyo, nimeona hilo niliseme kwa sababu yale nitakayoyasema huenda yasiwafurahishe baadhi ya masikio ya binadamu, kwa sababu kila binadamu ana viwango vyake vya uelewa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kila binadamu ana viwango vyake vya uelewa vya busara na hekima, subira, utulivu kutegemeana na ukomavu wa fikra, kutegemeana na makusanyo ya maono mbalimbali. Kwa hiyo, huenda nitakayoyasema kama wewe hujapata makusanyo ya maono hayo niko radhi kuja kushauriana na wewe nikusaidie kukutanabaisha hayo niliyokusudia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo sasa napenda kuishukuru familia yangu, kumshukuru Mama Sakina Shibuda, wanangu wote walioshiriki katika kampeni, Watanzania wote wa Maswa walioamua na kusema kwamba Maswa ina wenyewe na vilevile naomba nitumie nafasi hii adhimu kumshukuru Mwenyekiti wa chama cha CHADEMA, Mheshimiwa Freeman Mbowe kwa kukubali na kuhimiza na kushauri na kutambulisha ubora wangu hatimaye CHADEMA wakakubali niwe mgombea wa Ubunge katika jimbo la Maswa Magharibi, hivyo nakushukuru sana Mheshimiwa Mbowe na nawashukuru viongozi wote wa Kitaifa wa CHADEMA waliopitisha jina langu mkoa na wilaya. *(Makofi)*

Vilevile napenda kutumia nafasi hii kuwapa pole wananchi wa Shinyanga kwa kifo cha Mwenyekiti wetu Mheshimiwa Philip Shelembi Magadula aliyefariki na akatutoka. Nawaambia wananchi wa Shinyanga kuweni na subira kwani chelewa ufike ndiyo wazo lenye hekima na aliye na subira yupo na Mwenyezi Mungu hayo ya Shinyanga yanapikwa na yanawekwa siku moja yatatengwa mezani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukweli una tabia ya kuudhi masikio ya mtu dhurumati, lakini napenda kusema ya kwamba nashukuru sana sana juhudi za watu wote walioshirikiana nami kwa hali na mali. Mimi ndiyo Mbunge pekee katika Tanzania niliyefanya kampeni kwa siku nne na harusi ikajibu, nawashukuru sana wananchi wa Maswa kwa heshima waliyonipa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyosema usione chang'ara kina wenyewe, naendelea tena kusema nawashukuru sana timu ya kampeni iliyokuwa katika jimbo la Maswa na nawapa pole vijana kwa heka heka na matikisiko waliyopata na baadhi yao wakawa katika masuala ya kuwa gerezani, lakini namshukuru Mwenyezi Mungu amewanusuru. Kila linalomfika binadamu ni utashi wa Mwenyezi Mungu huenda kila linalokutokea unaweza ukachukia lakini Mungu ana jambo lake. *(Makofi)*

Vilevile napenda nitumie fursa hii kusema ya kwamba kuna Wabunge wa aina mbili, kuna Wabunge ambao ni maslahi ya jamii kama Shibuda na kuna Wabunge ambao ni maslahi binafsi hata kupigiwa simu wakipigiwa hawapokei, lakini hayo nitayafafanua baadaye. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutumia nafasi hii kusema kwamba Taifa letu hivi sasa lipo katika hali ya heka heka ya masuala ya uwajibikaji, vilevile napenda kusema ya kwamba nitatumia nafasi hii kumuomba Mheshimiwa Waziri Mkuu awe mshenga wetu ili aweze kutupelekea salamu kwa Mheshimiwa Rais kwamba Wabunge wa Bunge la Tanzania wanahitaji huduma pana ili tuweze kutekeleza majukumu yetu badala ya kukimbia majimbo yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kutumia nafasi hii kusema ya kwamba Mheshimiwa Waziri pamoja na Mheshimiwa Rais ukiwaona Wabunge asilimia 60 hawakurudi humu ndani ya jengo basi kuna sababu na hakuna Mbunge ambaye anakimbia wananchi wake asiwahudumie, lakini kuna sababu ambayo inasababisha kwamba Wabunge wakimbie. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kuna jambo moja ambalo nitapenda sana Mheshimiwa Waziri Mkuu alitambue hivi sasa panataka kuzuka janga la kuondoka uzalendo, uaminifu na utiifu wa kutumikia jamii na ndiyo maana panazaliwa ufisadi kwa sababu ukiangalia wastaafu utakuta ya kwamba wana maisha magumu sana na walikuwa waaminifu na watiifu, ukikuta mtu ambaye alikuwa fisadi nyumbani kwao kunang'ara kwa hiyo, anashawishi wengine waondokane na uzalendo na utiifu.

Kwa hiyo, haya ni lazima tuyafanyie kazi na kama alivyosema Mheshimiwa Edward Lowassa tuwe na maamuzi magumu na tusitake kupunguza hayo majambo kwa sababu ya maneno ya utamu ambayo siyo ya kweli. Vijana wapo katika msako wa maisha bora, wazee wapo katika msako wa virutubisho vya kung'ara, uchakavu wa maisha ya kustaafu hayo yote yatapatikana vipi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapenda kusema hayo kwa sababu kuna mambo mengi sana mbayo tusipokuwa hata na lugha sanifu tunaweza tukajikuta ya kwamba tunatumia maneno hatarishi ya kupotosha mantiki ya dhamira. Nitagusia maneno ya Kiswahili ambayo kwa kweli hata katika Bunge letu yanadhihaki na tunajikuta kwamba hatuendi sawasawa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo sasa najikitika katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu nichangie yafuatayo; kwanza matazamio ya Tanzania endelevu ya siku ya usoni, matazamio hayo yatajengwa na tabia na desturi za sisi viongozi ambao tuna deni la kuacha urithi endelevu kwa maslahi ya Taifa letu na urithi endelevu upatikane kwa kuelezana ukweli ambao hauna porojo bali unakita katika masuala endelevu kwa faida ya kesho. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, uongozi wa kujenga mbegu za makuzo bora, yenye kuendeleza umoja na mshikamano na upendo, amani na utulivu wa Taifa hili yatazaliwa na uwazi na ukweli wa sisi wanasiasa pamoja na Serikali kuamini ya kwamba tunapenda na tuna mshikamano na kuamini ya kwamba maana ya mfumo wa vyama vingi siyo kuibua mazalia ya mafarakano, tuepuke mambo ya kufikirika kuziba uovu wa mtu mmoja, tuepuke kufikirika kwamba mtu ukisema ya kwamba *DC* fulani mbovu maana yake unadhalilisha Serikali, udhaifu wa Shehe siyo udhaifu wa Msahafu, udhaifu wa Askofu siyo udhaifu wa Biblia.

Kwa hiyo, tuepukane na dhana potofu na hii ipo sana ya kufunika funika maovu kwa kusingizia kwamba kiongozi fulani akiambiwa ni dhaifu unamuumbua, unamdhalilisha. CCM chama tawala unadhalilisha Serikali *now is totally wrong,* nashukuru Mwenyezi Mungu nimekulia katika hicho chama chetu. *(Makofi)*

Tatu, uvivu wa kufikiri utaondolewa na changamoto za mashindanno ya mfumo wa vyama vingi na ndiyo maana hata Baba wa Taifa alisema, tuhakikishe ya kwamba tunaruhusu mfumo wa vyama vingi la sivyo patazaliwa kubweteka na kubweteka kupo. Naomba Waziri Mkuu asaidie kuwaambia Wakuu wa Mikoa na Wakuu wa Wilaya ya kwamba mtu asiye CCM asikilizwe kama ana nguvu za hoja kwa maslahi ya Taifa, cheo kisiwe kiziwi wa kusikiliza ukweli ambao siyo wa mtu wa kabila moja au dini moja, cheo chochote, tukifikia hatua ya kwamba hivi sasa hatuthaminiani kwa sababu mtu fulani ni wa upinzani tutakuja kubaguana kwenye dini, tutakuja kubaguana katika ukabila, nani kasema huyo siyo kabila letu, tunakwenda wapi, umri wangu ni wa kutoa nasaha na kukosoa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nne, tabia ya nchi ya vizazi vya kesho je, vitarithi tabia gani, tunavijengea taswira gani vizazi vya kesho, tabia ya nchi ya leo hivi sasa ninasikitika na nashukuru Mwenyezi Mungu nilipokuwa CCM mengi sikuyajua ya

upinzani na ninaomba mnipokee ndugu zangu Waheshimiwa Wabunge kwa sababu ya kujenga uendelevu makini, ninawajua Wabunge wote ni jasiri, na haya ninayoyasema ni kweli mmenilea wenyewe ndani ya CCM, mmenikuza wenyewe leo niko katika mfumo wa vyama vingi kwa kujaribu kuona ni nini maana ya mfumo wa vyama vingi Tanzania, nimejifunza kumbe ukiwa upinzani wewe si mwenzetu, si ndugu yetu, *DC* akionekana anazungumza na mtu wa upinzani anaanza kuambiwa huyo si mwenzetu, Kamati ya siasa inataka kumjadili imfukuze, *OCD* akikutana na mtu wa upinzani anaeleza ukweli akiamua kusema huyu anasema ukweli *OCD* ataambiwa si mwenzetu afukuzwe, tunakwenda wapi? Tunajenga urithi gani? Kama ni hivyo tufute mfumo wa vyama vingi, turudi kwenye mfumo wa chama kimoja, hakuna sababu ya kuendelea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo Katiba ya nchi Ibara ya 8 na 9 inazungumzia kuhusu rasilimali za Tanzania ziwe kwa faida ya maslahi ya Tanzania na maendeleo ya Taifa letu. Je, Serikali ya CCM ambayo ina makatazo pia ya Katiba ya CCM inayohimiza rasilimali za Tanzania zitumike kwa faida ya Tanzania je, leo naomba kuwauliza pana ukombozi gani wa zao la dhahabu katika mkoa wa Mwanza, Shinyanga, *Tanzanite* na samaki pana ukombozi gani dhidi ya vita ya ujinga, umaskini na malazi.

Baba wa Taifa na Hayati Karume walituasa, ahadi za mapinduzi matukufu ya Zanzibar zinatekelezwa vipi na zimeunganishwa ndani ya siasa ya Chama cha Mapinduzi, mnasaidiaje kutekeleza hata wosia wa Baba wa Taifa, vita ya ukombozi wa Bara la Afrika ilikuwa ni madai ya ardhi, tulitembea tulifanya maandamano, tulitoa ujumbe dhidi ya ukaburu, je, hivi sasa ikiwa sisi wenyewe tuna tabia ya kutengeneza mikataba ya uchoyo kwa maslahi ya nchi, ardhi hii mnataka kuwapa hawa wawekezaji je, wawekezaji hao wakichukua ardhi bora baada ya miaka kumi tutakuwa milioni 60, wanafunzi wetu wanaohitimu katika vyuo watakwenda wapi, nilioni hilo niliseme.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Baba wa Taifa alisema na nimejaribu kufanya hivyo hoja yake, leo Tanzania tuko katika mfumo wa vyama vingi najifunza mengi sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kusema tena ma-*DC* wasaidiwe, nimesema CCM sitaki ife lakini CCM napenda vilevile kama haitaki kufa kujivua gamba basi watambue ya kwamba wanajukumu kubwa sana lakini napenda kuwakumbusha kujivua gamba si kuondoa kikwapa, kikwapa huondolewa na udi, ueni madhalia. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwenye masikio ya kusikia atasikia, ambaye hapendi kusikia shauri yake. Lakini napenda kusema mkia mdogo wa tembo huondoa uzia wa nzi kwenye mgongo wa tembo, vyama hivi viondoe uzia mbalimbali, kujivua gamba kuwe kwa faida. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa naomba nizungumzie suala ambalo nadhani ni la muhimu sana. Ukweli una tabia ya kuudhi kama nilivyosema. Ulimi huchonganisha na ulimi hupatanisha. Naomba Mheshimiwa Mwenyekiti na Mheshimiwa Waziri Mkuu kama nilivyosema, mpanue wigo wa kutusaidia kupata pesa za kutumia majimbo yetu. Ni aibu Jaji Mstaafu au Mbunge Mstaafu, hata Waziri akistaafu wanakuwa ni watu hohe

hahe. Makanisa na Misikiti huimiza matoleo ya sadaka, naomba na sisi mtusaidie kutuongezea matumizi yetu ambayo yahahitajika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna fedheha ya neno moja ambalo posho limeleta aibu sana, lakini naomba kusema ya kwamba tabia ya choyo ndiyo inayoleta malipo ambayo hivi sasa tunajikuta kwamba tunababaika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, posho ni neno ambalo lina karaha, lakini napenda kusema wakati wa mkoloni malipo haya yalikuwa yanaitwa ni ujira wa mwia, yalikuwa hayaitwi posho. Neno stahiki la Kiswahili kwa malipo anayolipwa *(professional allowances)* Wabunge, Madaktari wanapokuwa katika majukumu kama ya leo hayaitwi posho yanaitawa ni malipo ya ujira wa mwia. Kwa hiyo, tumieni Kiswahili fasaha, na mtu anayetaka kuangalia haya akaangalie kwenye Kamusi ndiyo hayo yaliyokuwa yanalipwa. Kwa hiyo, naomba stahiki za posho ambazo tunaziita posho sasa zibadilishwe jina ziitwe malipo ya ujira wa mwia. *(Kicheko/Makofi)*

Naomba na nashauri muondoe neno posho, muondoe ukungu potofu. Mwia ni malipo ya kulinda taadhima ya hulka na weredi wa kuitwa Mbunge, uhitajika huo usibughudhiwe na maneno ya utatanishi. Tanzania ni nchi pekee yenye viongozi wengi ambao wakistaafu wanakuwa hohe hahe. Vihoja vingi vya umaskini vya Watanzania kwa wastaafu vinavuruga uadilifu na imani ya Watanzania kuendelea na kwamba wasiwe na vishawishi. Ufisadi tunauzalisha wenyewe, *MP* maskini kutumikia watu maskini hawezi. Tutenganishe uwezo wa Mbunge mfanyabiashara na Mbunge maskini kwa sababu mfanyabiashara ana mahali pale pa kuchukulia visenti senti. Watanzania wote tuwe jeshi la fikra moja, tuwaenzi viongozi wetu, tutumikie viongozi wetu. Walafi wa ubinafsi wakipata utajiri hudharau maskini, tutafakari kila tunapojikuta kwamba binadamu ni vigumu sana kujituhumu ni mjinga au ni mpumbavu lakini ni hodari wa kutuhumu wenzake. *(Makofi)*

Nawaomba Watanzania tuepukanena taadhira hiyo, nasema hayo kwa sababu Mbunge maslahi ya jamii ni tofauti na Mbunge maslahi binafsi. Mbunge maslahi binafsi hana moyo wa kujitolea, hachangii misikiti, hachangii ujenzi wa makanisa, hatoi sadaka, hashiriki misiba, hachangii harusi, hashiriki *harambee* za kwaya, ngoma na misikiti, hachangii maulidi, hachangii vituo vya chekechea, hatembelei hospitali akasaidia dawa, hatoi sadaka, hachangii usajili wa vikundi mbalimbali, kwa hiyo, nasema malipo hayo yanaitwa ujira wa mwia. *(Makofi/Kicheko)*

Watanzania tutumie Kiswahili fasaha, naomba kuhimiza sana na naomba Waziri wa Utumishi achukue maneno haya na ayaandike ili Waziri wa Fedha, mtani wangu apate Kiswahili fasaha. Watanzania tutazidiwa na Kenya kwa sababu wanajua Kiswahili fasaha. Nasema ujira wa mwia utolewe. Mheshimiwa Waziri Mkuu, kuwa mti dawa uhakikishe ya kwamba tunaongezewa, ujira wa mwia tunaopewa hivi sasa hautoshi, inafaa tupewe shilingi 500,000/= hata kwa siku tuweze kuhimili matarajio ya Wtanzania. Kutofautiana kifikra ndiyo maana pakazaliwa *panadol extra*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kuyasema hayo ninaomba kumpongeza Mheshimiwa Edward Lowassa kwa jinsi alivyoweza kusema kwamba tuwe na maamuzi magumu. Sasa kukasirika mtu ni hisia binafsi kama unampenda mtu utamtafsiri vizuri, kama una chuki binafsi kwa hila zako hilo hatuwezi kumuepusha kwa sababu Mwenyezi Mungu katupa mitihani, kuna malaika na ibilisi. *Inshallah* Mwenyezi Mungu tujalie amani na utulivu malipo ya mwia yatoke haraka, yasifutwe. *(Makofi/Kicheko/Vigelele)*

**MWENYEKITI:** Namuita sasa Mheshimiwa Alphaxard Kangi Ndege Lugola.

**MHE. ALPHAXARD K. N. LUGOLA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi na mimi ili niweze kuchangia hotuba...

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, tumsikilize mwenzetu tafadhali.

**MHE. ALPHAXARD K. N. LUGOLA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi ili niweze kuchangia hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye Serikali yetu mengi yamesemwa kwamba imefanya mambo mengi na hata hapa tulipokaa sasa hivi jengo hili limejengwa na Serikali tunayoiamini. Serikali ikifanya mambo mazuri ni sawa na mtu akifanya mambo mazuri lazima atabarikiwa na Mwenyezi Mungu na siku zote baraka huandamwa na uzushi. *(Makofi)*

Naishauri Serikali pamoja na uzushi wa kila namna nje na ndani ya Bunge, kaza buti msikate tamaa, uzushi hauna mipaka. Hata juzi tu katika hotuba ya rafiki yangu Mheshimiwa Freeman Mbowe wakati anazungumzia mauaji ya Jeshi la Polisi, Waheshimiwa Wabunge wenzangu jambo hili linakuzwa. Wakati anaendelea kuchambua mauaji ya Jeshi la Polisi alipofika *paragraph* ya tatu akaanza kutaja askari mmoja wa magereza aliua watu fulani, huyo ni Jeshi la Polisi? Alipofika mbele kidogo akasema, askari wa wanyamapori tarehe fulani aliua mtu, huyo ni askari polisi? Nawashauri ndugu zangu kwa uzushi huu hata wale wenzetu wanaoliwa na mamba mtawaorodhesha kwenye mauaji ya Jeshi la Polisi. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nichangie moja kwa moja kwenye Bajeti ya Waziri Mkuu, lengo letu ni kutekeleza malengo ya milenia, Ilani ya CCM na mpango wa miaka mitano. Lakini mimi naona vipo vikwazo mbele yetu ambavyo vinahitaji kufanyiwa kazi ndipo siku ya siku tunaweza kupata maendeleo yanayotokana na hayo niliyoyataja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vikwazo hivi wengine huwa wanavitumia kama kejeli, polisi wanapokuwa maskini wanaambiwa ni kwa sababu walimkamata Yesu wakamuua, seremala anapokuwa maskini kwa sababu ya vikwazo wanamkejeli kwamba ni kwa sababu alichonga msabala Yesu akateswa. Lakini siku ya siku ni vikwazo ndivyo vinavyosababisha watu tuendelee kuwa maskini na tushindwe hata kutumia rasilimali tulizonazo kuondoa umaskini, ni vikwazo gani hivi? *(Makofi)*

Nianze na tatizo la rushwa katika nchi hii, rushwa ni kikwazo kikubwa sana, huwezi kufikia malengo katika nchi hii kama bado kuna rushwa katika nchi hii. Mwalimu aliwahi kusema kanchi haka kananuka rushwa. Tujiulize leo harufu hii imeondoka? Alituambia tangu Uhuru watu walichapwa viboko kwa kuchukia rushwa lakini mpaka leo tunapambana na rushwa, rushwa haiishi, tatizo ni nini? Wanaokula rushwa wapo, chombo cha kupambana na rushwa kipo, wananchi tunasaidia kupambanana rushwa, Bajeti tunapitisha kupambana na rushwa lakini rushwa bado ipo lazima mahali fulani kuna tatizo.

Tangu Uhuru rushwa ilipambanwa kupitia *special branch police* tukabadilisha jina ikawa *Anti Corruption Squad*, tukabadilisha jina tena ikawa *PCB,* tukabadilisha jina ikawa *PCCB,* majina yote yataisha lakini rushwa bado inaendelea. Inawezekana chombo hiki kina matatizo, inawezekana watendaji hawa ni wafupi wanashindwa kuwaona wanaokula rushwa kwa ufupi wao. *(Makofi)*

Katika Biblia kulikuwa na mtu aliyeitwa Zakayo alikuwa mfupi wa kimo, alipoona anashindwa kumuona Yesu na anataka kumuona alithubutu na kulazimika kupanda kwenye mbuyu na akamuona Yesu. Wakati umefika chombo hiki mpande mbuyu ili muwaone wala rushwa na muwakamate. Inawezekana pua zetu haziwezi kunusa wala rushwa, tunao mbwa wanaonusa hata wala rushwa watawakamata na kuwaleta mbele ya vyombo vya Sheria, tumieni mbwa hawa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, rushwa hii inahitaji uamuzi mgumu na inawezekana ni tatizo la mfumo ndani ya chombo hiki, Mheshimiwa Waziri Mkuu chombo hiki kitazame vizuri, kina matatizo mkifanyie kazi ndipo tutaondokana na rushwa.

Niende kwenye kikwazo kingine cha misamaha ya kodi isiyokuwa na tija ambayo imekuwa ni mingi mno katika Taifa letu. Tafsiri ya vivutio inatumika vibaya katika maamuzi, hivi kweli kama tuna madini, madini ni kivutio kwa yenyewe! Kama tuna ardhi nzuri ni kivutio kwa yenyewe! Kama tuna mlima mrefu kuliko yote Afrika unavutia kwa wenyewe! Hivi kweli lazima mtalii tumlipie nauli aje aone Mlima Kilimanjaro kwamba tunamvutia! Hivi ni kweli lazima mtu aje kuona mbuga zetu tumlipie tiketi aje kuona mbuga! Vivutio vinajivutia vyenyewe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niliwahi kumtania msichana mmoja enzi zile nataka kuoa kwamba kwa sura uliyonayo labda wewe ndiyo unitolee mahari ndipo nitakuona. Nilikuwa namwambia hivyo kwa sababu alikuwa havutii, lakini kitu kinachovutia kinajiuza chenyewe. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kweli kuwapa miaka kumi wawekezaji kwenye ardhi yetu ni kuwachinja Watanzania. Watu kuchimba madini wanatulipa 5% ni kuwachinja Watanzania, huku ni kuhamisha mali kwa Watanzania ambao ni maskini na kuwapelekea matajiri ambao tayari wametajirika. Hainiingii akilini badala ya matajiri kutuletea mali sisi ndiyo tunachukua mali tunawapelekea matajiri, hii haitawezekana. Haiwezekani wananchi wa Bunda maeneo yao yachukuliwe na *EPZ* kwa muda wa miaka kumi bila wananchi wake kupata kodi yoyote, huku ni kuwachinja Watanzania. Narejea maneno ya

Mwalimu wakubwa wameshasema hakuna, hakuna! Hatuwezi kuhamisha mali kutoka kwa maskini kupeleka kwa tajiri. Huu ni mfumo gani? Mfumo wa shetani huu. Aliuita mfumo wa shetani kwa sababu kazi ya shetani ni kuchinja na kuangamiza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tufike mahali tubadilike, tujaribu kurejea maamuzi tunayoyapitisha hapa Bungeni, turejee sheria zetu, tuwatetee Watanzania juu ya ardhi yao na madini yao. Ngoja niwaambie, pale kwetu kuna mnyama anaitwa nyamulimi, ma-*buldozers* yaliyopo Geita, vijiko vilivyopo Geita usiku na mchana wanachimba kama mnyama nyamulimi na kuchukua mali nyingi ya Watanzania lakini kwa sababu wanatudanganya kwamba utafiti kuna mali ya miaka 50 tunabweteka hatufikishi hata miaka 15 watakuwa wamemaliza mali yote na hiki ndicho kitakuwa kifo cha Watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, inatia uchungu sana kwani hatuwezi kukubali mali yetu inahamishwa inapelekwa katika nchi nyingine wanajenga maghorofa, wanajenga mpaka nyumba nyingine za dhahabu, hii ni kufuru kubwa kwa Watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, inasikitisha sana kuona Watanzania tunakuwa hatuna uchungu na mali yetu, tunaruhusu watu ambao wana utajiri wanaendelea kuchukua mali yetu na sisi tunatazama, jambo hili hatutakubali. Ninaomba Mheshimiwa Waziri Mkuu, katika hili turejeshe sheria zile ambazo kwa kweli zinatorosha utajiri wetu ili tuweze kuzifanyia kazi. Keki ya Taifa ni sawa na kuota moto, lazima Watanzania wote tuote moto kwa mduara, lakini mifumo hii ya kinyonyaji Watanzania tunaota moto kwa foleni, tunaota moto kwa mstari. Ni saa ngapi mnyonge aliyepo mwisho wa mstari atapata keki ya Taifa? Ni lazima tubadilike. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mwibara tuna kilio na vikwazo vingi vinatufanya tusiondoe umaskini, vinatufanya tuendelee kuwa na njaa wakati wote. Mimi namshukuru Mheshimiwa Waziri Mkuu tulishapata awamu ya kwanza kwa ajili ya kupambana na njaa, nakushukuru sana.

Lakini mpaka sasa tunanunua kilo nne za mahindi kipimo cha amboni kwa shilingi 3,000/=, debe moja tunanunua kwa shilingi 14,000/= bado Wanamwibara tuna matatizo makubwa na hasa tunaposikia wenzetu Rukwa wana mahindi ambayo hawana mahali pa kuyaweka, tunaomba kwa kweli mahindi haya kama Serikali haiwezi kutuletea basi ituruhusu watuletee magari Wanamwibara tupande twende tukachukue mahindi Sumbawanga. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kilio cha Wanamwibara hakisikiki kwa sababu wapo karibu na maji ya Ziwa Victoria, kila wanapolia machozi yao yanakwenda na maji ya Ziwa Victoria. Leo Mbunge wao nipo Bungeni nawalilia kilio hiki, machozi yanadondoka hapa na Serikali iko karibu na machozi haya, machozi ya Mbunge wao hayataenda bure. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi tunalima viboko wanaharibu mazao yetu, tukipambana na viboko tunachukuliwa hatua kwamba tunaua nyara za Serikali,

Wanamwibara twende wapi? Tunaona tukimbilie majini tuvue samaki tunaambiwa ni zana haramu, Wanamwibara twende wapi? Tunakimbilia kwenye pamba tunalima, Bunge la Tisa limepitisha Sheria ya kutowanyonya wakulima kwamba lazima wafanyabiashara wawe na mzani ambao siyo wa rula, unaowanyonya wakulima, lakini leo hii wakulima wanaendelea kunyonywa na mzani ambao ni haramu, kwa nini haramu ya makokoro inakamatwa na kuchomwa moto? Nataka kusikia Mheshimiwa Waziri Mkuu haramu hii ya mzani na wao waende wakamate mizani na kuichoma moto kwa sababu sheria inakataza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunapokuwa na mifugo tunaona kwamba tutafute malisho kwa sababu ya ukame, lakini tunapokaribia kwenye maeneo ya mbuga kwenye nyasi tunaambiwa hapa ni *buffer zone*, Wanamwibara twende wapi? Tunaambiwa tupunguze mifugo, hata ukipunguza mifugo wakabaki kumi, mifugo kumi haihitaji nyasi? Twende wapi Wanamwibara? Mbona wale walio na fedha benki hamuwaambii hela zao zimejaa benki? Inatia uchungu sana. Wanamwibara sasa hivi tunasema kwamba tukimbilie kwenye mita 60 za Ziwa Victoria tulime kilimo cha umwagiliaji, tunafukuzwa na *BMU* tunaambiwa kwamba tunaharibu mazingira lakini tunaambiwa wale wa mjini Sheria imetungwa imewakuta ni wakulima gani wa Mwibara ambao Sheria hii haikuwakuta? Inatia uchungu sana. Wanamwibara kuna umeme unapita unakwenda Ukerewe, ardhi yetu inapitisha umeme lakini sisi hatuna umeme, twende wapi tukalilie Wanamwibara?

Kuna mtoto mmoja anaitwa Magembe Ngia Alloys alivyoona kwamba haiwezekani umeme kupita nyumbani kwangu bila mimi kuutumia, alichukua waya na kuurusha juu ya umeme alikauka pale pale kwa sababu alikuwa na uchungu kwa nini ardhi yake ipitishe umeme asioutumia?

Mheshimiwa Waziri Mkuu naomba jambo hili ni muhimu sana, tupate umeme Mwibara kwa sababu hatuwezi kukubali umeme upite unakwenda Ukerewe bila sisi kuutumia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mwibara tunaweza tukafukuza njaa wenyewe kwa sababu maji ya Ziwa Victoria tunayo, tuna ardhi nzuri Ziwa Victoria, kwa nini tusiwekewe miundombinu ya umwagiliaji ili tupambane na njaa sisi wenyewe? Tutasubiri vyakula kutoka maeneo mengine mpaka lini Wanamwibara wakati ni miundombinu inatakiwa ili sisi tuweze kuzalisha wenyewe?

Mheshimiwa Waziri Mkuu kama jambo la mzani halitatolewa ufumbuzi hapa mimi sitakuwa tayari kupitisha Bajeti yako na pia kama Wanamwibara hatutapata chakula kutokana na bei iliyopo sasa hivi kuwa kubwa wafanyabiashara wanapewa chakula kwa ajili ya kusambaza kutoka kwenye ghala la hifadhi matokeo yake mnasikia mahindi yanapelewa Kenya, yanavushwa Sirari, wananchi wa Mwibara waende wapi?

Ninaiomba Serikali katika masuala ya msingi msiwe na utani, msibembeleze, Serikali yetu iwasimamie wananchi ili wasinyonywe na genge la watu wachache ambao wana mtandao katika nchi hii. Tutaendelea kuwasaidia Serikali, Bunge lipo nyuma yenu

kama chombo kikuu katika nchi hii kuisimamia Serikali. Msiogope, dhamira ya Bunge hili ni kuhakikisha kwamba wananchi wanakuwa ni namba moja katika kutatuliwa matatizo yao. Hakuna awaye yote chini ya jua atakayekinzana na Serikali isitekeleze malengo yake kwa wananchi wake. *(Makofi)*

Kuna watu wanataka kuendelea kuandamana mpaka kwenye majimbo yetu, mimi nawakaribisha waje waandamane tutawasaidia kuandamana kutoka asubuhi mpaka jioni, tutawasaidia kuwaletea hata taa na karabai kwa sababu hatuna umeme ili waandamane, lakini wajue kwamba maandamano siyo suluhisho la Watanzania katika matatizo yao. Suluhisho la matatizo ya Watanzania ni mipango mizuri ambayo tumeiweka hapa, ni Bajeti tunazozipitisha hapa na tunahitaji hali ya utulivu ili wananchi washiriki katika kuondoa matatizo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wapinzani walikuja na *operation sangara*, wakawadanganya Wanamwibara kwamba Mbunge wao anachapa usingizi na ninyi mna njaa haombi chakula kuja Mwibara. Lakini kuna mama mmoja akawauliza, ninyi ambao mnatuhurumia kwa njaa kwenye magari yenu kuna magunia mangapi tukashushe? Aaaaah! Waligeuka, walitafutana, walikwenda kuonania Bunda ndipo wakagundua kwamba pale wameondoka kwa mtawanyiko ambao hauna tija. Ndiyo sababu nakuwa jasiri kuwaaambia karibuni sana Mwibara mkaandamane. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimalizie jambo la mwisho ambalo ni kuendelea kuwaona Watanzania kama ni mbumbumbu na kama hawaelewi ni kutowatendea haki Watanzania.  Mwibara tulikuwa tunakwenda kusoma shule kilomita 20, lakini leo unakwenda karibu *zero distance* halafu unawaambia Watanzania kwamba nchi hii haina Serikali, miaka 50 hatujafanya kitu. Watanzania wa leo siyo Watanzania wa jana na mkiendelea kuwadanganya Watanzania siku watakapowaparamia pale Mwibara msinitafute mimi kama baunsa kuwasaidia. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana na ninaunga mkono hoja na Mheshimiwa Waziri Mkuu ayazingatie niliyoyasema. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, tuna chini ya dakika saba kutokana na Kanuni zetu itabidi tuahirishe kikao chetu na shughuli zote za leo mpaka kesho saa tatu asubuhi. *(Makofi)*

*(Saa 1.40 usiku Bunge liliahirishwa mpaka siku ya Jumatano, Tarehe 29 Juni, 2011 saa tatu asubuhi)*